

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI  
ZANZIBAR**

MHE.	ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5.	Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.	Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7.	Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8.	Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvu/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvubi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedalii	-	Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy-	-	Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellel - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

## Kikao cha Nne – Tarehe 26 Septemba, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

### DUA

*Mhe. Mwenyekiti, (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua*

### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Mswada wa Sheria ya Usimamizi, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Kuhakikisha Uwajibikaji wa Taasisi za Mafuta na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mwenyekiti Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Usimamizi, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Kuhakikisha Uwajibikaji wa Taasisi za Mafuta na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

### MASWALI NA MAJIBU

#### Nam. 119

**Rais wa Zanzibar Kufanya Ziara za Kushtukiza Katika Mahospitali**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-**

Ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kukagua Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili zimesaidia sana kuondoa kero ya upatikanaji

wa huduma duni na kuleta faraja kwa wananchi waliokuwa wakitaabika na huduma za afya.

- (a) Je, ni lini Mhe. Rais wa Zanzibar atachukua hatua za kufanya ziara za kushtukiza katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili kusaidia kuondoa kero za upatikanaji wa huduma kwa wakati, ukosefu au upungufu wa vifaa vyta uchunguzi pamoja na ukosefu wa dawa.
- (b) Je, ni lini ahadi ya Mhe. Rais kwa wananchi wake kutibiwa bure aliyitoa kupitia vyombo vyta habari tarehe 2/10/2015 wakati wa Kampeni za Uchaguzi itaanza kutekelezwa, ili kuondoa michango ya huduma inayoendelea kujitokeza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:**

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nichukue nafasi hii kwa kumpa pole sana kwa kipigo cha jana na bila ya shaka ni ishara nzuri kwa Oktoba 01.

Pia nawapongeza Wabunge wetu wa Yanga kwa kujenga heshima ya klubu yetu. Vile vile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa namna walivyooonesha umoja na mshikamano katika kuwajali na kuwafariji wenzetu waliopatwa na majanga mkoani Kagera. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo naomba sasa nianze kwa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na kutoa maelezo mafupi ya utangulizi. Viongozi wetu wana utamaduni wa kufanya ziara katika sehemu mbalimbali za Unguja na Pemba kwa utaratibu waliojipangia.

Ziara hizo ni pamoja na kukutana na wananchi katika maeneo wanayoishi, kukagua miradi ya maendeleo, kuhudhuria sherehe za kitaifa, kuitikia mialiko ya wananchi na taasisi mbalimbali na nyengine ni kufanya ziara za kushitukiza katika maeneo husika.

Kupitia ziara hizo, wananchi hupata fursa ya kuonana na viongozi wao na kuwaeleza changamoto zinazowakabili. Kadhalika, serikali huchukua hatua za kutatua changamoto hizo. Hata hivyo, maamuzi ya lini na wapi ziara hizo

zitafanyika hubakia kuwa ni maamuzi ya kiongozi husika kwa kutilia maanani lengo na nia ya ziara hiyo. (*Makofi*)

Maagizo ya maelekezo yanayotolewa na kiongozi katika ziara hizo, hufanyiwa kazi na kutekelezwa kama ilivyoagizwa au kuelekezwu hata kama ziara hiyo haikuwa ya kushitukiza.

Suala la kufanya ziara ni jambo linalozingatia mazingira na taarifa mahsusii kuhusiana na jambo husika. Aidha, ni imani yetu kwamba kila jema lenye maslahi na wananchi wetu serikali na viongozi wake tutalichukulia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Mwenyekiti, swali la lini Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein atafanya ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Naomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na mimi kwamba uamuzi wa kufanya ziara hizo tumuachie Mhe. Rais mwenyewe kufuatana na ratiba zake, sio tu katika eneo hilo, lakini sehemu au idara yoyote ya serikali iwe ziara au kuwaita wahusika. (*Makoti*)

Kila mwaka serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya uimarishaji wa vifaa tiba pamoja na madawa kwa lengo la kuimarisha huduma za kiafya nchini, ili wananchi wetu waendelee kuwa na siha njema.

- (b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mhe. Rais ametoa ahadi katika kipindi cha kampeni ikiwemo kutoa matibabu bure kwa wananchi, upatikanaji wa maji safi na salama, elimu kwa umma, amani, umoja na mshikamano.

Aidha, ahadi zake zote zinatekelezwa na serikali nzima kwa ujumla wake. Ni muombe Mhe. Mwakilishi tuendelee kuhubiri amani, ili wananchi wetu waweze kunufaika vizuri zaidi na matunda ya maendeleo ya Serikali yao ya Awamu ya Saba.

Kuhusiana na swali la dawa na huduma zote zinazotolewa kama huduma za kujifungua zitaendelea kutolewa bure, isipokuwa pale penye kasoro ya fedha au dawa husika, basi mwananchi anaweza kuchangia mwenyewe, ili kuimarisha huduma husika. (*Makofi*)

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Niungane na Mhe.Waziri na niendelee kumpa pole vile vile kwa kipigo alichokipata jana Shinyanga ambacho hakukitegemea, na kipovu kuona mwezi ni dalili nzuri kwa siku ya Jumamosi ya tarehe 01 Oktoba 2016, asumini zitaonekana Kikwajuni tena. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swalii moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mengi ya utoaji huduma za jamii yanakabiliwa na changamoto zinazotokana na uzembe na kukosekana kwa uwajibikaji na Mhe. Rais amekuwa akisisitiza sana kuhusu uwajibikaji hasa katika sekta ya afya.

- (a) Je, lini narudia tena Mhe. Rais atamshauri afanye ziara za kushtukizia katika maeneo muhimu ikiwemo *x-ray* na *Ultra Sound* na sehemu nyengine.
- (b) Mhe. Waziri, atakubaliana nami kuwa ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza imezaa matunda kwa serikali hii. Je, ni lini watafuata nyayo zake, ili kuona wananchi wanapata matunda yake na badala ya kuzungumza kwa mdomo tu vitendo vikawa havionekani, maana yake majibu ya serikali siku zote yanaonekana kwa mdomo na vitendo havionekani.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake ya nyongeza kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nadhani si busara kuwapambanisha viongozi wawili na wala sio hekima, na kila kiongozi na *philosophy* yake ya uongozi, pia kila kiongozi ana mpangilio wa utaratibu wake wa kazi. Kwa kweli, viongozi wote duniani lengo lao ni moja tu la kuwashudumia wananchi wanaowaongoza. (*Makofi*)

Imani yangu kwamba sote tulipo Zanzibar tunaridhika na mwenendo wa uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein. Busara, hekima na miongozo yake anayoitoa kwetu sisi wasaidizi wake pamoja na watendaji wa serikali tunaamini

kwamba tunafanya vizuri. Kwa kweli, nchi yetu ilipo sipo ilipokuwepo juzi, na tunaamini kwamba tutaendelea kusonga mbele vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la kwamba kuna uzembe, sitegemei kama kwenye serikali yetu kuna uzembe wa aina yoyote. Lakini kama kuna mapungufu ni wajibu wa serikali kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi, na wala hakuna ambaye atachukuliwa hatua na kuadhibiwa kinyume na taratibu na sheria za nchi hii. (*Makofii*)

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ninampongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudzi zake kubwa za ubinadamu anazozifanya katika nchi yetu, na mara nyingi husema kwamba anayekuteua amekuamini, maana wako wengi amewaona na amewaaacha, lakini kwa bahati mbaya katika mazingira yetu tunayofanya kazi kila mmoja na imani yake. Swali langu lipo hapa Mhe. Mwenyekiti.

Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ni tegemeo au ni kimbilio la wanyonge anayekutwa na shida yoyote lazima aelekee huko kwa ajili ya kutafuta usalama wake na afya yake kuwa bora. Lakini kwa bahati mbaya kuna mazingira unaweza kuyakuta ukashtuka hasa wanapokwenda wagonjwa wetu mbalimbali kufika kule tunataka kipimo fulani akaambiwa hakipo na kuambiwa aende *Al-Rahma* au *Global Hospital*.

Je, hapa Wizara ya Afya ina mpango gani kuhakikisha hospitali ya rufaa inawanufaisha wananchi wake kwa usalama wao na afya zao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kweli, Mhe. Mjumbe anataka kujuu mipango ya serikali kwa kupitia Wizara ya Afya juu ya uimarisaji wa huduma za hospitali yetu ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi hapa kwamba tumepitisha sheria mbili katika kipindi ambacho sio kirefu sana, mionganoni mwa azma ya kupitisha sheria mbili zile ni kuimarisaji na kuisukuma mbele serikali yetu na hasa

Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, ili kufikia katika malengo hayo ya kuwa hospitali ya rufaa.

Kwa maana hiyo, ili tuweze kufanya kazi vizuri, lazima chombo kile kiwe na nguvu za kisheria. Malengo ya serikali ni kuanza misingi mizuri ya kisheria na baadaye tuweze kutafuta fedha, miundombinu, vitendea kazi pamoja na vifaa tiba, kwa ajili ya kuimarisha huduma hizo kwa lengo la maslahi mazuri na huduma kwa wananchi wetu wote wa Zanzibar.

Kwa hivyo, mipango ya serikali iko vizuri, na tayari tumeshaanza *foundation* ya kutengeneza sheria, vifaa tiba pamoja na vitendea kazi vyengine vitaendelea kutafutwa, kwa ajili ya kuimarisha huduma hizo za afya kwa wananchi wetu wa Zanzibar. (*Makofit*)

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya leo. Naomba niungane na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba Rais hawezi kukopia Rais mwengine kwani kila Rais ana lengo na madhumuni makubwa ni kuwaaletea maendeleo wananchi wake anaowaongoza.

Mhe. Mwenyekiti, swalı langu ni kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 24 Aprili, 2014 aliwatembelea wananchi wangu wa Welezo Wadi ya Mtifaani. Kwa kweli, hali ya barabara yao aliikuta mbovu na kwa kuwaonea huruma na kuwapenda wananchi wake hasa wanawake wanajifungulia njiani. Kutohana na hali hiyo, Mhe. Rais aliagiza agizo la kimapinduzi kwamba wananchi wale barabara yao itengenezwe, lakini masikitiko yangu makubwa, kwamba agizo hilo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kimapinduzi mpaka leo bado halijatekelezwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, naomba uulize swalı.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba, ni lini agizo hilo la kimapinduzi la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi litatekelezwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kumjibu Mhe. Mwakilishi swalı lake ambalo anataka kujua baada ya ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar ya tarehe 24 Aprili, 2014 lini itatekelezwa kuhusu maelekezo au maagizo ambayo aliyatoa Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa serikali ni kwamba kiongozi anapoagiza taasisi au wizara husika wanalichukua agizo la serikali na kuliingiza katika mipango ya serikali, ili utekelezaji wake uende vizuri. Kwa kweli sote tunajua kwamba utaratibu wa serikali kwa ajili ya kutekeleza mambo yake ni lazima jambo lipangiwe fedha na fedha tunapitisha sisi hapa.

Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba Wizara husika ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi jambo hilo itakuwa wamelichukua na kuliingiza katika mipango yao na bila ya shaka yoyote yatafanyiwa kazi. Kwa mfano, inawezekana kwamba ikawa wameshindwa kulitekeleza katika mwaka husika na wataliingiza katika mwaka unaofuata kutokana na *allocation* ya fedha, lakini pamoja na vipaumbele veya miradi ambavyo wamelenga.

Utaratibu wa serikali ni kwamba kila ambalo linaagizwa na Kiongozi Mkuu, lazima wizara ilichukue na kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niombe kwamba ahadi za Mhe. Rais hatutekelezi kwa mwaka mmoja, kwani ahadi zake ambazo alizozitoa wakati wa kipindi cha kampeni na kipindi cha utekelezaji ni muda wa miaka mitano. Kwa hivyo, tuendelee kuvuta subira, na kwamba yaliyoahidiwa yatakelezwa na kupata matunda mazuri zaidi kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofi*)

## Nam. 160

### Kuongezeka Makosa ya Jinai Watoto

**Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:**

Hivi karibuni kumeibuka wimbi kubwa la watoto kufanya makosa ya jinai bila ya kujitambua.

- (a) Je, ni watoto wangapi wamekekwa rumande kwa mwaka 2015/2016 kwa tuhuma mbalimbali.
- (b) Je, ni watoto wangapi wametiwa hatiani katika kipindi hicho.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kumjibu Mhe.

Mwakilishi swali lake Nam. 160 lenye kifungu (a) na (b). Lakini kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 imeeleza kwamba mtoto ni binadamu yejote ambaye hajafikisha umri wa miaka 18 toka kuzaliwa. Hivyo, chini ya sheria hiyo kumeundwa Mahkama ya Watoto ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwafikisha watoto ambao wanatuhumiwa kwa kufanya kosa lolote la jinai, isipokuwa mauaji ya makusudi, mauaji ya kutokukusudia, kubaka na uhaini.

Aidha, Mahkama hiyo ina jukumu la kuwashughulikia watoto wote wanaofikishwa mahakamani kuhusiana na kesi zinazohusu matunzo na malenzi yao.

Baada ya ufanuzi huo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2015/2016 hakuna mtoto yejote ambaye alipelekwa rumande kutokana na kutuhumiwa kufanya kosa la jinai. Hata hivyo, kifungu Nam. 45(1) cha Sheria ya mtoto kinasema kwamba mtoto yejote atakayefikishwa mbele ya Mahkama hiyo kwa ajili ya kushtakiwa, Mahkama inatakiwa kumwachilia kwa dhamana mtoto huyo na awe katika matunzo ya mzazi, mlezi au mtu mwengine yejote ambaye anaonekana anafaa. Jambo ambalo Mahkama inatakiwa kuzingatia wakati wa kumpa dhamana mtoto ni kuangalia iwapo mtoto huyo anaweza kuhudhuria Mahakamani kusikiliza kesi yake, kwa mtoto ambaye atakosa mtu au mlezi wa kumchukulia dhamana katika kesi, jukumu la kumchukulia dhamana limewekwa katika Afisi ya Ustawi wa Jamii.
- (b) Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2015/2016 jumla ya watoto kumi na moja (11) kati ya waliofikishwa Mahakamani kwa kutuhumiwa na makosa mbalimbali walipatikana na hatia na kupewa adhabu ikiwemo kulipa fidia, onyo kali, kushiriki kituo cha kurekebisha tabia na pia kulipia faini.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana. Pamoja na mazuri sana ya Serikali marefu lakini yasiyo na uhakika naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi au watoto mpaka sasa wamo Gerezani, na kwa kuwa kuwachanganisha watoto wadogo na wakubwa katika Gereza moja inaweza kupelekeea wigo mkubwa sana wa kuiga yale matatizo ya watu wakubwa. Serikali ina mpango gani kwa sasa kujenga Gereza la Watoto.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli suala la kuchanganya watoto na watu wazima hata katika hali ya kawaida, hata nyumbani inakuwa haipendezi. Lakini suala hilo tunalo na tumekuwa tukilififikiria namna gani kuweza kufanya kazi ili kuwatofautisha hawa watoto na watu wazima.

Kwa hivyo wazo lako na ushauri huo na tunaofanya kazi hatujakaa kimya tu, lakini lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba suala hilo linafikiwa muafaka kwa utekelezaji mzuri. (*Makofî*)

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali ambayo ameyatoa.

Hivi sasa katika Vyuo vyetu vya Mafunzo hasa kwenye Gereza la Kilimani tumetenganisha sehemu ya kukaa mahabusu na wafungwa; watoto na watu wazima. Hata hivyo, kwenye bajeti hii tunayokwenda nayo ya mwaka 2016/2017, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Gereza la Watoto kule Hanyegwamchana. Na tayari hivi ninavyosema mwezi huu tumeanza kupata milioni mia moja kwa ajili ya ujenzi huo wa Gereza la Watoto kule Hanyegwamchana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba niulize swalii la ziada kwa Mhe. Waziri Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora lenye vifungu (a) na (b).

- a) Ni lini hayo mahabusu ya hao watoto yamatimaliza kujengwa.
- b) Wizara yako imetembelea lini kuona mazingira ya hao watoto huko mahibusu yako vipi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nadir swalii lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Kwanza kwa kadri ya hali tuliyonayo tumejaribu sana kurekebisha hali ya eneo kupitia *Save the Children*, kuweka mazingira mazuri kwenye sehemu ambayo tunawatunza watoto hivi sasa pale Kilimani. Nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru pia na kuwapongeza *Save the Children* kwa kutusaidia kwa ajili ya kupunguza tatizo hilo. Lakini ni lini tatizo hilo litaondoka.

Tatizo hili litaondoka pale tu Serikali itakapokuwa imekamilisha fedha ambazo tumezitenga kwa ujenzi wa Gereza hilo. Ni imani yangu kwamba kwa mwaka huu tumetenga kiasi cha shilingi milioni 250 tuaanza na mwakani tutaweza kutenga fedha nyengine ili kukamilisha ujenzi huu wa Gereza la Watoto na hasa tukizingatia kwamba magereza ambayo tunayotaka kuyajenga sasa ni tofauti na yale ambayo yaliyojengwa zamani. Mhe. Mwenyekiti, tunayajenga kisasa, yenye *facilities* zote kwa ajili ya huduma za kibinadamu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kwanza tutambue ugeni wa Mhe. Spika kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Wageni wenywewe ni kama hawa wafuatayo:-

1.	Mhe. Job Ndugai	-	Spika
2.	Ndg. Raphael Nombo	-	Kaimu Katibu wa Bunge
3.	Ndg. Said Yakub	-	Msaidizi wa Mhe. Spika
4.	Ndg. Michael Ndofu	-	Mkurugenzi Utawala na Raslimali Watu

Waheshimiwa wageni karibuni sana. (*Makofit*)

## Nam. 81

### Vitenda Kazi Kwa Manispaa za Magharibi ‘A’ na ‘B’

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza:-**

Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Maalum vya SMZ inastahili pongezi kwa kuanzisha Manispaa Mpya za Magharibi “A” na Magharibi “B”. Kwa kuwa Manispaa hizo zimeanzishwa na lengo la Serikali kuongeza maendeleo kwa wananchi.

Je, Wizara imejiaandaa viyi juu ya vitenda kazi kwa Manispaa hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 81 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika kuhakikisha kuwa kila Baraza la Manispaa linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria namba 7 ya mwaka 2014 katika eneo lake la kiutawala "*Area of Jurisdiction*" imechukua hatua mbali mbali zikiwemo:-

1. Kuwaagiza Makatibu Tawala wa Wilaya za Magharibi "A" na "B" washirikiane na Makaimu Wakurugenzi wa Manispaa hizo katika kusimamia mapendekezo ya mgawanyo wa rasilimali watu, vitu na fedha zilizokuwa mali za Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi.
2. Aidha, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imo katika kusimamia na kutekeleza mpango wa Ugatuvi ambao ndio utakaoleta mageuzi makubwa katika Serikali za Mitaa. Ugatuvi huo utapelekea kuwa na watumishi wenye ujuzi kwa kuwawezesha kitaaluma na kuwa na zana bora za kufanya kazi.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Kwanza ninampongeza kwa dhati Mhe. Waziri kwa juhudini yake ya kuhakikisha kwamba miji yetu inakuwa katika mazingira mazuri na ya maendeleo pindi unapopita kwa usalama wako na mali zako.

Nikichukulia hilo Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Waziri haya yafuatayo kwa ufupi sana.

Je, kwa kuwa maeneo yetu yana mipaka mbali mbali au miundo mbali mbali kwa ajili ya kero. Kwa mfano, katika eneo la Meli Nne Uzi yaani daraja la Uzi, kuna mtaro ambao unahatarisha maisha ya watu siku za mvua. Lakini aidha kuna mtaro mwengine wa Nyumba Mbili kwa Chunda penye daraja kama hilo la Uzi, nalo linahatarisha maisha ya watu kutokana mvua zinazonyesha.

La mwisho katika hilo nataka kumwambia tu Mhe. Mwenyekiti, kutoka Msikitii wa Taveta kama unakwenda Magirisi pana jaa ambalo siyo rasmi ni kero kwa afya za watu wetu, na hatari mvua zinaponyesha kwa usalama wa maisha yao.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa mgao huo wa zana za kazi zinapangwa, na kero hizi zinaendelea katika jimbo langu kwenye maeneo ambayo niliyomtajia. Mhe. Mwenyekiti, kwa dharura atanisaidia vipi kuliondoa jaa hilo na kujengi mitaro

hiyo ili maji yaondoke wakati wa mvua twende salama kwa watu kwenye maisha yao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swal lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema mwanzo kwamba Mabaraza haya ya Manispaa ya Magharibi "A" na "B" na yeze nina imani Baraza la Manispaa linalomuhusu ni lile la Magharibi "B", lipo katika utaratibu wake hivi sasa wa kushughukia utendaji wake wa kazi kwenye mipaka yake ya kiutawala.

Ninataka nimuhakikishie kwamba Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya kwisha kumaliza kujipanga vizuri Baraza la Manispaa la Magharibi "B" litaweza kuchukua hatua katika kushughulikia madaraja hayo mawili ambayo ameyasema pamoja na kuondosha jaa ambalo linahatarisha maisha ya watu.

Nataka nimuhakikishie na wahakikishie wananchi wa Kijitoupele kwamba si muda mrefu Baraza litafanya kazi hiyo ya kuweza kuyashughulikia matatizo. Kwani nia ya uundwaji wa Mabaraza haya ni kuwahudumia wananchi ili kuweka mazingira salama katika miji yetu.

Ahsante sana. (*Makofî*).

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri katika majibu amesema katika mgawanyo wa Manispaa hizi mbili ya Magharibi "A" na "B" watapata mgawanyo wa mali pengine na wafanyakazi ili kuendeleza shughuli za majukumu yao kama ambavyo Serikali imetoa matarajio kwa wananchi wake.

Ni lini utaratibu wa mgawanyo huu wa wafanyakazi na mali kama magari utakamilika ili shughuli ziende vizuri ili tusije tukapata tatizo kwa Manispaa moja huduma zinakwenda na moja haziendi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swal lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Hivi sasa Serikali inafanya zoezi la kutambua mahitaji ya wataalamu na wafanyakazi kwenye maeneo yote ya Manispaa za Magharibi "A" na "B"

pamoja na Halmashauri zote nchini. Pale Serikali itakapokamilisha utaratibu huu itafanya utaratibu wa kuweza kuwaganya wafanyakazi. Kwanza waliopo katika taasisi hizi lakini pili kuwahamisha kutoka sekta nyengine za Serikali na kuwapeleka katika Manispaa hizo. Kwa hivyo mara tu baada ya zoezi hilo kukamilika basi wafanyakazi hawa watahamia kwenye taasisi au Manispaa husika.

Lakini kuhusu utaratibu wa kugawanya mali ni kwamba tunachozungumzia hapa ni mali ziliopo katika Manispaa Magharibi "B" ambayo ilikuwa ni Halmashauri, na vile vile mali nyengine ambazo zipo katika mipaka ambayo ipo katika Halmashauri au katika Manispaa hizo. Kwa hivyo pale tu tutakapomaliza kazi hiyo, ninapenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mali hizo zitagawanywa ili Manispaa hizi ziweze kutekeleza wajibu. Si muda mrefu tutakamilisha hasa kwa kutambua Sheria ya Fedha baada ya kukaa na Wizara ya Fedha na Mipango, tutaweza kupambanua mali gani iende katika Manispaa gani na mali gani iweze kwenda katika Manispaa gani.

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuniona kwa kuweza kupata kuuliza swali la ziada katika swali mama.

Mhe. Waziri kama unavyofahamu azma kubwa ya Serikali ni kulinda na kusimamia Sheria za nchi hii. Je, si muda mkubwa uliopita mwaka jana Wizara yako ilitangaza Manispaa mbili ya Magharibi "A" na "B" bila ya marekebisho ya sheria na Katiba ya nchi hii.

Je, huoni kwamba Serikali inavunja sheria zake wenyewe iliyotunga. (*Makofî*).

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza Serikali haijawahi na haitovunja sheria za nchi ambazo zimepitishwa na Baraza hili la Wawakilishi. (*Makofî*)

Na pale tu kwa utaratibu wa kawaida wa kiserikali dunia nzima, pale ambapo sheria inaonekana ina mapungufu ya utekelezaji wake, ndipo hapo Serikali huchukua hatua ya kufanya marekebisho kwa kuuleta ndani ya Baraza la Wawakilishi kama tulivyofanya kwenye Sheria Nam. 7 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo tumeipitisha juzi tu hapa iliyowasilishwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu. (*Makofî*)

## Nam. 167

### **Muitiko wa Wafanyabiashara Kutumia Mashamiana ya Sikukuu**

#### **Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza:-**

Katika kusherehekeea sikukuu ya Idd-el-Fitr, uwanja wa Mnazi Mmoja, Baraza la Mji lilijenga maturubali au mashamiana mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara mbali mbali, kwa ajili ya kuweka mazingira safi na salama.

Je, ni muitikio gani uliopatikana juu ya wafanyabiashara wetu, kutumia mashamiana hayo.

#### **Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 167 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kusherehekeea sikukuu ya Idd-el-fitri mwaka huu, Baraza la Manispaa ya Mjini lilijenga mashamiana ya kuuzia biashara katika uwanja wa Mnazi Mmoja. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kuweka mazingira mazuri ndani ya njii wetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi walilipokea suala hilo katika mtazamo tofauti, ambapo wengi wao wameliunga mkono Baraza kuwa sasa lina nia thabiti ya kutunza mazingira ya Mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha wananchi wengine walilalamika kuwa gharama za kupata nafasi ya kufanya biashara ni za juu. Hata hivyo, Baraza lilizingatia kilio hicho na kupunguza gharama hizo ili wananchi wetu wafurahie sikukuu kwa salama na katika mazingira bora.

Aidha, Baraza litaendelea na mpango huu huku ikipanga utaratibu wa kununua mashamiana hayo, ili mpango huo uwe endelevu si kwa Mnazi Mmoja tu bali na viwanja vyengine vya skukuuni.

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata):** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Narudia tena Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuangalia hali halisi ya nchi yetu na miji yetu yawe katika hali nadhifu juu ya usalama wa watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia wengi kwamba kipindi hiki cha sikukuu katika kiwanja cha Mnazi Mmoja baada ya kumalizika ile sherehe, hukuikuta karatasi yoyote katika uwanja ule. Natoa pongezi kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, swali langu Mhe. Waziri kanijibu, lakini nitamuuliza kwa vyengine tu, alisema sio kuondoa kiwanja cha Mnazi Mmoja peke yake, lakini na viwanja vyengine kama Kibanda Maiti na vyengine. Je, kwa kuwa viwanja vyetu viko vingi sasa, kwa mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele, Taveta, Uwanja wa Magirisi, maeneo yale vijana wetu na watoto wetu wanakuwa salama katika kutekeleza kazi kama hiyo, ana mpango gani wa kuangalia katika majimbo mbali mbali kwa usalama wa vijana wetu kuwawekea maturubali kwa usalama wao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya wenzangu watumishi wote wa Baraza la Manispaa ya Mjini tunazipokea sana pongezi zake kwa kazi ambayo tumeifanya.

Serikali ina mpango gani wa kuweza kueneza huduma hizi katika jimbo lake. Nataka niseme kwamba nia ya serikali na nia ya Baraza la Manispaa ni kutoa huduma nzuri kwa wananchi zinazoendana na wakati wa sasa na kujenga au kuweka mazingira bora ya usafi ndani ya miji yetu. Kwa hivyo, kwa kuwa jambo hili tumelianza katika viwanja vya Mnazi Mmoja, na kama nilivyosema na kuahidi katika bajeti yangu ya mwaka huu wa 2016/2017, hatua kwa hatua tutaendelea manispaa zote na halmashauri kujenga mazingira mazuri ya kujenga mashamiana badala ya kujenga magunia, ili tuweze kutunza mazingira yetu.

**Mhe. Shehe Hamad Mattar:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii. Kwanza naipongeza sana wizara kwa kuititia Baraza la Manispaa katika kuamua kuvibadilisha viwanja vyetu hivi na kuweka mfumo huu mpya, nazipongeza sana. Lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa sababu katika msimu uliopita wa Skukuu ya Iddi El Fitri, kulikuwa kuna manung'uniko makubwa sana kwa baadhi ya wafanyabiashara, kwamba malipo yalikuwa makubwa, lakini vile vie malipo yalitofautiana, wengine walilipa shilingi 110,000/- na wengine wakalipa chini ya hapo.

Je, ni sababu zipi zilizosababisha wengine kutolipa bei ambayo imepangwa kukawa kuna manung'uniko kama hayo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kulikuwa kuna manung'uniko ya wafanyabiashara ambao walitumia kufanya biashara zao katika viwanja vya Mnazi Mmoja.

Ni kweli kabisa bei ya mwanzo ambayo ilikuwa imepangwa ya kuwakodisha wananchi katika viwanja hivyo ni shilingi 110,000/- kwa wafanyabiashara wa *toys* na kwa wafanyabiashara wa chakula ilikuwa ni shilingi 100,000/-.

Baada ya manung'uniko serikali kwa kupitia Baraza la Manispaa, ilichukua hatua ya kuwapunguzia ada hiyo wafanyabiashara. Kwenye maeneo ya *toys* walipunguziwa hadi shilingi 90,000/- na kwenye maeneo ya chakula walipunguziwa hadi shilingi 80,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo hakukuwa na mtu ambaye huyu alipewa bei hii na huyu alipewa bei hii, isipokuwa ilichukuliwa hatua ya kuwapunguzia wafanyabiashara hao. Lakini kwa wale ambao walishalipa, maana yake fedha hizo zilishaingia kwenye mfuko, isingekuwa rahisi tena kuweza kuzirejesha kwa sababu risiti tayari zilishatolewa, na kama tungezirejesha tungkuja kupata *audit query* baadae, lakini shughuli ilikwenda salama na serikali ilisikiliza kilio cha wananchi. (*Makofi*)

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa fursa kila mwananchi uwezo wa kwenda kuishi, kutembea mahala popote, na sherehe ya Iddi ni katika sherehe muhimu katika nchi yetu na wananchi wetu wote hufaidika na hupenda wote kusherehekeea kwa pamoja.

- (a) Je, ni kwa nini Mzanzibari anakosa fursa ya kwenda kutembelea ndugu zake kwa kutumia usafiri wa gari kwa kupakia kwenye meli ili aweze kusherehekeea sherehe ya Iddi huko Tanzania Bara.
- (b) Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la viwanja ambalo Mhe. Waziri ameliongelea, vijana wengi, kina baba na kina mama wamekuwa wanatoka Mkoo wa Kusini kuja mjini. Je, serikali haioni kupanga utaratibu mpya wa kuweza kuhakikisha mwaka ujao, ili wananchi wote wa Mkoo wa Kusini waweze kusherehekeea sikukuu

yao kwa pamoja huko huko ili kupunguza msongamano uliopo. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza serikali daima itaendelea kuzitii katiba zake zote mbili; ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Zanzibar. Kwa kufanya hivyo maana yake kila mwananchi anayo fursa ya kuamua kwenda anakotaka na hasa wakati wa skukuu kusheherekeea pahala anapotaka. Sasa suala la serikali ina mpango gani, ningemuomba Mhe. Mwakilishi juu ya suala hasa la meli, suala lake angelipeleka kwenye Shirika la Meli na Uwakala, ili wakaweka ratiba maalumu kwa wakati wa skukuu kuwawezesha wananchi kwenda Pemba, Dar es Salaam na kwengineko.

Vile vile suala la usafiri wa magari mpaka sasa hivi sekta ya magari ni sekta binafsi, kwa hivyo ni jukumu letu kuwashajihisha wananchi waweze kuelewa umuhimu wa shughuli hii ili waweze kuwapeleka wananchi kule ambapo wanataka. Serikali ina mpango gani kuhusu suala la kuvitengeneza viwanja vya Mkoa wa Kusini navyo kuvifanya kuwa na *facility* kama zile za Mkoa wa Mjini. Jukumu hilo tutawaelekeza Halmashauri za Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini, ili waweze kujenga mazingira bora, ili na wananchi wa Mkoa wa Kusini nao waweze kufaidika, kwa sababu haya yanayofanyika katika manispaa hizi ni ya manispaa hizi, na yale yatakayofanyika nje ya manispaa hizi yatakuwa ni ya Halmashauri katika Mkoa husika. Ahsante sana.

## Nam. 80

### **Maiti ya Mtoto Mchanga Kuchelewa Kukabidhiwa Jamaa Zake**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swalii langu namba 80, kwanza nichukue fursa hii kuwapa pole waathirika wa tukio hilo, akiwa Bi Halima yuko hapo juu hivi sasa kaja kusikiliza suala lake hili. Nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada alizochukua kwa dhati katika Wizara ya Afya.

Kuna harufu nimeisikia Mhe. Waziri atakuja kunithibitishia kwa niaba ya wananchi kutoa bilioni 1.6 kwa suala la madawa, ndio pale tunapopiga kelele, mtu mzima akilia kuna jambo...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, naomba uulize swalii.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali hivi sasa itoe jawabu muafaka kwa swali langu namba 80.

Hivi karibuni imeripotiwa na vyombo vya habari mbali mbali nchini kuwa kumefanyika uzembe katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, ambapo maiti ya mtoto mchanga iliwekwa muda wa siku tatu mpaka inaanza kutoa harufu ndipo wamekabidhiwa jamaa zake baada ya kusumbuliwa kwa muda mrefu.

- (a) Je, hadi hivi sasa hatua gani zimechukuliwa kwa waliohusika na uzembe huo.
- (b) Je, hatua gani zimechukuliwa ili kuhakikisha kuwa uzembe kama huo hautokezei tena.
- (c) Kwa kuwa mzazi wa mtoto huyo alijifungua kwa operesheni, na kwa kuwa mzazi huyo alipata matatizo makubwa ya kisaikolojia kutokana na tukio hilo. Je, wizara ipo tayari kumpa fidia kwa athari za kisaikolojia alizozipata pamoja na familia yake.

**Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa hapa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kuwa na afya njema na uzima.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Lakini kabla sijamjibu Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo niweke sawa maelezo yaliyotolewa kwenye swali hilo.

Kwanza kabisa ni kweli tukio hilo lilitokea mnamo tarehe 18/07/2016, lakini sivyo kama hivi liliyoutolewa kwenye swali, nitalitolea maelezo lilitokea vipi. Katika uchunguzi wa kina uliofanyika kwa timu mbali mbali, ikiwemo timu ya nidhamu, timu ya wauguzi, timu ya madaktari Mnazi Mmoja.  
Uchunguzi huo umebaini yafuatayo:-

Mzazi alipowasilishwa hapo *maternity ward* Mnazi Mmoja alikuwa kweli katika hali mbaya na alikuwa anahitaji kufanyiwa operesheni, baada ya kuwasilishwa tu pale na madaktari walikuwa wanamshughulikia, bahati mbaya sana mume wake mzazi huyo hakuacha jina lake wala namba yake ya simu kwenye kitabu. Kwa hivyo, hilo lilikuwa tatizo la kwanza, uchunguzi wetu umebaini hilo.

Lakini la pili, kuna utaratibu ambao umepangwa mzazi akishafikishwa tu pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuna sehemu muuguzi wake anatakiwa aende akaripoti kwenye ofisi hiyo maalumu. Sasa muuguzi yule ama mume wake kwa wakati huo kwa ripoti zetu zinavyotwambia, alielezwa aende akawasilishe baadhi ya vifaa vinavyotakiwa pamoja na jina na namba ya simu, lakini hilo nalo halikutokezea. Nafikiri ilikuwa ni muhama aliokuwa nao yule muuguzi.

Na la tatu, jamaa hao ama jamaa huyo mume wa huyo mzazi baada ya kutoacha namba zake za simu, na baada ya madaktari na wauguzi kuhangai kwa muda mrefu sana kumtafuta halikupatikana hilo.

Tatizo lililotokea kwa upande wetu wa Wizara ya Afya, na hili naomba nikiri, ambalo limechukuliwa hatua za kinidhamu katika kujibu kifungu (a) (b) na (c). Tatizo lililotokezea kwa upande wetu wa Wizara ya Afya, kuna kanuni inayosema mtu akishafariki tu, maiti yeoyote ikiwa ya mtoto mchanga, kijana au ya mtu mzima basi maiti ile inatakiwa ipelekwe *mortuary* moja kwa moja, kama jamaa zake hawapo pale panapohusika. Hata ajali inapotokeza kokote, maiti ile kwanzia inatakiwa ifikishwe *mortuary* moja kwa moja inafanyiwa uchunguzi na baadae kupewa jamaa. Lakini mtu anapofariki ndani ya wodi, jambo la mwanzo kama jamaa hayupo karibu ama kile cheti hakijatolewa, basi maiti yule anatakiwa kupelekwa *mortuary*.

Mhe. Mwenyekiti, uzembe uliofanyika ni kwamba maiti ile haikupelekwa *mortuary* na *shift* zote tatu. Kwa hivyo, tulichokifanya sisi kutokana na hali ya mgonjwa kuwa mbaya na alipelekwa *ICU* baada ya hapo, na zile *shift* zote tatu hazikupeleka maiti ile *mortuary*, kila *shift* ilipokuja ilijua kwamba atakuja mtu wake maiti kuja kuchukua, kila *shift* ilipokuja ikajua hivyo. Kwa hivyo, maiti ile ikakaa pale kwa muda wa siku tatu.

Mhe. Mwenyekiti, tulichokifanya sisi na hii ni adhabu ya mwanzo kutolewa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, tumewapa onyo wafanyakazi wote 9 wa kila shift, yaani 9 x 3 ni 27, wamepewa onyo kali na onyo la kimaandishi. Baada ya hapo limetolewa dokezo maalumu kwa hospitali zote, maiti inapotokea haina mwenyewe pale pale ndani ya saa 12 inatakiwa ifikishwe *mortuary*, dhamana ya pale inakuwa sio ya wale wauguzi ama hospitali zile, bali ni ya *mortuary* moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupitia vifungu vyote vya kisheria, baada ya kupitia sheria ya utumishi na kuchukua hatua hizo za kinidhamu, kutokana na kifungu cha 83 cha sheria ya utumishi, na baada ya kufanya uchunguzi wote wa kina, Wizara imeona kwamba kosa hili ni la pande mbili, upande mmoja ni la wazazi

ambao hawakuja ku-*claim* maiti yao wala hawakuacha namba ya kutafutwa wala taarifa yoyote.

La pili, ambalo limeshachukuliwa hatua ni la wafanyakazi wetu, hakukuwa na haja yoyote ya kutoa fidia kwa familia. Ahsante. (*Makofit*)

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitangulize kusema *Innaa lillaahi Wainnaa ilayhi Raajiu*.

Waheshimiwa Mawaziri nawaombeni radhi sana, na sio ujinga kuomba radhi. Mhe. Waziri kule Mhe. Haji Omar Kheri. Serikali mkiambiwa wazembe huu ndio uzembe wenu nakuthibitishieni.

Mhe. Issa Gavu waziri katoka sasa hivi hapa kasema hii serikali sio zembe, lakini huu ndio uzembe kwa kosa hili lililotokea. Mgongwa kachukuliwa kutoka Hospitali ya Mwembeladu kaletwa pale na huku Mhe. Rais keshatangaza huduma bure, si uzembe huu. Mtu maiti inafika kuoza siku tatu inatoa harufu ni uzembe gani huo. Kama halitoshi hilo

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, naomba uulize swali la nyongeza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ngoja Mhe. Mwenyekiti. Katoa maelezo Mhe. Waziri na mimi nifanyie haki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, maelezo aliyotoa Mhe. Waziri yалиhusiana na swali lako. Naomba uulize swali lako la nyongeza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wizara ya Afya kwa uzembe waliokuwa nao, mimi nilikuwa mjumbe wa kamati, kuna dawa zinaharibika maabara kuletwa Hospitali ya Mnazi Mmoja zinashindwa niliuliza kwenye kamati, kutoka maabara Maruhubi mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja inachukua siku ngapi ukija kwa miguu, dawa zinahitajika hapo. Nikaambiwa sema swali lako, kama nusu saa. Dawa zinaharibika katika bohari kuu Maruhubi kuletwa pale kwa miguu haifiki siku tatu au nne. Wizara ya Afya ni wazembe na sio wafuatilaji na hawataki kujituma. (*Makofit*)

Swali langu ni kwamba, pamoja na serikali kuchukua hatua, ambapo sifirkirii mtu anaumwa na mwanawе, mjamzito kweli asiwekwe hospitali, anakesha pale kulala chini, hatuna la kusema ni uzembe na ubabaishaji, huu ni uzembe wa mwisho kwa serikali

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, naomba uulize swali lako la nyongeza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Unajua uchungu ni kitu kizito sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofî*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Najua una uchungu sana, lakini taratibu zinavyotaka uulize swali lako la nyongeza.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na serikali kuchukua hatua za nidhamu kwa makosa yaliyofanyika katika mazingira ya utu na uungwana.

Wizara imechukua hatua gani dhidi ya waathirika wa tukio japo kuwaomba radhi, na muathirika mwenyewe nimemleta yupo hapo juu, angalau kukutana naye na kumpa maneno mazuri, na maneno mazuri ni sadaka. Je, watachukua hatua gani ili kurekebisha, na Bi Halima yupo hapo juu. (*Makofî*)

**Mhe. Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim, lakini anachanganya swali lake sana.

- (a) Kwa sababu suala la bohari na dawa, hakuna dawa zinazotakiwa kuharibika wala tatizo lolote sasa hivi hakuna, hilo naomba nikiri hakuna.
- (b) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim anasema huyo mgonjwa yuko hapa sasa hivi hayupo, na mimi naomba nitibitishe kwamba hayupo huyo mgonjwa hapa. Huyo mgonjwa aliyetokezewa na hilo tukio hayupo humu ndani, na Wizara ya Afya ilifanya utaratibu maalumu wa kumtafuta na kumfanyia mahojiano huyo mgonjwa. Kwa hivyo, kama yupo athititishe amsimamishe pale hayupo, kwa hivyo analidanganya Baraza la Wawakilishi. La pili hilo.
- (c) Mhe. Mwenyekiti, huyu mgonjwa tayari Kamati ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imeshakutana naye na kutoa taarifa, na mume wake mwenyewe amekubaliana na kamati kusema kwamba ni kosa langu mimi ambaye sikuacha namba ni metafutwa kwa siku tatu. Kosa lililofanyika pale hospitali ni kutopeleka maiti kutoka *maternity* kwenda *mortuary*, hilo ndio kosa. Lakini kosa la mwanzo kubwa lililotokezea ni kutoacha namba ya simu, kwa sababu kama hujaacha namba ya simu huwezi kutafutwa, utatafutwa wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme wafanyakazi hawa wa Wizara ya Afya wanafanya kazi kwa uadilifu wa hali ya juu kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Wanafanya kazi ya kujitolea, huwezi kulinganisha mtu anayeokoa roho ya mtu mwengine ama mfanyakazi anayeokoa roho ya mtu mwengine kwa malipo tunayowapa, huwezi kulinganisha ni kazi ya wito.

Kwa hivyo kila tukiwatia maneno humu ndani tukasema hawa watu wazembe, hawa watu hivi, wajibu wangu mimi kuwatetea na kwenda kisheria na ni wajibu wangu panapotokezea kasoro kama Waziri na Wizara ya Afya na uongozi wa Wizara ya Afya nzima ni kuchukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria, lakini tusiwtie maneno watu ambao wanawajibika, wanafanya kazi kutumikia wananchi na wanafanya kazi wakati mwengine katika mazingira magumu sana.

Tunajua hali yetu ya kiuchumi, tunajua hali yetu ya kifedha, tunajua jinsi tulivyo, na tunajua kwamba matibabu nchini kwetu yanatolewa bila ya malipo, si nchi nyingi Afrika juzi tulikuwa tunazungumza pale, na kiongozi wa Wizara ya Afya aliyejuka kutoka Zimbabwe kanambia hata wao Zimbabwe wameshindwa, mnamo mwaka 1987 wameshindwa kutoa huduma za Afya. Wao walipata uhuru wao 1981 na 1987 wakashindwa kutoa huduma bure za afya. Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na kwamba mitambo ilikuwa haitaki.

Mhe. Waziri, pamoja na kwamba hizo bahati mbaya ambazo Mhe. Waziri amezisema zimekuwa zikitokea mara nyingi sana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa nini Serikali haidhibiti hizo bahati mbaya, *actually* ni uzembe Mhe. Waziri ameu-*defend* tu. Kwa nini haichukui hatua kabla haya matokeo hayajatokea na badala yake Serikali inakuwa inasubiri matokeo yatokee halafu ndipo madokezo na mambo mengine yanafanyika. Kwa nini Serikali haidhibiti kwa sababu hizi bahati mbaya zimekuwa nyingi na zina-*cost* maisha ya watu.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Wizara ya Afya pamoja na wafanyakazi wake wote wa Wizara ya Afya sio kama wanasubiri bahati mbaya itokee ndio wachukue hatua, hilo halipo kabisa, na wafanyakazi wote wanapewa mafunzo ya maadili mbali mbali pamoja na kujibu lugha nzuri, kutotoa ujuba hayo ni mionganii mwa malalamiko ambayo tunapata kila siku sisi, lakini tunaendelea kuyafanyia kazi na watu mbali mbali ama wafanyakazi mbali mbali wanaendelea kupewa maonyo hayo.

Kwa hivyo naomba niseme kwamba hatusubiri bahati mbaya itokee ndio tuchukue hatua, sisi tunachukua hatua za kuelimisha, hatua za kuwafahamisha wafanyakazi pamoja na hizi sheria zote kila pale jambo linapotokezea jipya ambapo wanahitaji kufahamishwa, lakini wakati huo huo inapotokezea bahati mbaya kama hiyo, basi hatusiti kuchukua hatua za kisheria na hatua za kinidhamu.

Kuna kamati maalumu ambayo pale Mnazi Mmoja peke yake ipo ya nidhamu ambayo inashughulikia Hospitali ya Mnazi Mmoja mbali ya kamati nyengine za nidhamu ambazo zinashughulikia vituo vingine viliopo Wilayani au Mikoani, yaani *ZMO Office*.

Kwa hivyo hilo naomba niseme kwamba kila linapotokezea basi hatua husika huchukuliwa kwa mujibu wa sheria. Ahsante

**Mhe. Hamad Abdalla Rashid:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa wafanyakazi wa kada ya Afya sehemu ya uuguzi ni wachache na ambao mara nyangi kadhia hii ya kukosa huduma bora kwa wananchi wetu inatoka, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kada hii inapata wafanyakazi wa kutosha ili kuweza kuondoa lawama hizi za kuwaita wazembe kwa sababu ya uchache wao.

Na je, Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba karibu itafunguliwa ikiwa sasa hivi wafanyakazi hawatoshi mumejipanga vipi kuhakikisha hospitali ile ambayo itachukua karibu wauguzi 150 angalau kuweza kutoa huduma hospitali ile, mumejipanga vipi Wizara ya Afya ili kutoa huduma hizi na kwa kweli mimi kama muuguzi naumia roho sana muuguzi kuitwa mzembe, uchache wao ndio unaowafanya kuhakikishwa wanaitwa wazembe.

Ni lini Wizara itachukua hatua kujipanga kuhakikisha wauguzi wanakuwemo wa kutosha katika mahospiteli yetu.

**Mhe.Waziri wa Afya:** Kwanza namshukuru kwa swali lake zuri sana, kwa sababu kweli kada ya wauguzi tunahitaji kuongeza wafanyakazi zaidi na sio kama hawapo kwenye soko wafanyakazi hao, kwa sababu Chuo chetu cha Afya kinazalisha takriban wauguzi 200 na zaidi kidogo kila mwaka. Sasa tayari Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshapeleka maombi yetu Utumishi kwa ajili ya kuongeza kada ya wauguzi. Na ni kweli katika jitihada za Mhe. Dkt. Ali

Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi huduma za afya zimeendelea kuwa bora zaidi.

La kwanza kabisa kuna Hospitali ya *Neuro* (mishipya fahamu, vichwa maji na uti wa mgongo) ambayo ilifunguliwa na ye ye mwenyewe Mhe. Rais miaka miwili iliyopita hadi jana imefikisha wagonjwa 500 ambao wamefanyiwa operesheni hapa ambapo operesheni zile hapo awali zilikuwa zinafanyika nje ya nchi. Kwa hivyo Serikali imeweza kuokoa zaidi ya dola milioni 8 na operesheni zile kufanyika hapa tukishirikiana na Taasisi kutoka Spain.

Lakini la pili, hospitali ya Abdalla Mzee iko katika hatua za mwisho kabisa kukamilika. Ni kweli pale panahitajika kwa kiwango cha chini kabisa kwa vifaa vilivyofungwa na huduma zilizotayarishwa pale panahitajika wafanyakazi 150, wafanyakazi hawa 150 hatuwezi kuwatoa ndani sehemu yoyote nyengine kwa sababu tayari huduma ziendelee kutolewa katika maeneo yote ya Wizara yetu ya Afya.

Kwa hivyo, tayari tumeshawasilisha maombi yetu ya kupata kibali ya kuajiri wafanyakazi wapya 150 Wizara ya Utumishi, na hivi sasa wakati wowote tunasubiri majibu hayo kwa sababu hao nao lazima wapange na Wizara ya Fedha kwa upande wa mishahara, watakapopatikana tu tuwaleta kisiwani Pemba kwa ajili ya kufanya kazi pale.

Lakini changamoto kubwa nyengine iliyokuwepo wafanyakazi hao tungependa sisi watooke Pemba wengi wao, lakini kada zinazotakiwa bahati mbaya hazipo, kwa hivyo kada nyengine inabidi tutolee hapa Unguja, na kada nyengine pia itabidi tuagize kutoka katika soko la ajira la wafanyakazi waliokuwa wamesoma kada zile, kama vile mfano *radiology* na mambo mengine kutoka wenzenzu Tanzania Bara. Kwa hivyo, watakapopatikana tu tutawaleta.

Changamoto nyengine pia ni sehemu ya makaazi, kwa sababu watu 150 hakuna sehemu ambayo unaweza kuwakodia wote kwa kada ya afya wakapata sehemu ya makaazi kwa kule Pemba, kwa hivyo, changamoto hiyo nayo pia inafanyiwa kazi na Serikali hivi sasa. Ahsante Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Simai Mohamed Said:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu alijirudia mara nyingi kusema kwamba maiti iliyokuwa ishafariki, sasa nilikuwa napata tatizo kufahamu maiti gani iliyofariki mara mbili. Nafikiria alikusudia mgonjwa aliyefariki katika wodi, kwa hivyo naomba Hansard iweze kuweka sawa kwamba alikusudia mgonjwa aliyefariki kwenye wodi sio maiti iliyofariki. Ahsante.

## Nam. 46

### Misaada kwa Vikundi vya Akina Mama

**Mhe. Suleiman Makame Ali** - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na jitihada za Serikali kuwawezesha akina mama ili waweze kujikwamua na umasikini, katika nchi yetu. Na kwa kuwa katika Jimbo la Ziwani kumekuwepo na vikundi vingi vya akina mama walijikusanya ili kuijendeleza kiuchumi. Na kwa kuwa kina mama hao hawajawahi kupata msaada kutoka Serikalini.

Je, ni lini akinamama wa Jimbo la langu la Ziwani watapatiwa msaada kama wanavyopata wenzao katika maeneo mengine.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto -**  
Aliliju:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 46 linalohusu kupatiwa kwa msaada wa uwezeshaji kwa vikundi vya akina mama wa jimbo la Ziwanii Pemba kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Mwakilishi kwa kutambua uwepo wa vikundi vya kina mama wanaojishughulisha na kazi mbali mbali za kujiongezea kipato katika jimbo la Ziwanii. Ni imani yangu kuwa tutashirikiana kwa pamoja na Mheshimiwa Mwakilishi kuwasaidia akina mama hao kuijendeleza kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, inatambua uwepo wa vikundi vya akina mama wanaojishughulisha na shughuli za ufinyanzi, utengenezaji wa sabuni na ufwugaji katika Jimbo la Ziwanii Pemba. Kutambua uwepo wa vikundi hivi kunatokana na ziara iliyowahi kufanywa na Wizara kuititia Idara inayoshughulikia masuala ya Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Jimboni hapo. Katika ziara hiyo ushauri ultolewa juu ya kukuza na kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali.

Mhe. Mwenyekiti, viongozi wa vikundi hivyo, pamoja na vikundi vyengine wamewahi kupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili waweze kuendesha shughuli zao kwa mafanikio. Baada ya mafunzo hayo, vikundi hivyo vimepatiwa fursa ya kushiriki katika maonesho mbali mbali yaliyoandalowiwa na Wizara kwa lengo la kuwasaidia kuwapatia masoko ya bidhaa zao.

Mhe. Mwenyekiti, yote hayo yaliyofanyika ni msaada ultolewa na Serikali kuptit Wizara ya Kazi, Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ambao umesaidia kuimarisha shughuli za vikundi hivyo vya kina mama ukilinganisha na hapo awali kabla ya kupatiwa fursa hizo.

Pia napenda kumkumbusha Mhe. Mwakilishi na wanavikundi kuwa, misaada na fursa nyengine zinazopatikana baada ya mafunzo hutegemea zaidi hali ya kikundi, utayari na mahitaji yao. Na kwa hili, Wizara iko tayari kushirikiana na vikundi vya Wanawake wa Jimbo la Ziwani - Pemba ili kusaidia na kujiendezea Kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa misaada ya kifedha ambayo hutolewa kwa njia ya mikopo. Wizara ya Kazi Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imeshatoa kiasi cha Shilingi Milioni Kumi na Laki Tano (10,500,000/-) kwa vikundi, na kiasi cha shilingi Milioni Tano la Laki Tisa (5,900,000/-) kwa wajasiriamali mmoja mmoja katika Jimbo la Ziwani, Pemba. Vikundi vilivyopewa fedha hizo ni mchanganyiko ambavyo vinajishughulisha na uanikaji wa dagaa, ukulima wa mwani na ufugaji wa kuku.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu ambe ametuwezesha kufika leo hii katika Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Waziri kuna vikundi vingi vya akina mama pamoja na vijana ambao wamejipanga kwa ajili ya kuweza kujiwezesha kimaisha pamoja na watoto wao.

Je, Mhe. Waziri ili uweze kupatiwa mkopo katika Wizara yako ya Uwezesaji ni masharti gani yanazingatiwa, au ni vigezo gani vinazingatiwa kwa wenye vikundi ili waweze kupatiwa mikopo.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, taratibu na sheria zinazotakiwa kwa ajili ya kupatiwa mikopo la kwanza ni pamoja na kupata elimu kwanza, wanataka mkopo wa aina gani.

Pili ni kuweza kuwa katika vikundi ambavyo vimesajiliwa na ambavyo tayari vina shughuli inayofanya, taratibu zinazofanywa wanakuja wanakwenda kwenye Wizara yetu wakifika pale wanawasiliana na Idara husika,

wanaohusika wanatathmini wanaona mahitaji uliyonayo, wanakwenda kuangaliwa vikundi vilivyoko. Kwamba ule mkopo uliokusudiwa ndivyo kitu kinachowea na kwamba ile fedha ukipewa una uwezo wa kurudisha.

Kwa sababu kutokana na uzoefu inaonesha kwamba wengi waliokuwa hawatathminiwi miradi yao wanafika hawawezi kurudisha mikopo, kwa hivyo wanaaua ule mtaji wa Ofisi, wakishafanyiwa hapo wanaangaliwa sasa kile kikundi walichoko maana yake inawezekana ni kikundi kimoja ambacho kimeshajiandikisha na kinaeleweka lakini kikawa ndani yake kuna watu wenye *interest* tofauti wanapewa kwa mujibu wa *interest* walizonazo lakini chini ya mwamvuli wa kikundi ambacho kiko pale kimesajiliwa, ambacho hakipungui watu watano.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

- a) Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yako inahakikisha kwamba inasaidia wanavikundi akina mama, kwa kuwa mimi jimbo langu lina vikundi takriban 350 vya kinamama na vina zaidi ya watu watano, vikundi vingapi Wizara yako ishavipa mikopo kuwasaidia.
- b) Ni lini tutakwenda mimi na wewe mguu kwa mguu kuwasikiliza matatizo yao katika jimbo langu la Chaani.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Napenda kumwambia tu Mhe. aliyejukweko kwamba yote haya yatafanyika ikiwa yeye mwenyewe ndio atakayetupa ushirikiano wa kwanza, kwa sababu kama wapo watu hawa 350 atuoneshe hawa wako wapi na tuwapate vipi, na kama anaona yeye anaweza kuwapata awaelekeze ofisini kwetu. Lakini akiona tuwafuatilie twende nao pamoja ni yeye kupanga ziara na mratibu kwa mujibu wa maafisa wake, ofisi yetu iko tayari kufanya kazi na ndio makusudi ya kuwekewa Idara husika katika suala hilo.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikishajihisha kinamama kujiunga katika vikundi hivi, sasa vikundi hivi vingi vimekuwa havina tija kwa kinamama kutokana na aidha kukosa soko hasa la ndani, lakini pia kutokana na kukosa elimu hasa ya kifedha juu ya kuviendesha vikundi hivi.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ipo haja ya kuja na mpango mwengine mbadala wa kuwaendeleza akinamama badala ya kung'ang'anaa na mpango huu wa kuwashajihisha kuijunga vikundi ambaa unanufaisha wachache, na vikundi vingi vyengine vinakuwa havinufaiki badala yake vinakufa njiani.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Napenda nimhakikishie kwamba Mheshimiwa aliyesema kwamba vikundi vyote vilivyosajiliwa na ambavyo vimetolewa mikopo chini ya Wizara yetu, mpaka sasa hivi kwa utafiti tuliofanya hakuna hata kimoja ambacho kimekuwa, ni vile vyote ambavyo vimekosa elimu, na vingi vimeingizwa kwenye *NGO's* nyengine ambazo hawaji kwetu.

Lakini wale waliokuja kama nilivyosema kwanza kuna elimu muafaka inatolewa na ukitaka kulithibitisha Mhe. naomba uje ofisini kwangu nikukutanishe na watu wanaohusika na mikopo ili uweze kujifunza vizuri zaidi, na ili uweze kuwa mtu wa kuweza kuwasaidia zaidi wengine kuonesha kwamba kazi iliyofanywa na Serikali ni kazi muhimu na tunafanya kwa uaminifu.

Kwenye suala la soko tunajitahidi sana kushirikiana na Waziri wa Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko na wajasiriamali mbali mbali, kwa kutumia kitengo chetu kilichoko Mbweni cha *Incubators* na pia kuwashakikisha kwamba hawa ndio tunaowaunganisha na watu watakaoweza kununua biashara zao. Kuna utaratibu maalumu ambaa kunakuwa na *management* wanakwenda kuwafuatilia masoko hata kwenye mahotelii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nataka kukwambia kwamba wamepata masoko mengi sana, kitu ambacho kinatutatiza ambacho tunakifanya kazi sasa hivi ni kuweza kuitishwa kwenye kiwango kinachopimwa na *section* inayoshughulikia kupasisha ili waweze kupata *label* zinazovutia na *size* inayotakiwa kwenye mahotelii.

Mwanzo tulikuwa tunatengeneza bidhaa ambazo ni kubwa zaidi lakini kumbe kwenye mahotelii wana *size* maalumu wanazopewa, kwa hivyo tunatafuta vifaa hivi na tuko njiani kuvipata.

## Nam. 151

### **Urejeshaji wa Fedha za Mkopo wa Elimu ya Juu**

**Mhe. Mohammed Said Mohammed** – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema imeanzisha Bodi ya mikopo ya Elimu ya juu ili kuwapatia fedha wanafunzi wa vyuo mbali mbali.

- a) Je, Serikali inadai kiasi gani cha fedha tangu kuanzisha Programu hiyo hadi sasa.
- b) Ni wanafunzi wangapi wamerejesha fedha hizo tangu kuajiriwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohammed Said Mohammed Mwakilishi wa Jimbo la Mpenda swali lake Namba 151 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya ufanuzi kama hivi ifuatavyo:

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ilianzishwa kwa Sheria namba 3 ya mwaka 2011 kwa madhumuni ya kuwapatia mikopo wanafunzi wa Zanzibar wanaojiunga na Taasisi za Elimu ya Juu. Kabla ya kuundwa kwa chombo hicho, kazi za utoaji mikopo zilikuwa zikitekelezwa na Mfuko wa Elimu ya Juu wa Zanzibar uliofanya kazi kuanzia mwaka 2006 hadi 2010. Hivyo Bodi ya Mikopo ilipofanya kazi zake rasmi ilirithi madeni ya mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Elimu ya Juu wa Zanzibar. Baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakillishi kama hivi ifuatavyo:

(a) Kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2016, wanafunzi walioomba mikopo ya elimu ya juu walikopeshwa Tshs. Bilioni 35. Fedha hizo ni jumla ya fedha zilizokopeshwa na Mfuko wa Elimu ya Juu pamoja na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kati ya fedha hizo Tshs. Bilioni 7.1 zilikopeshwa na uliokuwa Mfuko wa Elimu ya Juu (Kuanzia mwaka 2006 – 2010) na Tshs. Bilioni 27.9 zimekopeshwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar.

(b) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inaendelea kukusanya marejesho ya mkopo kutoka kwa wahitimu waliofaidika kwa kipindi cha miaka kumi ambapo hadi mwezi Agosti 2016, Bodi imekusanya

jumla ya Tshs. 1.9 bilioni kutoka kwa wahitimu 1,161 na wahitimu 41 tu ndio waliokamilisha kulipa madeni yao yote. Hivi sasa, Bodi ya Mikopo imeanza kuwachukulia hatua kali wahitimu ambao hawajajitambulisha kwa kuwataka walipe na faini. Hatua hiyo imesaidia kuwapata baadhi ya wakopaji ambao muda mrefu walikuwa hawajajitokeza. Bodi inaendelea kuwafuatilia wakopaji 3,700. Ahsante.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana pamoa na majibu marefu ya Serikali naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Bodi kwa kukusanya fedha nyingi ambazo zipo mpaka sasa, lakini vile vile swali langu linakuja kwa kuwa kuna wanafunzi wengine hawakuajiriwa katika Serikali au ajira zisizokuwa rasmi, ni mkakati gani wa Serikali kufanya wale ambao waliokuwa hawakuajiriwa kwenye sekta rasmi zitakusanya fedha zile na kurudi ili ziwasaidie wengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Wizara inaandaa mikakati ya kuweza kuifikia kila mkopaji kwanza kwa kuhakiki, wameanza kujitokeza kufanya uhakiki baadae tunawafuatilia katika Taasisi zao walizoajiriwa; iwe Taasisi rasmi au zisizo rasmi, ziwe za ndani ya Zanzibar au za Jamhuri ya Muungano. Tumeshaanza kuzungumza na wenzetu Wizara ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano kuangalia wale ambao wameajiriwa katika Taasisi za Bara nao pia kuweza kupata. Lakini pia sasa hivi tunafanya kazi ya kurekebisha sheria yetu ili pia kuweza kumlazimisha mtu baada ya kipindi cha mwaka mmoja kumaliza masomo aanze kulipa, awe ameajiriwa au hajaajiriwa. Au ameajiriwa katika Taasisi rasmi au zisizo rasmi, na kama itashhindikana basi wadhamini wake labda wengine wanaweza kuwa hawajulikani wapi walipo, lakini wadhamini wake tunajua wapi walipo, kwa hivyo sheria itachukua hatua wakati huo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna wakopaji takribani 3700 ambao bado wanafuatiliwa ili kuweza kulipa mikopo waliokopa. Je, ni kiasi gani cha fedha cha wakopaji hawa 3700 ambao hawajalipa mikopo yao ili kuweza kuwasaidia wanafunzi wengine kuweza kuendelea na masomo yao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, tunao wakopaji 3700 ambao hawajalipa, kwa hivyo takwimu sahihi ya idadi ya fedha hizi ambazo wanadaiwa wanafunzi hawa tutakupatia baadae *in shaa Allah*.

**Mhe. Yussuf Hassan Idd:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa wale wanufaika wa mkopo ambao wamefariki, je, Wizara ina mpango gani wa kuzirejesha zile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, tunasisitiza kusema kwamba waliokopa walikuwa na wadhamini wao, kwa hivyo wadhamini watabeba jukumu la waliofariki, kama wanavyobeba maslahi ya waliofariki basi pia na deni wanalibeba warithi, yaani wadhamini kwa maana hiyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe muda wetu wa maswali umekwisha lakini kwa kutumia kanuni ya 39(3) kwa mamlaka niliyopewa naongeza dakika 5 za maswali tunaendelea. Katibu kwa swali linalofuata.

## Nam. 37

### Utunzaji wa Takwimu za Watalii

**Mhe. Nassor Salim Ali (Kny.Mhe. Salma Mussa Bilal):** - Aliuliza:-

Katika sekta ambayo inaingiza mapato makubwa ya nchi ni sekta ya utalii.

- (a) Je, Serikali ina takwimu sahihi ya watalii wanaoingia nchini.
- (b) Ni njia gani inayotumika kuhakikisha kwamba hakuna uvujaji wa mapato katika sekta hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo** -  
Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal, Viti Maalum swali lake namba 37 kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nikiri kuwa sekta ya Utalii ni miongoni mwa sekta inayochangia kwa kiasi kikubwa katika kuingiza mapato nchini. Sekta hii inakisiwa kuchangia zaidi ya asilimia 80 ya fedha za kigeni.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile sekta ya Utalii kwa ujumla wake imekuwa ikichangia zaidi ya asilimia 20 ya pato la Taifa ambapo huduma za malazi na chakula zilichangia asilimia 8.1 katika mwaka 2015.

Aidha, takwimu zinaonesha sekta ndogo ya huduma na chakula pekee iliajiri watu wapatao 8,443 (*Direct Employment*) kwa mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, nafahamu kuwa takwimu ndio msingi sahihi wa maendeleo ya sekta yoyote ile ikiwemo sekta ya Utalii. Naomba niliarifu Baraza lako Tukufu kuwa suala la ukusanyaji wa idadi ya watalii wanaoingia nchini kwa mujibu wa sheria hujumuisha taasisi kuu tatu ambazo ni Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Utalii na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ushirikiano wa dhati wa taasisi hizi ndio unaosababisha upatikanaji kwa takwimu sahihi au kinyume chake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi nilizozieleza hapo kabla tumeshabaini na kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya changamoto zilizokuwa zikikwamisha upatikanaji wa idadi sahihi za wageni wanaoingia nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo napenda niwaarifu wajumbe kuwa Wizara yangu inaamini kuwa takwimu za watalii wanaoingia nchini ni sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuziomba Taasisi zote zinazohusika na upatikanaji wa takwimu wa Takwimu za Utalii, kuendeleza ushirikiano wao kwa Wizara yangu nikiamini sote tunahusika katika kuendeleza Sekta ya Utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa hakuna uvujaji wa mapato katika Sekta ya Utalii njia zifuatazo zinatumika.

- (b) Njia hizi ni kama zifuatazo: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hufanya ukaguzi kwenye miradi ya Utalii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wawekezaji wetu wanalipa kodi, tozo za leseni zao kwa mujibu wa taratibu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuhakikisha wafanyabiashara katika Sekta ya Utalii na Watalii kufanya malipo yao kupitia benki za hapa nchini kwetu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuwashajiisha wananchi kuweza kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika Sekta ya Utalii kwa kiwango na ubora unaotakiwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na jitihada zake za kuwawezesha wajasiri amali katika Sekta ya Utalii ili waweze kutoa huduma bora kwa wageni wetu. Ahsante.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza kwa Mhe. Waziri, anambie nini maana ya tozo, na tozo za aina ngapi ambazo wawekezaji hawa wa utalii wanatakiwa kutoa kwa Serikali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba maana ya tozo ni ile sehemu ya pato wanalotozwa wageni wakati wanapoingia katika sehemu zetu za utalii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo arejee swali lake la (b).

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Mhe. Mwenyekiti, swali langu la kifungu (b) linasema hivi. Ni tozo za aina ngapi ambazo huwa zinatolewa na wawekezaji hawa wa mahotelii kwa Serikali. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba alivytaka kujuua ni tozo za aina ngapi wanazotoza au wanazotozwa hawa wageni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi kupitia swali hili hizi aina za tozo nitamjibu kwa njia ya maandishi. (*Makofii*).

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba nimjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Magomeni swali la nyongeza.

Tozo kwa lugha nyengine ni ile *levy* inayotozwa kwa watalii, mahotelii na katika maeneo mengine. Kwa hivyo kuna aina tatu ya tozo zinazotozwa katika nchi yetu hapa Zanzibar.

### Kupatiwa Wataalamu wa Kilimo

**Mhe. Maryam Thani Juma** – Aliuliza:

Kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu na niseme kwamba wananchi wa Jimbo langu wanategemea sana kilimo kama vile tungule, mboga mboga na matikiti. Kilimo hicho cha mazao hayo hawavuni ipasavyo kutokana na utaalamu mdogo walionao wa kilimo hicho.

Je, Serikali imejipangaje kuwapatia wataalamu wa kilimo wakulima hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Maryam Thani Juma Mwakilishi wa Jimbo la Gando swalii lake namba 129 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba “Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu”, inakadirwa asilimia 70 ya Wazanzibari wamejajiri katika sekta ya kilimo. Serikali kupitia Wizara hii imekuwa inatoa utaalamu wa kilimo kwa kupitia wataalamu waliomaliza Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa ngazi ya cheti na diploma. Wizara kupitia Idara ya Kilimo, Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo na Kuendeleza Sekta ya Mifugo (ASSP & ASDP-L), pamoja na taasisi za kibinafsi zikiwemo *Tanzania Horticultural Association (TAHA)* na UWAWIMA, VSO, Kampuni ya ZAIDI zinatoa taaluma ya kilimo bora. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swalii moja la nyongeza lenye (a) na (b).

- a) Mhe. Naibu Waziri naomba kujua ni mabwana shamba wangapi na mabibi shamba wangapi waliopo katika Wilaya ya Wete.
- b) Ni utaratibu gani hutumia kuwatemeblea wananchi kuwashauri ili kupata tija katika kilimo hicho.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:**

- (a) Mhe. Mwenyekiti, kwa vile swalii lake ni la takwimu naomba nimletee kwa maandishi, lakini kwa kumsaidia hapo hapo kwamba tuna mabwana shamba na mabibi shamba kule kwa kila shehia wanawapitia watu wao. Ahsante.

- b) Utaratibu wetu ni kwamba tumewapatia vipando (pikipiki), kwa hivyo wanawapatia wale wenye mashamba yao kwa kuwasikiliza hoja zao na vile vile kuna vituo ambavyo vipo na maafisa kila Wilaya wanatakiwa wao wenyewe binafsi wakiwa na matatizo basi waende hapo wawasilishe tatizo lao.

**Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi swali langu kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri alieleza kwamba kuna taasisi ambazo zinatoa elimu ya kilimo cha biashara. Je, wizara inatoa msada gani kwa taasisi hizo ili kuona hawa wakulima wetu wanaendelea vizuri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, kama Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ina mashirikiano makubwa sana na taasisi hizi, vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mradi wake wa MIVARF una malengo ya kujenga *processing food*. Kwa hiyo tayari pale tuna mashirikiano makubwa sana ili kuweza kuvifanya *process* vile vyakula kwa ajili ya kuvisindika. Ahsante.

### Nam. 35

#### Minara ya Mawasiliano

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf – Aliuliza:-**

Jimbo la Bumbwini limebahatika kuwa na minara miwili ya simu ambayo ipo karibu mno. Mnara mmoja kati ya hiyo unatoa huduma za Zantel na mwengine uliobakia upo tu bila ya kushughulikiwa wala kukaguliwa kwa muda wa miaka minne sasa.

- (a) Je, ni nani mmiliki wa mnara huo
- (b) Ni nini malengo ya kuwekwa kwa mnara huo.
- (c) Je, mnara huo unafanya kazi, na iwapo mnara huo haufanyi kazi, huoni kuwa kuna haja kwa Wizara yako kufanya utaratibu utaohakikisha kuwa mnara huo unaondolewa ili kuepusha madhara yoyote yanayoweza kutokea kwa wananchi wanaoishi karibu na mnara huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Mwenyekiti, mmiliki wa mnara wa mbao kwa miaka minne sasa umeachwa bila ya shughuli yoyote ni Kampuni ya *Excellentcom* kutoka Tanzania Bara ambayo ilipata usajili wake kutoka *TCRA*.
- (b) Mhe. Mwenyekiti, mnara huo haufanyi kazi kwa sasa, hata hivyo mnara huo kuwepo kwake hautoleta madhara yoyote kiafya kwa wakaazi wa eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Kampuni ya *Excellentcom* hivi sasa imefilisiwa na kuna kesi inayoendelea Mahakamani. Hivyo, inashauri kwamba wamiliki wa eneo hilo waendelee kusubiri hadi hapo hukumu ya kesi itakayotolewa kwa maamuzi zaidi. Ahsante.

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba mnara huu wenyewe wamefilisiwa na anatwambia kwamba mnara huu hautoleta madhara yoyote kwa wananchi waliokuwepo pale. Naomba nimwambie Mhe. Naibu Waziri mnara ule kwa sasa watoto imekuwa ndio ngazi yao ya kupanda na kwenda juu kucheza. Je, huoni kama mtoto yeypate atakayepanda kule juu inaweza kutokea hatari yoyote na nyinyi kama serikali mnachukua hatua gani ya kuuondosha kabisa ule mnara pale ulipo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ule mnara watoto wanauchezza lakini kama nilivyosema hapo kabla lile suala hivi sasa liko Mahakamani, sisi hatuwezi kuyaingilia maamuzi ya Mahakama, lakini mimi nitamshauri kwa vile ye ye ni mwananchi na vile vigezo Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini basi ashirikiane na watu wa shehia yake kuhakikisha watoto hawachezei si mnara tu bali eneo lolote la hatari kwa maisha yao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ningeomba kumuuliza swali la ziada Mhe. Naibu Waziri,

- (a) Kwa kuwa tunafahamu kwamba minara husababisha kensa na maradhi mengi katika jamii, ni vigezo gani mnatumia kuwaruhusu wenyewe minara kuweka minara yao katika maeneo ya wananchi.
- b) Ni lini mtahakikisha minara hiyo mnaiondosha katika sehemu za wananchi karibu na nyumba zao na kuhamisha sehemu maalum kuruhusu minara hiyo kufanya kazi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Mwenyekiti, minara ile haina athari yoyote kwa sababu kama unavyojuu kuna wataalamu wa mionzi wapo katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia, ambapo *TCRA* ni suala la Muungano katika mambo ya mawasiliano. Kwa hiyo, wametuhakikishia kwamba minara ile haina tatizo lolote kwa afya ya binadamu na ndio maana imeruhusiwa kihalali kabisa kuwepo katika maeneo hayo husika. Kwa hiyo, mimi napenda kumtoa wasi wasi kwa sababu serikali sisi tunajali afya za wananchi wetu, hivyo hatutokubali hata siku moja kama kuna jambo la hatari tukahatarisha maisha ya wananchi wetu. Kwa hiyo, mimi namuondo shaka kwa hili na wataalamu wamethibitisha hilo na hiyo minara inatumika duniani kote na ingekuwa ina madhara basi isingeruhusiwa na nchi zilizoendelea zaidi kiteknolojia.

Suala lake la pili ni kwamba minara ambayo imo katika kesi za Mahakama hatuna uwezo wa kuyafanya hayo yote, lakini vile vile nataka kumuarifu kwamba kila siku teknolojia inapoendelea basi minara inazidi kupungua, kwa sababu sasa hivi tunashajihisha makampuni ya simu kufunga minara ambayo *height* yao inaanzia mita 60 kwenda juu, hii inapunguza kuweka minara zaidi.

Kwa hiyo, hiyo ndio kazi tunayoifanya, kuwashajihisha makampuni ya simu kufunga minara ambayo ni mirefu zaidi ndio inapunguza kuwepo kwa minara ile mifupi ambayo imeenea maeneo mengi hivi sasa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kipindi cha maswali na majibu tumemalizia hapa, lakini naomba kwanza tuendelee na taratibu zinazofuata tuwatambue wageni waliokuja leo.

Mgeni wa kwanza ni wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, bibi Halima Khamis Omar ni mwananchi kutoka Mwera.

Wageni wengine ni wa Mhe. Wanu Hafidh Ameir viti maalum ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Skuli ya SUFA, jumla yao ni 12, naomba wasimame popote walipo.

Pia wageni wengine ni wa Mhe. Suleiman Makame Ali, Jimbo la Ziwani ambaye ni Hamza Suleiman Hamad, Katibu wa Tawi la CCM Wesha na Mkubwa Said Mkubwa, Katibu wa UVCCM, Tawi la Ziwani. Karibuni sana.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Mswada wa Sheria ya (Utafutaji na Uchimbaji) Mafuta na Gesi Asilia, 2016**

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya ili kuweza kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Kuhakikisha Uwajibikaji wa Taasisi ya Mafuta na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa nia na dhamira walizonazo za kuendeleza nchi hii na kutuongoza kwa salama na amani na wananchi kuweza kuendelea na shughuli zao za maisha za kila siku bila ya bughudha ya aina yoyote. Tunawashukuru viongozi wetu hawa, Mwenyezi Mungu awape maisha marefu. Aidha, tunawaomba wananchi kuendelea kuilinda amani iliyopo kwani ndio hazina pekee kwa maisha yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiwezesha Zanzibar kuwa na mamlaka yake wenyewe ya kushughulikia masuala yote yanayohusu rasilimali ya mafuta na gesi asilia na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kifungu chake cha 2(2) cha sheria husika.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mhe. Spika na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa na makini mnayoifanya katika kutusimamia na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku hapa Barazani, *in sha Allah* Mwenyezi Mungu ataendelea kuwapa busara, hekima na uadilifu katika kuliongoza Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mashirikiano makubwa walijotupa katika kufanikisha mswada huu muhimu. Kwa kweli wajumbe hawa walijituma sana bila ya kujali wakati. Shukurani za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Kamati

hiyo Mhe. Hamza Hassan Juma kwa busara zake katika kipindi chote cha kuupitia, kuurekebisha na kuimariswa mswada huu muhimu, nawashukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa ya moyo wangu, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao walijotupa katika semina na majadiliano mbali mbali, kwa kweli imetusaidia sana katika kufanikisha kazi hii ya kihistoria kwa Zanzibar, nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa watendaji na wataalamu wangu wote wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara akisaidiwa na kamati maalumu iliyoundwa na wizara kwa ajili ya utayarishaji wa mswada huu.

Aidha, pongezi maalumu ziende Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa msaada na muongozo mkubwa walijotupa kwenye fani ya sheria, nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukiri kuwa wataalamu hawa kwa umoja wao wamefanya kazi kubwa sana katika kuandaa mswada huu muhimu kwa Taifa letu hadi kuweza kuufikisha leo hii katika Baraza lako tukufu. Kwa heshima kubwa tunajivunia kuuleta hapa Barazani kwa kuuwasilisha ili tuweze kutoa maoni yetu, ili baadae uwe sheria kwa manufaa ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti na Shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta Zanzibar sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetayarisha sheria ya mafuta na gesi asilia ili kuiwezesha Zanzibar kutumia fursa iliyopo katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ili shughuli hizo ziweze kuendelezwa kwa manufaa ya Taifa na watu wake. Ni dhahiri kwamba suala hili la kuwa na sheria madhubuti itakayowezesha Zanzibar kusimamia masuala hayo ni jambo la msingi, kwani kabla ya sheria hii Zanzibar haikuwa na sheria yake yenye ya kusimamia masuala ya mafuta na gesi asilia ukiacha zile sheria za *Mining Mineral Oil, Decree Cap 108* na ile ya *Mining Oil Cap 106*. Hivyo, mswada wa sheria hii una lengo la kuiwezesha Zanzibar kusimamia yenye masuala ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba kwa kipindi kirefu suala la mafuta na gesi asilia limekuwa ni suala linalosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya 1977 na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta ya 1980; *Petroleum, Exploration and Production Act, 1980*. Hata hivyo, kutokana na mijadala ya muda mrefu juu ya namna ya uendeshaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia baina ya serikali zetu mbili; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumepelekea kuwepo kwa mapendekezo ya kila upande kusimamia wenyewe sekta hii.

Utekelezaji wa mapendekezo hayo ulitegemewa kuchukua nafasi yake kwa kufanyiwa marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini baada ya kutofanyika kwa marekebisho yaliyokusudiwa awali pamoja na kutokamilika hatua za kuipitisha Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulingana na ratiba iliyopangwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha sheria mpya ya mafuta ya Tanzania Nam. 21 ya 2015. Chini ya sheria hiyo kifungu Nam. 2(2) kimeipa mamlaka Zanzibar ya kusimamia wenyewe masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Sheria hiyo imekidhi makubaliano kati ya serikali mbili kwa kuweka vifungu ambavyo vimeruhusu kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi kwa upande wa Zanzibar pamoja na mapato yatakayotokana na rasilimali hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria huu umegawika katika sehemu kumi na moja ikiwa na jumla ya vifungu 155. Miiongoni mwa mambo muhimu yaliyoainishwa katika mswada huu wa sheria ni uanzishwaji wa mamlaka na usimamizi wa masuala ya mafuta, *Zanzibar Petroleum Upstream Regulatory Authority* ikijumuisha uongozi wa mamlaka hiyo. Uanzishaji wa Bodi ya Wakurugenzi pamoja na kubainisha mpango wa uendeshaji wa mamlaka na taratibu za kifedha.

Mamlaka hiyo ndiyo itakayomshauri Mhe. Waziri kutoa leseni kwa makampuni ambayo yatajihusisha na biashara ya uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi asilia hapa nchini. Vile vile mswada unazungumzia kuanzisha kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta Zanzibar (*Zanzibar Petroleum Development Company*) ambayo itaanzishwa kwa mujibu wa sheria ya usajili wa makampuni Zanzibar. Vile vile mswada unazungumzia uendeshaji wa shughuli za mafuta yakiwemo masuala ya usimamizi wa maeneo ya mafuta, haki, utoaji wa leseni, utangazaji wa zabuni za utafutaji na uchimbaji wa mafuta pamoja na mikataba ya mafuta. Mswada kwa upande mwengine unazungumzia ukomo wa shughuli za uzalishaji wa mafuta na kuhakikisha kwamba maeneo yaliyotumika kwa shughuli za mafuta yanarejeshwa katika hali yake ya kawaida.

Mswada huu unatoa muongozo kuhusiana na usalama wa afya na mazingira ya kazi ikiwa na lengo la kulinda maisha ya watu kutokana na shughuli hizi za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi.

Pia Mswada unazungumzia ushirikishwaji wa jamii, (*local content*) na uwajibikaji wa makampuni kwa jamii (*Corporate Social responsibility*), pamoja na uadilifu kwa makampuni.

Mswada pia unazungumzia makosa mbali mbali na adhabu zake ili kuweka nidhamu na kuwezesha usimamizi bora wa sheria hii pamoja na utatuzi wa migogoro inayohusiana na masuala ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wajadili na kuchangia kwa upeo mswada huu, kwa vile utawezesha kuwepo kwa mfumo wa kisheria katika kusimamia utekelezaji wa sera ya mafuta na gesi asilia na kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kudhibiti na kusimamia moja kwa moja shughuli zinazohusiana na mafuta na gesi asilia nchini.

Mwisho kabisa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu baada ya majadiliano kuuridhia na kuupitisha mswada huu muhimu kwa faida ya Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Kabla ya hapo nilikuwa naomba wale wanaotaka kuchangia waanze kuleta majina yao.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi naomba kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya (Utafutaji na Uchimbaji) Mafuta na Gesi Asilia, 2016.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma hotuba yangu kwanza nilikuwa naomba maji ya kunywa, lakini la pili nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe waangalie *copy* ya marekebisho tuliyoyafanya kwenye kamati. Kwa sababu ni mengi sana tumechukua karibu kurasa 19. Kwa hiyo, wakati watakapokuwa wanajadili mswada huu inawezekana yale ambayo watakayokuwa wameyachangia tayari kamati ilikwishayazingatia kwenye mswada. Sasa

naomba sana wanapochangia mswada huu waangalie zaidi na haya marekebisho ambayo tumeyafanya.

Mhe Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo sasa naendelea tena kutoa shukuran zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mizima mwenye afya njema au tukiwa wazima wenyе afya njema, ili kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Usimamizi wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti na Shughuli za Utafutaji wa Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kuanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na kuhakikisha uwajibikaji wa taasisi za mafuta na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuendelea katuongoza kwa salama na amani na wananchi kuendelea na shughuli zao za maisha za kila siku bila ya bughudha ya aina yoyote. Tunawaomba wananchi waendelee kuilinda amani hii iliyopo kwani hiyo ndiyo hazina pekee ya maisha yetu na vizazi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, pili nakushukuru wewe na wasaidizi wako kwa kazi kubwa na makini mnayoifanya katika kutusimamia na kutuwezesha katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, tatu kwa niaba ya Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi hatuna budi kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na timu yake ya wataalamu ikiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dkt. Ali Khalil Mirza akisaidiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Nishati pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Usimamizi wa Mazingira na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ikiongozwa na Mwanasheria wetu Mkuu Mhe. Said Hassan Said.

Aidha, pongezi maalumu ziende kwa Ndugu Saleh Said Mbarak kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu, ambaye alikuwa ndiye “Dictionary” letu kwa upande wa utaalamu wa Sheria pamoja na ufundi wa sheria na miongozo yote kwenye fani ya Sheria. Kwa kweli serikali yetu inayo hazina nzuri ya wataalamu katika fani hizi nilizozitaja hapo juu. Kwa hiyo, ni vyema wataalamu hawa wakalindwa na kupewa fursa kubwa zaidi ili kuonesha utaalamu wao kwa maslahi ya taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu hawa wamefanya kazi kubwa sana katika kuandaa mswaada huu muhimu kwa taifa letu, hadi kuweza kuufikisha kwenye Kamati yako na hii leo kwa heshima kubwa tunajivunia kuuleta hapa Barazani kwa kuuwasilisha, ili tuweze kutoa maoni yetu na baadae tuwe na sheria kamili. Wataalamu wetu hawa inaonesha waliangalia Sheria za Nchi mbali mbali na kuweza kuchukua yale mazuri yote na kuacha yale mabaya, na ndio maana tukaweza kupata Mswaada huu ambaa naamini wajumbe wote watauchangia na kutoa maoni yao ili kuuboresha na hatimaye kuupitisha kwa nguvu zetu zote kwa pamoja kwa maslahi mapana ya nchi yetu na Wazanzibari wote. Pia sisi ndio tutaokuwa mabalozi wazuri huko Majimboni mwetu tutakaporudi ili kuweza kuwaelimisha wananchi wetu kwani hiyo ndio kazi kubwa itakayotukabili baada ya kuupitisha Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu uliipa siku tano ili kuupitia mswaada huu zikiwemo siku mbili za wadau, lakini kutokana na uzito na umuhimu wa Mswada huu kamati yangu ilitumia siku nane kuukamilisha Mswada huu, na kubwa ilikuwa ni kwa wajumbe kuweza kujua madhumuni hasa ya mswada wenyewe, lakini pia kujua sheria zitakazotulinda na wananchi wetu watilindwa vipi na mali zao pale zitakazoathirika, lakini pia urejeshwaji wa hali ya kawaida pale itakapojitekeza uharibifu wa mazingira, halikadhalika kujiridhisha na hakutokuwa na matatizo wakati wa utekelezaji wa mradi. Lakini kubwa kabisa na la mwisho ilikuwa ni namna gani wananchi wetu hasa wa Zanzibar wataweza kufaidika vipi na rasilimali hii ya Mafuta na Gesi Asilia wakati wa maandalizi hadi kuanza uzalishaji wake hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka pia niwahakikishie Wajumbe wako wote wa Baraza pamoja na wananchi wetu wa Zanzibar wamewekewa maslahi makubwa sana kuanzia kwenye utoaji wa vibali vyote vyaya leseni kupitia Kampuni yetu ya ndani (*ZPDC*), ambayo itakuwa ni wakala wa serikali. Vile vile watafaidika na elimu, ufundi, ajira pamoja na ushiriki wa moja kwa moja kwenye kutoa huduma kwa makampuni yatakayokuja na pia kulindwa kwa mazingira pale ambapo athari itajitokeza. Kwa kweli iko haja ya sisi sote tuwapongeze wataalamu wetu hawa kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nne niwashukuru Wajumbe wangu wote wa Kamati pamoja na Makatibu wetu kwa kuweza kunipa msaada mkubwa wakati wote tulipokuwa tukiupitia na kuujadili mswada huu muhimu kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo sasa naomba niwataje Wajumbe wa Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
5. Mhe. Said Omar Said	Mjumbe
6. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohammedali	Mjumbe
7. Mhe. Bahati Khamis Kombo	Mjumbe
8. Mhe. Kadija Omar Kibano	Mjumbe
9. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
10. Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu; na
11. Ndg. Himid Haji Choko	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru sana makatibu wetu hawa kwa kazi kubwa waliyoifanya kuweza kuhakikisha kwamba marekebisho wanayaweka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niungane na Mhe. Waziri kwa kuelezea kuwa mswada huu ukipita na kuwa sheria itakuwa ndio ufunguo wa uchumi mkubwa kwa nchi yetu na unaweza kuitoa nchi yetu na wananchi wetu kutoka katika umaskini na kuwa nchi yenye uchumi wa kati jambo ambalo litawafanya wananchi wetu wa Zanzibar kuishi maisha mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile sote hatuna budi tumpongeze na tumshukuru Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutupatia njia ya kuweza kuiwezesha Zanzibar kuwa na mamlaka yake yenye katika kushughulikia masuala yote yanayohusu rasilimali ya Mafuta na Gesi asilia hapa Zanzibar pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo, kwani uamuzi wake wa kuupeleka Mswada wa Sheria ya *OIL AND GAS REVENUE ACT YA 2015*, na kuanzisha Sheria Nam.2 ya 2015 ya Utawala, Ukuusanyaji na Usimamizi wa Fedha za Mafuta na Gesi, ambapo Kifungu cha 2 cha Sheria hiyo ndicho kilichoipa Zanzibar mamlaka ya kuweza sasa kutunga sheria yake yenye ya masuala yanayohusiana na mafuta na gesi, na hapa hivi sasa ndio tupo kuifanya kazi hiyo.

Kwa hiyo, kwa niaba ya Kamati tunamuombea dua Mhe Jakaya Mrisho Kikwete apumzike kwa salama nyumbani kwake na kulea wajukuu wake baada ya kilitumikia taifa kwa zaidi ya miaka 40. Tunamuombea afya njema yeye na Mama Salma Kikwete ingawa bado tunawahitaji kwa mawazo na mashauriano mbali mbali kila mara hasa katika kuweka sawa majadiliano pale yatakapojitokeza katika mustakbali wa suala hili hapo baadae, kwani tunaamini

wamestaafu lakini bado uwezo wa kufanya kazi wanao, na vile vile wana uwezo wa kutoa ushauri wao mkubwa kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni wa aina yake na ni mara ya kwanza kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunga Sheria kwa jambo la Muungano na kutoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kuweza kutunga Sheria kwa jambo la Muungano ambalo limo nje ya mipaka yake yaani jambo la Muungano, kwani Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 64(2) ambapo kimetoa mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria ambazo sio za Muungano ambazo zimo kwenye mamlaka ya Zanzibar, lakini Bunge la Jamhuri ya Muungano pia limepewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 64(1) na kifungu cha 64(4)(c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kutunga Sheria ambazo ni za Muungano na zile za Tanzania Bara. Lakini kwa umuhimu wa suala hili nyeti la rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bunge imeona kwamba iko haja sasa ya kutunga sheria ili kuweza kulipa mamlaka Baraza la Wawakilishi kutunga sheria kwa jambo hili ambapo hadi sasa bado liko kwenye orodha ya 15 ya mambo ya Muungano, ndio maana leo hii tuko hapa kutunga sheria hii ya mafuta na gesi hapa Zanzibar kupitia sheria hii.

Suala hili limekuwa na mjadala muda mrefu, miaka mingi huko mitaani kuhusu Zanzibar kuwa na mamlaka yake katika jambo hili. Pia kwa niaba ya kamati yangu naomba kuwatoa wasiwasi wananchi wote wa Zanzibar kuwa rasilimali hii itakuwa chini ya mamlaka ya Zanzibar tena kwa asilimia 100. Kwa mujibu wa kifungu cha (2) cha Sheria ya *REVENUE MANAGEMENT ACT* ya 2015 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio iliyoipa mamlaka Zanzibar kuweza kutunga sheria yake ya Mafuta na Gesi na kuipa Zanzibar mamlaka ya kushughulikia masuala hayo.

Kwa hiyo, sasa ni wajibu wetu kuichangamkia fursa hii ambayo tuliihitaji kwa muda mrefu, na kwa ushahidi Baraza hili tukufu la Wawakilishi kwa wakati huo lilipitisha kwa kauli moja Wawakilishi sote tulikuwepo wa Chama Tawala pamoja na Chama cha Upinzani kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia kwenye orodha ya mambo ya Muungano ili kuipa Zanzibar uwezo wa kushughulikia masuala ya uchimbaji wa mafuta na gesi.

Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba leo tumepeata nafasi ya kuweza kulishughulikia suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo niliyoyaeleza hapo juu, lakini bado ipo haja kubwa kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukamilisha mchakato wa Katiba iliyopendekezwa na Bunge la Katiba, ili wananchi wapate fursa ya kuipigia kura ya maoni na kuipitisha ile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili suala la Mafuta na Gesi liwe sio tena jambo la Muungano, kwani ni suala ambalo tayari kwenye katiba hiyo lilikwishingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama sio hivyo basi, Bunge la Jamhuri ya Muungano kufanya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ili kuondoa kabisa suala hili la Mafuta na Gesi kwenye orodha ya Muungano, kwani Katiba ndio yenyne nguvu na hakuna sheria yoyote yenyne nguvu inayokiuka Katiba. Kwa maana hiyo, tunaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka Bungeni Mswada wa Marekebisho ya Katiba kwenye orodha ya 15 ya mambo ya Muungano ili kuipa nguvu za kikatiba sheria hii tunayoitunga hapa leo. Sio hili tu, pia lipo suala la Bandari ambapo Zanzibar tumetunga Sheria ya Shirika la Bandari na hadi leo inatumika tena vizuri bila ya matatizo yoyote, lakini bado limo katika orodha ya mambo ya Muungano. Sio hayo tu, pia kuna suala la *TRA* hadi leo lipo katika orodha ya mambo ya Muungano lakini mapato yanayokusanywa Zanzibar yanaingia moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unatumika bila ya matatizo yoyote. Kwa maana hiyo, tunaamini na sheria hii tukiipitisha basi itaweza kufanya kazi vizuri bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya mambo ya Muungano ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili mambo yawe sawa kwa mujibu wa Katiba ya Muungano, na kwa sasa mambo haya wakati wake umefika ili yafuate utaratibu wa kisheria. Kwa maana hiyo, tunamuomba tena Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuileta Katiba inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wananchi tuipigie kura ya maoni ili tuweze kufaidika vizuri na rasilimali hizo nilizozitaja hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako sasa naomba kuingia kwenye uchambuzi wa mswada wenyewe. Aidha, naomba Wajumbe wote waujadili mswada huu kwa pamoja na marekebisho tuliyofafanya kamati kurekebisha *spelling* pamoja na kuboresha lugha iliyotumika pamoja na kufuta na kuvibadilisha baadhi ya vifungu ili kuufanya uwe bora zaidi na kuleta maana iliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuingia kwenye mswada wenyewe nitaomba ruhusa yako kidogo nijaribu kuizungumzia sera ili tujue sera imezungumza vipi na mswada umeoana vipi na hiyo sera.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulipokabidhiwa mswada huu ambao tunaujadili hivi sasa haukuwa na marejeo ya Sera ya Mafuta na Gesi Asilia na ilituwia vigumu kuufahamu msingi na muongozo wa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia, kwani suala hili ni kubwa tena lina changamoto nyangi sana kiuchumi na kijamii. Sasa sera hiyo ndio inayotoa msingi wa sheria itakayotungwa na kuainisha ni namna gani wananchi watakavyolindwa, na ni hatua gani zinahitaji kuangaliwa kwa karibu zaidi. Pia kuangalia matokeo ya baadae na kuweka tahadhari huko mbele tunakokwenda ili kusije kukatokea migogoro, mivutano ya jamii au kuumiza wananchi hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Kamati yangu tumepata bahati ya kupatiwa *copy* ya Sera hiyo hivi karibuni ingawa hadi leo tunapojadili Mswada huu Wajumbe wengi bado hawajaipata jambo ambalo sio zuri sana kwetu, lakini pia hata sisi tulipatiwa basi iko katika lugha moja tu ya Kiingereza. Kwa hiyo, tunaiomba serikali yetu kuitafsiri Sera hiyo kwa lugha yetu ya Kiswahili, ili Wajumbe na wananchi wengi waweze kuielewa vizuri zaidi inatoa miongozo gani ili pale itakapotokea kukiukwa basi wananchi wetu waweze kuelekeza Sera vile inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukue muda wako mwingi kuzungumzia suala la Sera kwani tayari baada ya kuipitia kwa kifupi yale mambo mengi ambayo yametolewa muongozo kwenye Sera hii basi yamewekewa kwenye msingi madhubuti wa Sheria ya Mswada huu. Kwa mfano, kuonesha ni kwa sababu gani na viashiria gani hadi kuweko Sera hiyo, kuweka tahadhari kwa wananchi kuhusu matumaini na matarajio ya wananchi, kutoa tahadhari vile vile kwa wananchi ili kutokuja kuigawa nchi yetu kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimajimbo na kuepuka mgawanyiko wowote wa kijamii kwa suala hili la mafuta na gesi. Pia imejibu miongozo na ushauri wa viongozi na wanasiasa mbali mbali kwa nyakati tofauti kutamka kuwa Mafuta na Gesi yapo Zanzibar, na tupewe mamlaka ya kushughulika wenyewe.

Vile vile Sera imeelezea dalili zinazoonesha kuwa hii rasilimali ipo kutokana na nchi zilizotzunguka kuwa karibu zote zimo katika harakati za utafiti na karibu zote tayari wameshagundua kuwa hii rasilimali ipo. Kwa hapa Zanzibar katika tafiti hizo ndio maana tayari vimeshakatwa Vitalu karibu vitano huko Baharini ambapo imeonakana dalili kubwa kuwa Mafuta au Gesi na hapo ndio maana Vitalu hivyo tayari kuna Makampuni ya Uchimbaji wa Mafuta tayari yalikwishakutia saini baadhi ya makubaliano ya awali, na *TPDC* ambayo ilikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo hapo mwanzo ambapo ndio waliokuwa wamepewa dhamana ya kushughulikia suala hili, na hii ndio dalili ya mwanzo

ya kuwa na hapa kwetu Zanzibar hii mali ipo. Lakini isitoshe Zanzibar katika miaka ya nyuma kuliwahi kufanyika utafiti na kugundulika ipo dalili kubwa ya kutosha kuwa rasilimali hii ya mafuta na gesi ipo hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Sera imetoa miongozo kwa namna kushughulikia maeneo ambayo yako zaidi ya maili 200 baharini ambayo yametambuliwa na Sheria ya Kimataifa inayoshughulikia na kutawala maeneo ya mipaka ya kimataifa *United Nations Law of the Sea (UNCLOS)* ambapo tayari Jamhuri ya Muungano imeshapeleka maombi ya kuongeza maeneo yake kwa upande wa Bahari kuu ambapo ikikubaliwa tu ni dhahiri kwa kuwa sheria hii itakuwepo tayari ni moja kwa moja kuwa na maeneo ya Zanzibar yataweza kushughulikiwa chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sera imetoa muongozo kuwa rasilimali hii iwekewe mipango madhubuti kuanzia mapato, matumizi lakini pia kuboresha Sekta nyingine za kiuchumi ili iweze kuja kuwanufaisha vizazi vijavyo, lakini pia kutoa tahadhari kwa kuimarisha sekta nyingine, kuibua sekta mpya za kiuchumi ili kuongeza wigo wa ajira na mapato kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwa Wazanzibari wote.

Vile vile kuimarisha huduma za Afya, Elimu, miundombinu lakini pia kujenga kizazi kilichoelimika kisayansi na Teknolojia ili kuondokana na utegemezi wa wataalamu huko tunakokwenda kuhakikisha nchi inapiga hatua kubwa za maendeleo katika nyanja zote.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona niichambue kidogo haya ni mionganoni mwa mambo mengi yaliyomo katika Sera yetu ya mafuta na gesi kwa faida tu ya Wajumbe wenzetu ambao hawakubahatika kuipata Sera hiyo, lakini kama nilivyoeleza hapo mwanzo mambo mengi yamezingatiwa kwenye Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kuingia kwenye mswada wenywewe.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kifungu cha (1) cha mswada ambapo Sheria hii itaanza kutumika mara tu baada ya Waziri kuutangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inamshauri Mhe. Waziri kuhakikisha kuwa mara tu baada ya Mhe. Rais kuutia saini Mswada huu basi asichelewe kuutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili iweze kufanya kazi, kwani hivi sasa macho na masikio ya wananchi wote wa Zanzibar wanausubiri kwa hamu kubwa, kwani utakuwa ndio nuru ya matumaini yao hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya pili ya Mswada huu unaelezea ni namna gani rasilimali hii itakavyomilikiwa na wananchi moja kwa moja kupitia kwa serikali, kwani vibali na leseni zote hazitotolewa moja kwa moja kwa kampuni yoyote itakayokuja, isipokuwa ni lazima ipitie kwa Kampuni ya Taifa ambayo itakuwa ni wakala wa serikali kwa Kamati ya Maendeleo ya Petroli ya Zanzibar (ZPDC).

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo, hakutokuwa na Kampuni yoyote ya nje itakayowenza kufanya jambo lolote bila ya uwakala wa Kampuni ya Serikali, hii nilioitaja hapo juu. Hii inaonesha wazi kwamba wananchi watakuwa ndio wamiliki moja kwa moja wa rasilimali hii ya Mafuta na Gesi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imeridhika sana, kwani uchumi huu ni mkubwa sana Duniani kwa kumuachia Mamlaka makubwa Waziri peke yake inaweza kuhamasisha rushwa kubwa hapo baadae, lakini sheria hii ili kutekelezeka hata baada ya kuupitisha na kutiwa saini kuna kazi kubwa ili kuanza kutumika. Kwani ni lazima mara tu baada ya kupita sheria ni lazima iundwe Mamlaka, pia iundwe Kampuni ya Taifa ya Mafuta na Gesi, lakini pia iundwe na Bodi ambayo ndiyo itaweza kufanya kazi taasisi hizi tatu tafauti ndio zitakazowenza kufanya kazi ya kuweza kumshauri Mhe. Waziri.

Pia isitoshe mara tu baada ya kuupitisha Mswada huu kuwa Sheria Waziri anatakiwa atunge Kanuni kwa haraka sana ili Sheria hii iweze kutekelezeka. Kutohana na umuhimu huo, Kamati yangu inamuomba sana Mhe. Waziri kuanza kutayarisha Kanuni haraka iwezenakanavyo ili sheria hii iweze kufanya kazi kwa haraka, kwani uzoefu wetu umeonesha ziko sheria nyingi ambazo zinahitaji kutungiwa Kanuni, lakini hadi leo bado kanuni hizo hazijaweza kutungwa na baadhi ya mawaziri. Kwa hiyo, ni jambo linazorotesha utendaji kwa baadhi ya maeneo. Pia, katika utekelezaji mzuri wa sheria hii waziri ametakiwa kuandaa Sera ya Mafuta na Gesi Asilia, tunashukuru sana kwamba tayari ipo na kwa kiasi fulani imekidhi mahitaji ya Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha (6) cha Mswada kimeelezea kazi na wajibu wa Waziri, Kamati yangu mwanzo ilikuwa na wasi wasi mkubwa wa mamlaka makubwa aliyopewa Waziri kwenye Sheria hii lakini tumejiridhisha kuwa Waziri takriban karibu mambo yote atakayoyafanya atayafanya kupitia ushauri wa Mamlaka pamoja na Bodi ambayo itakayoundwa kupitia Sheria hii, na hata baadhi ya maamuzi makubwa basi itabidi aidha apate ridhaa ya Baraza la Mapinduzi.

Kama inavyoelezwa kwenye orodha ya kifungu hicho cha 6 na vifungu vyengine katika Sheria hii, ingawa hapa tunatoa angalizo kwamba sheria hii maamuzi makubwa tunaruhusu yafanywe na Serikali pekee, isipokuwa tu pale Waziri alipotakiwa kutoa taarifa ya fedha au taarifa ya utekelezaji kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini kwenye Sheria ijayo ambayo itazungumzia masuala ya makubaliano ya masuala ya mapato ya Mafuta na Gesi katika mambo ya miongozo ya kodi na matumizi na migao ya rasilimali kuna baadhi ya mambo hayo mengine itabidi lazima yapate ridhaa ya Baraza la Wawakilishi katika sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha (6) (2) cha Mswada huu kama Sera inavyoelekeza kinampa majukumu Waziri kwa kumtaka kuongeza ushiriki wa jamii katika sekta hii ya Mafuta na Gesi, ikiwemo uwazi, mambo mbali mbali hii ndio itawewezezesha wananchi kujua taarifa nyingi na pia kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi katika Sekta hii ya Mafuta na Gesi. Pia imeeleza kuwa atahakikisha mipaka sahihi ya maeneo yanayotumika katika masuala ya mafuta na Gesi asilia suala hili ni la pande mbili; kuna mipaka ya ndani watakayopewa makampuni kukatiwa vitalu na mipaka mingine ya vitalu ambavyo imepakana na nchi nyingine za jirani. Kwa maana hiyo tunamshauri Waziri kuwa awe muangalifu sana pale atakapokuja kushauriwa na wataalamu wake wakati wa ukataji wa ugawaji wa Vitalu kwani vile vile kuanza mapema kuitambua mipaka ya eneo letu la Zanzibar na nchi jirani ikiwemo ukanda wa Bahari kuu, kwani migogoro mingi duniani na nchi nyingi duniani zenye uchumi huu wa Mafuta na Gesi kumetokea kwenye Vitalu vilivyoko mipakani.

Jambo ambalo limepelekea vita katika nchi hizo na nyengine hadi leo zinaendelea na vita hivyo zinaendelea na kuwaacha wananchi wasio na hatia hasa kinamama na Watoto wamekuwa ni wahanga wakubwa kutokana na maumbile yao kutokumudu vurugu na vita.

Leo katika nchi hizo badala ya rasilimali hii kuwainua kiuchumi matokeo yake imekuwa ni balaa kubwa kwao kupelekea uharibifu wa mali zao na kupata ulemavu wa maisha na wengine kupata vifo.

Kwa hiyo, Mhe Waziri na Serikali kwa ujumla hapa ndipo kwenye mtihani mkubwa katika sekta hii ya Mafuta na Gesi asilia, lakini tunaamini viongozi wetu ni watu wenye busara, wenye maarifa makubwa akiwemo Mhe. Rais Mhe. Waziri mwenyewe pamoa na wataalamu wetu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Tunaamini jambo la mwanzo ambalo atawenza kulishughulikia watatumia njia za Kidiplomasia kwa kushirikiana na viongozi wenzao wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na nchi jirani kwa yale maeneo ambayo tumepekana.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 6(2)(d) cha Mswada huu kinalezea kuwa Waziri atahakikisha uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika kuendeleza mfumo wa usimamizi wa mapato na ukusanyaji wa kodi na mipango ya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki bado hakijatuhakikishia Wajumbe kuwa Waziri aliyetajwa katika Sheria hii kuwa ndiye atakayekua msimamizi unaohusu masuala ya mapato na matumizi, kwani hadi hivi sasa tunapitisha sheria hii hatujatunga Sheria ya *Revenue Management Act*, ambayo itakayotoa dhima ambayo itakayokuwa na dhima na miongozo ya usimamizi wa masuala ya makusanyo ya mapato ya Mafuta na Gesi asilia na mipango mingine ya matumizi ya fedha zitakazokusanywa katika sekta hii. Kwa hiyo, kwa biashara hii ya mapato, biashara hii mapato yake huanza kukusanywa mapema pale mwanzo tu Makampuni yanapokuja na kuanza kutia saini makubaliano ya awali yaani *Memorandum of Understanding* basi tayari fedha japo kiasi kidogo huanza kukusanywa kabla ya mapato mengine baadae ya kukodisha Vitalu, na utoaji wa leseni.

Kutokana na *speed* kubwa ya Makampuni kuanza kupiga hodi basi tunaamini *MoU* hautomalizika mwaka mmoja tayari kuna makubaliano Serikali yetu itaanza kuingia na baadhi ya makampuni wataingia makubaliano ya awali katika vitalu vya Zanzibar na fedha za kodi zinaendelea kulipwa huko *TPDC* ambapo wao ndio walikuwa na mamlaka hiyo hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti ndio maana kamati yangu inashauri kuwa sheria hiyo ije mapema ili kuanza kukusanya fedha, kwani kuanza kuingia katika mfuko mkuu wa Serikali moja kwa moja bila ya kutengenezewa masharti maalumu zinaweza kuja kutumika kwa mambo mengine na kushindwa kutumika kwa misingi iliyowekwa na Sheria husika, lakini hapa kinachotakiwa zaidi ni nia njema ya udhibiti wa mapato na matumizi hayo, kwani ukizingatia hata kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano kipo kifungu (133 na 134 ) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachotaka kuwepo *Account* ya pamoja ya makusanyo na mapato yote ya Muungano na yatumike kwa shughuli za Muungano pamoja na maelekezo, pamoja na timu ya pamoja itakayoundwa. Lakini hadi leo suala hili halikutekelezeka, kwa hiyo kitu ambacho kamati yangu inashauri kwamba itungwe hiyo sheria, lakini vile vile iweko na nia njema ya kuweza kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaitaka serikali kuhakikisha sheria hii kama nilivyosema hapo mwanzo inaletwa haraka iwezekanavyo hapa Barazani ili tuipitishe, kwani hatua katika biashara hii kuna mapato mengi yataanza kukusanywa mapema kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwani kama nilivyoeleza hapo mwanzo kuna masuala ya vibali nya awali, kuna leseni, kuna masuala ya mirahaba na mambo mengine ambayo yamewekwa katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kama kinavyooleza kif. 6 (2)(g) kuwa Waziri atahakikisha kuwa kunakuwepo uwiano wa upatikanaji wa mahitaji ya ndani na usafirishaji mafuta nje ya nchi ili kuona wananchi wanafaidika na rasilimali hiyo, hili ni jambo muhimu sana kwa uchumi wa taifa letu, kwani ili sekta hii iweze kufanya kazi zake vizuri basi ni lazima kuwepo na miongozo maalumu ya kudhibiti soko la ndani na lile la nje, kwani iko mifano hai ya nchi ambazo zinazalisha Mafuta lakini upatikanaji wa huduma hiyo ndani ya nchi zao unakuwa ni mgumu sana, na hata bei wakati mwengine inakuwa ni juu na kuwapelekea wananchi kukosa kuona ile faida ya rasilimali hiyo ndani ya nchi zao, na baadae husababisha vurugu na uasi dhidi ya viongozi wao.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ya tatu ya mswada ina vifungu 25 kuanzia Kifungu cha (7 hadi 32) ambavyo vinalezeza muundo wa vyombo mbali mbali vitakavyowajibika katika Sheria hii ikiwemo Mamlaka, Kampuni pamoja na Bodi, kama Sera ilivyolekeza.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo hivi vyote ni muhimu katika Sheria hii, lakini Kamati yangu imekuwa na usoefu katika mashirika mbali mbali ya serikali kuwa hayana mamlaka ya moja kwa moja katika mipango yao ya kazi hasa katika miundo yao ya utumishi, lakini pia kwenye matumizi ya fedha ambazo wanazalisha kwani pesa zote huingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, na hata inakuwa vigumu na inachukuwa muda mrefu kuweza kupata marejesho yao ya pesa hizo kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao. Jambo hili hupelekea kuwapangulia kazi zao walizojipangia kwa kila awamu na wakati mwengine hupewa nusu ya zile walizopangiwa, sasa kwa sekta hii ya Mafuta na Gesi, Kamati yangu inatoa tahadhari mapema, kuwa wao wanafanya kazi na makampuni yenye uwezo mkubwa na fedha nydingi, na kila kitu kinatakiwa kiwe juu ya mstari.

Vile vile, jambo jengine ni suala zima la kuitambua miundo ya taasisi na kuweza kuwalipa stahiki zao kama vile wataalamu na bodi watakavyoweza kushauri.

Vile vile katika Sekta hii kwa kutumia uzoefu wa taasisi zetu kutokuangaliwa stahiki zao zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana taasisi hii iweze kupatiwa fedha wakatazozimba kwa wakati, kwani tunategemea wataalamu wengi ambao tutakaowasomesha kwa gharama kubwa lakini pia kwa kuzingatia maslahi yao na ili tusije tarajia kuja kukimbiwa na wataalamu hao.

### **MAMLAKA YA UDHIBITI, UTAFUTAJI, UENDELEZAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI**

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaiomba serikali kuchekecha na kuteua Wajumbe walio makini sana kwenye Mamlaka hii ambao watakuwa wataalamu, weledi, waadilifu na pia wenye uzalendo, kwani hawa ndio watakaokuwa ni washauri wakuu wa masuala yote ya Mafuta na Gesi asilia kitaalamu, kwa kuanzia hatua za awali hadi hatua za uzalishaji na ukomo wa shughuli hizo. Pia, wao ndio watakaokuwa washauri wakuu kwa Waziri kwani mikataba na mambo karibu yote yatakayotoka kwenye Kampuni kwenda kwa Waziri basi wao ndio watakaokuwa washauri wakubwa wa kitaalamu kabla ya Waziri kuchukua hatua nyingine au kufanya maamuzi ya kiutendaji, ikiwemo kutoa au kufuta vibali na kuangalia na kudhibiti uzalishaji pamoa na mpango kazi wa makampuni ya uzalishaji wa makampuni haya ya uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kuhakikisha inasimamia ushindani ulio sawa kwa makampuni yatakayokuwepo katika uzalishaji eneo hili ndio gumu sana kwani wakirubuniwa tu wataalamu wetu basi haitotendeka haki na ndio maana tukasema ni lazima na maslahi yao yazingatiwe mapema, kwani kazi zao zinaambatana na fitna kubwa ya fedha na rushwa, kutoka kwenye makampuni makubwa yatakayokuwepo hapa nchini. Lakini pia watakuwa na uwezo wa kutoa ushauri wa adhabu kwa makampuni watakaokiuka au kuzuia utekelezaji wa sheria hii, tunaamini maoni yetu serikali itayazingatia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili kamati yangu imegundua kuwa hadi hivi sasa wataalamu tunao lakini bado ni wachache sana, na wengi wao wanayo taaluma ya darasani zaidi lakini iko haja kwa hivi sasa aidha hawa wataalamu tuliokuwa nao au walioko vyuoni kuanza kuwapatia mafunzo ya vitendo kwenye maeneo ya uzalishaji, ili kujua hasa mazingira ya kitaalamu kwenye kazi yenye, na wizara tulipowauliza wamejipanga vipi katika kuikabili hali hii. Ingawa pamoa na kwamba walitwambia kuna vijana karibu 60 wako katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi kujisomea masuala ya Mafuta na Gesi,

lakini Kamati yangu bado haijaridhika kwani karibu vijana wote hawa aidha wanajisomesha wenyewe kuititia Mkopo wa Elimu ya juu au wanalipiwa na wazee wao moja kwa moja, na wachache ambaao wanalipiwa na Serikali na mpaka sasa hivi hawa wote niliowatataj pamoja na kwamba wapo Vyoni, bado hawajaajiriwa na serikali. Kwa hivyo Kamati yangu inaiomba Serikali kuhakikisha vijana hao wote ambaao niliowatataj hapo juu wanaajiriwa mara tu baada ya kurudi nyumbani ili kuwadhibiti, kwani hadi sasa tunahesabu ya wataalamu ambaao bado hatuna udhibiti nao.

## **BODI YA WAKURUGENZI WA MAMLAKA**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia imeupitia muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ukimuacha Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais kwa masharti ya Sheria hii, na wajumbe wengine watakaoingia kwa nafasi zao. Kamati yangu imefanya marekebisho na tunamshukuru Mhe. Waziri amekubaliana na marekebisho hayo nayo na kwa wale maafisa ambaao walotajwa kwenye sheria hii kwamba watakaoingia kwa nafasi zao kutoka katika Wizara tofauti, tumependekeza lile neno "Maafisa" liondoshwe basi liwe maafisa waandamizi ambaao watakuwa na uzito katika maamuzi ya vikao, kwani majukumu ya Bodi hii yatakuwa ni mazito na lazima wawemo wajumbe wenyе maamuzi makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu kifungu cha (12)(h), Kamati yangu ilipendekeza neno "Afisa" liondoke na iwe "Muwakilishi mmoja kutoka sekta binafsi". Mhe. Mwenyekiti, marekebisho haya kamati yangu imeyafanya baada ya kuona katika ule muundo wa Bodi kwamba kulitakiwa awepo mjumbe mmoja katika sekta binafsi pamoja na kwamba uzito wa suala hili karibu asilimia mia moja ni la Serikali Kuu, lakini bado Kamati yangu inaendelea kushauri kwamba bado nafasi ya mjumbe mmoja wa kutoka sekta binafsi atakuwa hatsoshi, ni vyema basi akawepo zaidi mjumbe mmoja, kwani katika Sekta hii mpya hapa kwetu tunahitaji watu wenyе maarifa makubwa ambaao wamebobea katika masuala ya biashara na kiuchumi ambaao wako nje ya Serikali na ambaao kuwemo kwao kungeliweza kusaidia sana kutoa maarifa na ushauri wa kiuchumi na utaalamu katika Bodi, kwani Sekta Binafsi imejawa na wabunifu wengi ambaao wamejiimarisha katika biashara na fani nyingine nyingi za kiuchumi, bila ya kusahau pia Waziri muhusika na Sheria hii ni vyema aangalie na jinsia katika uteuzi wa nafasi hizo za Ujumbe wa Bodi, kwani katika Bodi nyingi hapa kwetu zimesheheni wajumbe wa jinsia moja tu na kuiacha jinsia nyingine ikikosa kutoa mchango wao kwa Taifa.(Makofî)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa hivi sasa nchi yetu imejaa wataalamu wa fani mbalimbali wa jinsia zote, basi Kamati yangu inamuomba sana Waziri aliangalie hilo hasa kwa kuwa Waziri wa mwanzo wa Mswada huu au atakayesimamia Sheria hii ya Mafuta na Gesi ni mwanamke. Kwa hiyo kamati yangu kwa mara ya kwanza inatarajia kupata Bodi hii mpya itakayosheheni jinsia hiyo nyengine nilioitaja hapo juu ambayo ilioachwa nyuma kwa muda mrefu ikipewa nafasi kubwa na ikiwezekana hamsini kwa hamsini. (*Makofii*)

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 16 naomba Wajumbe wasome pamoja na Jadweli la kwanza lililoko kwenye Ukarasa wa 130 wa mswada huu linalozungumza mienendo ya vikao vya Bodi ya Wakurugenzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imefanya marekebisho katika jadweli la kwanza liliopo ukurasa wa (130) na kukiandika upya kifungu cha (1) na kusomeka kama hivi ifuatavyo:-

- (1) Bodi itakutana kikao cha kawaida angalau mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu (3).
- (2) Bodi inaweza kukutana katika kikao cha dharura wakati wowote inapohitajika kufanya hivyo.
- (3) Vikao vya Bodi vitafanyika ndani ya Zanzibar, isipokuwa ikijitokeza haja ya kikao nje ya Zanzibar baada ya kupata ushauri au ridhaa ya Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, hayo ni marekebisho ambayo tuliyofanya katika jadweli la kwanza ambalo lipo ukurasa wa 130 wa Mwenendo wa Vikao Vya Bodi.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho haya tumeyafanya ili kuzuia mianya ya kufanyika vikao vya Bodi nje ya nchi bila ya sababu za msingi, kwani usoefu unatwambia ziko baadhi ya Bodi katika nchi jirani wamewahi kufanya vikao vyake vya Bodi nchi za Ulaya bila ya sababu za msingi wakati ndani ya nchi zao kuna kumbi nyingi za mikutano tena zenye viwango vya Kimataifa, lakini kwa vile pesa ziko za kutosha basi waliamua kufanya vikao vyao hivyo nje ya Nchi. Kwa hivyo, kwa kuwa Sekta hii ya mafuta na Gesi Asilia ni Biashara ya Kimataifa basi watu wanaweza bila ya sababu za msingi wakaamua kuichukua nafasi hiyo au kuitumia fursa hiyo ya kufanya vikao vyao vya Bodi nje ya nchi katika Nchi za Ulaya au nchi nyengine mbali mbali. Lakini Kamati yangu bado katika marekebisho hayo tumetoa nafasi kama itabidi kufanyika vikao nje ya nchi basi ni lazima wapate ruhusa kwa Waziri kama nilivyoeleza hapo mwanzo, na kueleza sababu za msingi kwa maslahi ambayo Waziri atayaridhia.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kwenye jadweli hilo hilo kifungu cha 11(1) kinachoelezea nafasi tupu ya mjambe, Kamati yangu inapendekeza kuongezwa maneno kwa "miezi kumi na mbili mfululizo" baada ya neno "ugonjwa", kwani kumekuwa na mifano hai kuwa ziko Bodi ambazo inatokezea mjambe anakuwa mgonjwa zaidi ya mwaka mmoja anashindwa kuhudhuria katika vikao na hakuna mabadiliko yoyote yanayofanywa kwenye Bodi hizo na kusababisha kukosa michango muhimu ya mawazo katika Bodi hizo, na kwa maumbile ya kazi za Bodi hii wajumbe wanatakiwa washiriki kikamilifu katika maamuzi yote ya Bodi.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 19 (2) kinaelezea wakuu wa Idara na vitengo vyengine wataoteuliwa na Bodi kwa mujibu wa vigezo na masharti mengine ambayo yatakayohusiana na Sheria inayohusiana na Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti eneo hili sina haja ya kulirejea kwani matatizo yetu au hofu yetu ndio ile ile kuja kutokuzingatiwa maslahi yao pamoja na ile miundo yao ya kiutumishi.

## **KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA**

Mhe Mwenyekiti, Kifungu cha 32 (1) kama alivyoelezea Waziri Kifungu hiki kinaanzisha Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi ya Taifa (ZPDC) ambayo itashiriki moja kwa moja katika biashara ya utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kama wakala wa Serikali au kwa niaba ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, uanzishwaji wa Kampuni hii ndio matumaini makubwa kwa wananchi wa Zanzibar, kama ilivyoelekeza au ilivyotolewa muongozo kwenye Sera ya Mafuta na Gesi, kwani inatudhihirishia kuwa rasilimali yetu hatopewa mgeni ye yote isipokuwa atapewa kuititia uwakala wa Kampuni ya ZPDC, hapa tunawapongeza sana wanasheria wetu pamoja na wataalamu wetu wa ndani ambao ndio waliotengeneza Sheria hii na kujali maslahi mapana ya wananchi wetu wa Zanzibar. Kwani ziko nchi nyingine hapo miaka ya nyuma na nyingine hadi leo ni watu binafsi ndio wanaomiliki visima vya Mafuta na Gesi na kujitengeneza utajiri mkubwa wakiwaacha wananchi wa nchi hizo kwenye umaskini wa kutupwa. Lakini katika sheria yetu hii Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru sana wanasheria wetu pamoja na wataalamu kwa kuweza kuanzisha kampuni hii ambayo itasimamia maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 32(4), Kamati yangu inakubaliana na nia ya Serikali kwa Kampuni ya Serikali kumilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja na suala hili ni muhimu sana na lisachwe tu kwenye Sheria hii peke yake

bali tunapendekeza lije liingizwe kwenye Katiba ya Zanzibar ambapo itakapokuja kufanyiwa marekebisho na kubadilishwa kwake basi iwe kwa kura ya maoni ili wananchi waamue, kwani inawezekana siku moja akaja akatokea Rais mwenye tamaa akalishawishi Baraza lake la Mawaziri, pamoja na Baraza la Wawakilishi kuirekebisha Sheria hiyo na kutoa mwanya kwao kununua hisa katika kampuni hii ya Serikali na kujitajirisha kupitia rasilimali ya wananchi, na jambo hili sio geni, kwani hapa hapa Tanzania kuna baadhi ya watu waliwahi kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwamilikisha Vitalu ili kutafuta wawekezaji wa nje waweze kuyauza kwa kuingia ubia na makampuni hayo ya nje.Kwa hiyo kwa suala hili basi ni vyema maamuzi makubwa kama hayo ni lazima yawekewe masharti magumu kupitia kura ya ridhaa ya Wananchi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Mswada huu, ina vifungu 79, kuanzia kifungu cha(33 hadi 109 ).

Aidha, kifungu cha 33 kinalezea mgao wa maeneo ya Ardhi kwa ajili ya Vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia kama ramani itakavyoelekeza baada ya kuthibitishwa na Mamlaka na Waziri kupata idhini ya Baraza la Mawaziri, lakini kabla ya Waziri kufungua na kutangaza maeneo hayo ya Vitalu, ni vyema kama maelekezo ya Kifungu cha 34 (2) na (3) (a), (b), pamoja na (i) hadi (vi), hadi Kifungu cha (11) ni lazima kwanza ifanyike tathmini ya Mazingira ambapo Waziri atazingatia athari kwa jamii ikiwemo wamiliki wa maeneo hayo kuchukuliwa na kuweza kufidiwa. Hapa Kamati yangu inaomba hii fidia watakayolipa wananchi iendane na bei ya soko na sio kuangalia Sheria ya Ardhi ambayo kwa wananchi wengi wamekuwa wakiilalamikia sana kuwa haiendani na wakati kwani fidia wanayoipata wengi hivi sasa imewaingiza kwenye umaskini wa kudumu badala ya kuwasaidia kuendeleza maisha yao, na hili tumeliona wenyewe kwenye maeneo ya uwekezaji wa mahoteli, wananchi wengi wamebaki kuwa maskini kwa kulipwa fidia ndogo wakati uwekezaji wa mahoteli ukiendelea kuingiza mamiloni ya shilingi.(*Makofii*)

Kwa hiyo, ni vyema katika sheria hii, ni vyema hiyo fidia kwa wananchi iwekwe kwa mujibu wa soko na sio kama ilivyo hivi sasa, ili fidia hiyo iwe endelevu kwa wananchi na kufaidika na matunda ya uwekezaji huo mpya na utakaokuwa ushiriki bora kwa wananchi katika biashara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama Sera ilivyoelezea taarifa na tathmini ya mazingira ndio itakayotoa maelekezo mazima na hatma ya uwekezaji na tathmini hii itatoa

mwanga kwa Maendeleo ya Taifa hapo ikiwa Kilimo, Uvuvi ambao unaweza kuathirika na vile vile kuweza kuijandaa na kupambana na changamoto zake.

Vile vile, kwenye Sekta na biashara ya utalii ambayo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini pia athari nyengine za kijamii ikiwemo uingiaji wa watu kiholela hasa watakaoingia nchini kuja kutafuta ajira katika sekta za Gesi na Mafuta pamoja na sekta nyengine, lakini pia kudhibiti mfumko wa bei wa bidhaa na maingiliano ya jamii katika kulinda utamaduni wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, tathmini ya mazingira iangalie sana athari kubwa inayowapata hasa akinamama na Watoto hasa kwa udhalilishaji, ni vyema tathmini iangalie zaidi ni vipi akinamama watawezesha kuijajiri na kuajiriwa kwani bila ya kuwawekea mipango madhubuti basi watakuwa wanaendelea kubakia masikini na kuwa watazamaji tu na kujikuta baadhi yao kuijingiza kwenye mambo ambayo siyo mazuri kama ilivyo kwa baadhi ya nchi zeny uchumi wa mafuta na Gesi Asilia, pia ni vyema kuimariswa Skuli za amali ili kuwawezesha vijana wengi kupata taaluma ya kuweza kuajiriwa kwenye sekta hii ya Gesi na Mafuta au kuijajiri wao wenywewe, ni lazima kuwekwe mafungu maalumu kwa ajili ya kutoa taaluma kwa jamii kwenye uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, tathmini ya Mazingira pia iangalie sana zile shughuli za kiuchumi zitakazoathirika moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida na kuwaandalia shughuli mbadala zitakazoendesha maisha yao pale zitakapokuja kukatishwa kutohana na uwekezaji huu mkubwa katika nchi yetu, kwa mfano wenzetu Nigeria kwenye bonde la Niger Delta, bomba la mafuta liliwahi kupasuka na kupelekea mto ambao wananchi wakiutumia kwa shughuli zao za kilimo, pamoja uvuvi hata ndege waliokuwa wakitumia mtoule tumeshuhudia wakiathirika sana pamoja na kufa kutohana na kuvuja kwa bomba hilo la mafuta. Kwa hivyo biashara hii ni nzuri lakini pia ni vizuri kuweza kuijandaa na changamoto zitakazokuja kujitokeza hapo baadae, na haya yote yatakuwa mepesi ikiwa jamii itashirikishwa mapema na kupewa taaluma ya kutosha ili na wao kuijandaa na hayo mabadiliko yatakayoweza kujitokeza.

## KIBALI CHA UTAFITI WA AWALI

Mhe Mwenyekiti, sehemu hii imeanzia kifungu cha 33 hadi 109. Kwa kuzingatia kifungu cha 35(1) cha Sheria hii inaelezea hatua mbali mbali za kuanza utafutaji wa Vibali na Leseni na vibali nya ruhusa ya uzalishaji. Sehemu hii ndio hatua muhimu itakayokuwa inayotakiwa kuwa na usimamizi mzuri kama Sera ilivyoeleza, kwani katika hatua hii Makampuni tayari yanakuwa yameshajifunga kuingia katika mikataba na Serikali kwa ajili ya

utafiti, uchimbaji, uzalishaji na uendelezaji wa rasilimali hii, na hapo na sisi wajibu wetu mkubwa ni kuangalia maslahi ya wananchi wetu kama Sera ilivyoeleza, kwa kuwa wananchi wetu wamejenga matumaini na kuona shughuli hizo wananchi wetu ili waanze kufaidika au kunufaika moja kwa moja kuititia taaluma, ushirikishwaji katika uhaulishwaji wa maeneo yao na pia kuandaliwa na fursa zitakazokuwepo kuititia uwekezaji huu mkubwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili, Kamati yangu inaiomba tu Serikali kuangalia zaidi kwa yale maeneo ambayo yamehifadhiwa kwa ajili ya shughuli maalumu ya hifadhi ya viumbe hai ikiwemo wanyama, misitu, na shughuli nyingine za kijamii ikiwemo maeneo ya makaburi yaani maeneo ya kuzikana na mengine ya kijamii, lakini hapa cha muhimu ni kuangalia ni kipi kitakacholeta tija zaidi, tusije tukazuia kutoa vitalu eti kwa sababu kuna vyura ambaio ni adimu hapa Duniani, hapo kikubwa ni kuangalia tija na vile Sheria hii kama inavyoeleza kuwa waziri atatoa kibali basi ahakikishe matakwa yote ya Sheria hii pamoja na masharti yale ya Mazingira yamefuatwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu kuanzia hivi sasa kuandaa wataalamu wa kutosha katika Sekta hii ya Mafuta na Gesi kwani mara tu baada ya Sheria hii kuititia basi kuna harakati za kuanza kwani pia kwenye huo utafiti wa awali basi ni lazima kuwashirikisha wataalamu wetu wa ndani na wathibitishe na kujiridhisha kwa kila hatua ya utafiti. Vile vile ili kuhakikisha taarifa hizo zinakabidhiwa Serikalini katika hali ya usahihi na kusiwe na mwanya wa kuziachia Kampuni za nje na kuziuza taarifa hizo na kujipatia mapato ambapo yalitakiwa yaingie Serikalini, na mapato hayo kama tulivyoshauri mwanzo ni vyema yakaanza kuwekewa utaratibu mzuri wa kisheria na kuhakikisha zinatumika zaidi katika kuboresha au katika kusomesha wataalamu wetu wa ndani na kuimarisha miundombinu ya ofisi zao pamoja na vitendea kazi, hasa tukizingatia shughuli hizo ni za kisayansi zaidi. Kwa hiyo tunatakiwa tuwe na vifaa vyta kisasa ili kuweza kupata *Data* sahihi kwa muda wote, pamoja kuwa kwa hivi sasa hatuna vifaa vyta kisasa vyta kuweza kukusanya taarifa za utafiti, ni vyema basi tukaandaa mazingira ya kuwa na kituo chetu cha utafiti hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia Sheria hii imempa mamlaka Waziri kwa kutoa kibali cha awali kwa Kampuni na kuhakikisha masharti yote yaliyowekwa na Sheria hii na kuangalia tathmini ya Mazingira na kupeleka mpango kazi wa Kampuni, kwa hiyo kama haya yote yatazingatiwa basi wananchi wetu wataweza kufaidika sana na Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama kifungu cha 49 (1) kinalezea kuwa ni lazima Kampuni itakayopewa leseni iwe na uwezo na uzoefu katika shughuli za uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kusiwepo mwanya wa kuja kuipa leseni Kampuni ambayo haijawahi kufanya kazi yoyote hapa Duniani, kwani hayo tumeshayashuhudia kwa baadhi ya miradi mengine ambayo inafanyika hapa kwetu, na matokezo yake kuitia hasara Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 50 (1) kinalezea hifadhi ya Vitalu. Katika eneo hili Kamati yangu inaishauri Serikali kuhifadhi baadhi ya Vitalu kwa matumizi ya baadae ya nchi lakini pia kufanya tathmini kubwa ya kutosha kabla ya kuvitoa na kujiridhisha rasilimali iliyoko kiasi gani, kwani kuna baadhi ya nchi waliwahi kukata Vitalu vikubwa na kuwapa Makampuni ya nje na baadae waligundua kuwa wamewapa vitalu vikubwa kimoja kinatoka vitalu vitatu na kuikosesa mapato makubwa Serikali na hivi sasa wameanza kupunguza ukubwa wa Vitalu hivyo kwa kuzingatia tathmini au kwa kuzingatia utafiti uliopatikana. Kwa hiyo hapa kuna changamoto kubwa hasa katika maeneo ambayo tumepakana na wenzetu Jamhuri ya Muungano ambayo tayari vimeshatolewa vitalu hivyo kupitia mikataba ya huko nyuma, sasa tukijakugundua kwamba vimetolewa na imeonekana kuwa ni vikubwa sana, sasa hapo ndipo busara zije kutumika ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Zanzibar yanazingatiwa ipasavyo.

Pia kamati yangu inashauri wakati wa ugawaji wa vitalu hivi, basi kuwapatia makampuni makubwa tofauti yenye uwezo mkubwa na isipewe kampuni moja, kwani biashara hii ni vizuri ukaiwekea makampuni tofauti, kama wenzangu walivyoleza kwamba mayai huwezi ukayatia kwenye kapu moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waziri yejote atakayekaa katika wizara hii, atakuwa na mtihani mkubwa wa kimaslahi hasa katika eneo la kutoa, na kuongeza muda wa leseni, hapa ni vyema mawaziri wakawa waadilifu, kwa kusikiliza na kufuata ushauri wa wataalamu, kwani eneo hili ndilo linaloweza kuwafanya makampuni yatakayokuwepo kupata usawa miiongoni mwao, na sio makampuni mengine kupewa upendeleo.

## **LESENI**

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia masharti ya Kifungu cha 51 (1)(e) moja ya masharti ya kampuni kupata leseni ya kuchimba mafuta na gesi, ni kuwasilisha mpango kazi wake na kuonesha ni mipango gani walinyonayo katika kutoa elimu na mafunzo kwa wazawa, ili kuweza kuziba pengo la wataalamu wa kigeni, kuwapisha wataalamu wazalendo baada ya kupata utaalamu huo na

kuweza kushika nafasi muhimu za kitaalamu na kiufundi. Katika mpango huu utawahakikishia wazawa, yaani wananchi wa Zanzibar kuweza kuajiriwa na kushika hatamu kubwa za kiutawala, kwani tumeshuhudia nchi mbali mbali zinazochimba mafuta na gesi, wananchi wao hivi sasa ndio wamekuwa wataalamu wakubwa na viongozi katika makampuni mbali mbali makubwa ya mafuta hapa duniani.

Ukiacha utaalamu mkubwa pia kampuni ioneshe ina mpango gani wa kutoa mafunzo ya ajira kwa wananchi wa kawaida, hasa ambao wanaishi katika maeneo ambayo miradi hiyo itakuwa inafanyika. Kwa kuzingatia hayo, pia waziri amepewa nguvu kwenye kifungu cha 52(1), ili kuhakikisha wananchi wazalendo wanafaidika na kila hatua ya utekelezaji wa mradi huu. Tunawashukuru sana wataalamu wetu kwa kuweza kuliona hili.

## **LESENI YA UENDELEZAJI**

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 63(1)(a – f), kimeelezea masharti ya kupata leseni, kwa Kampuni ya Serikali na kampuni za nje. Katika eneo hili kumekuwa na hofu kubwa kwa watu mbali mbali waliosoma mswada huu kuhusu utoaji wa Vibali vya Utafiti wa Awali, Leseni na Leseni za uendelezaji, labda kwa kuhisi kuwa kuna uwezekano mkubwa wa baadhi ya makampuni kupewa vibali vya awali na baadae kuja kunyimwa leseni za uendelezaji hapo baadae. Nadhani eneo hili tuwatie moyo sana wananchi wetu. Kwa masharti haya kamati yangu imeyakubali, ili kuhakikisha kuwa tunapata makampuni yenye uwezo mkubwa na sio makampuni ya ubabaishaji, kwani biashara hii ni kubwa na kampuni yoyote ikija kutaka leseni, basi wataweza kufuata masharti yote ya sheria hii na kuweza kuzalisha mali ya kutosha, kwani hatutegemei kuwa zitakuja kampuni kuomba leseni na kutumia mapesa mengi bila ya kuwa na uhakika na wanachokifanya, kwani kwa mujibu wa sheria hii kampuni ikishindwa kazi katikati njiani, basi serikali haitolipa chochote na chote kilichowekezwa kitakuwa mikononi mwa serikali kupitia kampuni ya serikali kama hiyo niliyoitaja hapo juu.

Kwa hivyo, wajumbe na wananchi tuone ni jinsi gani sheria hii ilivyowajali na kuwalinda wananchi wake. Lakini pamoja na kuwa kamati yangu imeridhia hatua hizo, lakini pia iko haja waziri utakapokuja kutoa ufanuzi, ili kuendelea kuwatoa hofu zaidi wawekezaji wa nje na kuwa hakuna matarajio ya kuipa kampuni kibali na baadae kuwanyima leseni ya uendelezaji kama hofu ilivyotanda huko nje, hili litazidi kuwatia moyo makampuni ili kuja kuwekeza Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia kampuni itakayopata leseni ya uchimbaji na uzalishaji inatakiwa kuonesha kujenga uwezo wa utaalamu na uzalendo, pia kutoa ajira kwa wananchi kama sera inavyotoa muongozo na kuwawezesha wazalendo. Aidha kuonesha njia za kiusalama kwa wafanyakazi pamoja na afya zao na jamii, vile vile hatua zitakazotumika wakati wa dharura na hii itawaondolea hofu wananchi, kwani tumeshuhudia ajali za kuripuka kwa visima vyta mafuta, kupasuka kwa mabomba ya kusafirishia mafuta na gesi na watu wanavyoathirika. Kwa hivyo, ni vyema mipango yao ikaonesha mapema ni jinsi gani wananchi wataweza kulindwa, na makampuni yataweza vipi kukabiliana na majanga kama hayo ya dharura pale itakapotokezea.

### **KIBALI CHA UZALISHAJI**

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 71 (1) kinaelezea namna ya waziri atakavyoweza kutoa kibali cha uzalishaji baada ya Mamlaka kujiridhisha na hatua zote tangu kibali cha awali, leseni, leseni ya uendelezaji na hatimaye kumshauri waziri kutoa kibali cha uzalishaji. Baada ya kujiridhisha na hatua hizo zote, pamoja na kuwa ni mlolongo mrefu, lakini sheria hii inaonesha ni jinsi gani serikali yetu ilivyokuwa makini kwa kupitia mamlaka itakayokuwa makini, kufuutilia kila hatua ya uzalishaji na ndio maana tukasema ni lazima serikali kuangalia sana maslahi ya wataalamu katika mamlaka hii itakayoundwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 72(5) kinaelezea iwapo mkusanyiko wa mafuta unaendelea hadi nje ya mipaka ya Zanzibar, serikali itafikia makubaliano na nchi nyingine ili kuona mgawanyo wa mapato unaenda vizuri, na hapa ndio pale kamati yangu ilipoishauri serikali mara tu baada ya kupita sheria hii na kutiwa saini, basi suala la mwanzo ni kuangalia mipaka yetu ili kuweka utaratibu mzuri wa uvunaji wa rasilimali hii kubwa hapa duniani. Lakini pia itazitoa hofu kampuni za nje zitakazokuja kutaka kuwekeza katika vitalu vyetu vyta Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imeridhika na mfumo mzima wa uwazi kwa kila hatua, tangu kampuni kualikwa, kupewa vibali vyta awali, lakini pia kuwajulisha wananchi kupitia tamko la serikali kwenye Gazeti la Serikali, kama Kifungu cha 84(1 na 3) kinavyoolezea. Sheria hii inaonesha ni jinsi gani walioandaa mswada huu, walivyokuwa makini katika kulinda maslahi ya umma pamoja na mpango mzima wa kazi, ambapo wananchi wataweza kufaidika kwa kuitumia fursa hiyo.

## **MASHARTI YA JUMLA**

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 77 (1) kinaelezea masharti ya jumla, ikiwemo kuweka kumbukumbu za rajisi, za mikataba ya Makampuni ya Mafuta na Gesi Asilia na kweka kumbukumbu za makubaliano na mabadiliko mengine yote ya katika mikataba. Pia kifungu cha 77(2) kimeelezea kuwa rajisi zitakuwa wazi kwa umma, isipokuwa kama maelekezo mengine ya kisheria yatakavyooleza.

Vile vile Kifungu cha 79(2)(a - j) kinaelezea kuhusu maombi ya kuhaulisha hati baina ya makampuni, ambapo waziri anahitajika kuyaridhia. Hili ni suala jema, kwani tumekuwa na uzoefu huko nyuma kwa wamiliki wa mahotelii mbali mbali ya kitalii kuhaulishana mikataba yao au ya hisa, bila ya kuijulisha serikali na matokeo yake kuikoseshaa serikali mapato yake.

Jengine kwenye kifungu cha 82 ambacho kinazitaka kampuni kuwasilisha kumbukumbu za ugunduzi na taarifa nyingine kwa mamlaka, ili kujua ni ugunduzi gani umeonekana na kuifanya serikali kutoa miongozo ya nini cha kufanyika hapo baadae kutokana na taarifa mbali mbali.

Kifungu cha 89 kinawabana makampuni ya nje kuhakikisha kwamba uzalishaji unatosheleza soko la ndani. Aidha, kifungu cha 89(2) kinadhibiti kutokupindukia hisa ya faida katika kampuni na mkandarasi.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 94 (1 - 3) kinatoa miongozo kwa makampuni yatakayopewa leseni kutochimba chini ya masafa maalumu yaliyowekwa kwenye mikataba, ili kuepusha kuja kuingiliana kwenye mipaka na kusababisha uvunaji wa mafuta kutoka kwenye vitaluu vinavyokaribiana, na hapo ndio mara nyingi hutokea ugomvi baina ya nchi na nchi au baadhi ya makampuni kwa kuibiana rasilimali hiyo ya mafuta na gesi. Hapa serikali inatakiwa iwe makini hasa Mhe. Waziri, kama sheria inavyomuelekeza kuhakikisha kwamba, hakuna kampuni itakayopewa kitalu kuchimba zaidi ya mita 1,000.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 98(1) kinaelezea kuhusu haki ya matumizi ya ardhi, kwa mkaazi halali eneo la uchimbaji wa mafuta na gesi, na shughuli za ufugaji, kilimo au ufugaji ambaa hautaathiri shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ambapo mwananchi hatoruhusiwa kujenga jengo lolote bila ya ridhaa kwa maandishi ya kampuni, au kama akikataa bila sababu waziri anaweza kutoa kibali bila kuathiri maslahi ya mkaazi.

Suala hili ni vyema wakati wa utekelezaji wake basi wahusika wawe makini katika kufikia makubaliano, kwani jirani zetu katika hizi nchi za Afrika ya

Mashariki, kuliwahi kutokea mgogoro mkubwa baina ya wananchi wa kijiji fulani na serikali, kwani serikali ilikusudia kufanya shughuli za maendeleo, lakini wanakijiji walikuja juu kuzuia eneo lao serikali isiweze kufanya mradi huo, na matokeo yake ikasababisha maisha ya watu kupotea. Kwa hivyo, hii iwe kama ni tahadhari kwetu. Vile vile kifungu kidogo cha(4) kinaelezea kampuni kuonesha mpango kazi, ambapo kama kuna maeneo yatakayoweza kuathirika ni mipango gani atawea kushughulikia, ikiwemo sekta ya uvuvi, usafiri wa majini, isipokuwa itaijulisha mamlaka kwa kuzingatia maslahi ya wananchi pia ni eneo la kuzingatia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu haikukubaliana na Kifungu cha 99(1) cha mswada huu, kwani kinaelezea makaazi ya mwananchi atakayeathirika kupata hasara katika eneo lake au mazao yake, basi atalipwa fidia kwa kutumia sheria ya usimamizi wa ardhi iliyopo hivi sasa. Hii haitakuwa haki, kwani sheria yetu ya usimamizi wa ardhi imeshapitwa na wakati, kwani inaelezea kuwa ardhi ni mali ya serikali na itakapotaka kuitumia kwa shughuli yoyote ya maendeleo, basi mtu huyo atalipwa fidia aidha kwa vipando au kile alichokiwekeza hapo juu. Kwa hivyo, kamati yangu inapendekeza kuwa, mtu atakayeathiriwa katika shughuli zake za kiuchumi, basi alipwe kwa mujibu wa thamani ya soko au tathmini itakayofikiwa. Kwani uzoefu unatwambia hivi sasa katika ukanda wa maeneo ya utalii, kama nilivyoleza pale mwanzo, kwamba watu wengi wamelipwa fidia ndogo na sasa hivi wamekuwa maskini. Vile vile wengine ambao walikuwa wakitumia ardhi ile kwa kilimo, sasa hivi hawawezi tena kuwa na ardhi ya kilimo. Kwa hivyo, fidia kamati yangu inapendekeza iwe endelevu

## **MRAHABA**

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 101 kinaelezea namna ya mgawanyo wa mapato ya mafuta na gesi asilia, kama inavyoonekana katika ukurasa wa 133 wa sheria hii.

Mhe Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe waangalie ukurasa wa 133, ni namna gani serikali itakavyoweza kupata mirahaba au zile *shares* (his) zake au gawio lake. Hapa ndipo wajumbe na wananchi wengi pamoja na wadau wengine, ndipo wanapopasubiria kwa hamu ufanuzi wake wa kina, ili waweze kuridhika na kuona faida watakayoipata wananchi, yaani *Production Sharing Agreement* kwa ufupi wake ni (*PSA*).

Kwa maoni ya kamati baada ya kupata semina kutoka taasisi tofauti, za wataalamu wa nje na vile vile na wataalamu wa wizara, kamati yangu

tumeridhia na tumeona kuwa serikali itafaidika sana kupertia mgao huo, na hakutokuwa na hasara kwa serikali, kwani kutakuwa na migao ya aina tatu.

Mgao wa mwanzo kwa maeneo ya nchi kavu, serikali itapata asilimia 15.5% na asilimia 7% kwa upande wa baharini. Kwa kuzingatia ugumu na uzito wa kazi hiyo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, asilimia iliopo hapo juu basi itakuwa ni nzuri sana tu kwa serikali.

Pili, ni mgao atakaojilipa mkandarasi na kurejesha gharama zake yaani *cost oil* na

Tatu, wakati wa uzalishaji faida itakayopatikana ya mauzo ya mafuta au gesi kuanzia mwanzo, serikali itaanza kupata asilimia 50 kwa 50, kuanzia pipa moja hadi mapipa 12,499 kwa eneo la nchi kavu. Kwa hivyo, asilimia ya serikali itakuwa inapanda kila wingi wa uzalishaji wa mapipa ya mafuta utakavyokua. Kwa hivyo, serikali tunategemea kwa niaba ya wananchi itaweza kupata mapato makubwa sana, hasa kwa kuzingatia kwamba mwanzo serikali inakuwa haikutoa hata shilingi moja katika uwekezaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, mkandarasi atapata asilimia 50 kwa 50 katika hatua ya mwanzo ya uzalishaji na kila uzalishaji unapoongezeka yale mapato ya asilimia ya mkandarasi au ya kampuni ya nje, yatakuwa yanashuka kwa asilimia 5 na mapato ya serikali yatakuwa yanapanda kwa asilimia 5, hadi kufikia asilimia 70 kwa 30, ambapo serikali itapata asilimia 70 na mwekezaji atapata asilimia 30.

Vile vile ukiacha hiyo pia serikali kama jadweli la pili linavyoeleza, kwa upande wa baharini kama hapo mwanzo nilivyoeleza, vile vile serikali itaendelea kupata mapato yake kutoka katika asilimia ya huyo mkandarasi wa kigeni au kampuni ya kigeni, vile vile asilimia ile itaweza kulipiwa kodi, kwa hivyo kodi ile pia itaweza kuingia serikalini. Kwa hivyo, mapato mengi serikali inategemea kuyapata kupertia kwenye mgao huu.

Mhe. Mwenyekiti, sio hivyo tu, bali katika Kifungu cha 102 kinachozungumzia kampuni na mkandarasi watalipa ada ya leseni ya kila mwaka, pia hayo yatakuwa ni mapato ya serikali, ambapo pia itajumuisha kodi na ada za mafunzo ya utafiti. Pamoja na malipo hayo, kuna malipo ya ziada ambayo kampuni na mkandarasi watalipa serikali, kutokana na maelekezo ambayo waziri atatunga kanuni hapo baadae na kuidhinishwa na Baraza la Mapinduzi. Kutokana na hayo yote ambayo nimeyaelezea, ndio maana kamati yangu imeridhika na mapato hayo ambayo serikali itayapata, kama yalivyowekwa katika jadweli na miongozo mingine ya sheria hii.

Mhe Mwenyekiti, pamoja na kamati kuridhika na mapato hayo yote, lakini bado tunahitaji sheria ya udhibiti na matumizi ya fedha za maendeleo kama ilivyoelezwa huko mbele, sheria hii ndio itakuwa muhimu katika kusimamia matumizi ya fedha hizi.

### **UKOMO WA SHUGHULI ZA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA**

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ina vifungu 7, kuanzia cha 110 hadi 117, ambacho kinaelezea masharti ambayo kampuni na mkandarasi wataeleza mpango wa ukomo wa mradi wao, na masharti yaliyowekwa na sheria hii ni mazuri, kwani kampuni na mkandarasi atalazimishwa kupeleka mpango huo miaka mitano kabla ya shughuli hiyo kufungwa au kabla ya kitalu hicho kufungwa, na itasaidia serikali kujua ni maeneo gani ya kuyasimamia kwa karibu, ili kuhakikisha kwamba mradi ukimalizika, basi maeneo hayo yanaendelea kutumika kwa shughuli nytingine za kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha mpango huo wa ukomo unakuwa unadhibitiwa baada shughuli kukamilika. Kifungu cha 111 kimewekewa masharti ya kuanzishwa mfuko wa ukomo wa shughuli hizo na mfuko ambaa utaweza kugharimia shughuli za uondoaji wa miundombinu yote ambayo haitohitajika tena, na pia kuyarejesha maeneo katika hali yake ya kawaida, kama tathmini ya mazingira itakavyoeleza ili yawewe kutumika kwa kuzingatia masharti hayo ya mazingira kama nilivoyoyataja, lakini katika eneo hili tunaiomba serikali kuwa makini sana na hatua za mwisho, kwani mkandarasi akishamaliza kurejesha gharama zake alizotumia, mitambo yote itakuwa ni mali ya serikali, na mpango huo wa ukomo itabidi uoneshe ni namna gani inaweza kutumika tena na serikali au kuondolewa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo jambo kubwa la muhimu ni kuona masuala yote ya uharibifu wa mazingira yamezingatiwa ipasavyo kama inavyoeleza katika Kifungu cha 131 cha sheria hii. .

### **TATHMINI YA WADAU**

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ina vifungu 5 kuanzia 134 hadi 138, sehemu ambayo inaonesha ni jinsi gani wananchi wa kawaida watafaidika moja kwa moja na shughuli za mafuta na gesi asilia, kwenye masuala ya elimu, afya, maji safi na salama, kushirikiana na wafanyabiashara wazalendo katika kuinua na kuzitumia bidhaa zao za ndani, vile vile kutoa kipaumbele kwa kutumia bidhaa zinazozalishwa ndani ya Nchi, pamoja na mambo mengine ya kijamii.

Mhe Spika, eneo hili ni gumu kulifahamu lakini kimsingi kwa uzoefu wa Nchi nydingi basi sisi tuko vizuri. Na tayari wapo Makampuni wameonyesha nia ya kukubaliana na masharti hayo yote katika hii sheria yetu.

### **MAKOSA NA ADHABU**

Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu 11 kuanzia cha 139 hadi 146. Kamati yangu katika sehemu hii haina pingamizi nayo kwani adhabu zilizotajwa zimezingatia ukubwa na uzito wa masuala haya ya Mafuta na Gesi.

### **UTATUZI WA MIGOGORO**

Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu 4 kuanzia kifungu cha 147 hadi 150 inazungumzia utatuza wa migogoro, sehemu hii inaelezea iwapo kutatokezea utata kwa Kampuni baina yao ambazo hazihusiani na Serikali, Mmalaka itaweza kuingilia kati na kuleta suluhu kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa.

### **MASHARTI YA MPITO**

Mhe. Spika, sehemu hii iko katika kifungu cha 151, kifungu hiki kama kilivyo kwa kweli kitaleta matatizo kidogo, kwa hiyo, kamati yangu inaomba kuondoa neno "haitokuwa na wajibu" badala yake kuweka neno kwamba "haitofungwa na mikataba yoyote". Sasa hili kidogo litakuwa ni suala zuri kwani tayari kuna mikataba ambapo huku nyuma ilikwisha kuingiwa.

### **MASHARTI YA JUMLA**

Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu 4 kuanzia, kifungu cha 152 hadi 155. Aidha, kifungu cha 154 kinaelezea kuanzisha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Petroli, Sheria hii ndio itakayokua msimamizi mkuu wa mipango yote ya maenedeleo ya Serikali ya sasa na ya hapo baadae na hiki ndicho kilio chetu kikubwa, wajumbe tunaiomba Serikali kuhakikisha Sheria hiyo inakuja hapa Barazani hivi karibuni ili kuweza kutimiza lengo la Sheria hiyo.

### **MWISHO**

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu inaishauri Serikali yetu katika hiyo mipango ya baade katika kuimarisha urchumi wa Zanzibar kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Petroli ambayo sheria hiyo itakuja hapo baadae kuangalia maeneo muhimu ya kukuza na kulinda utalii wetu, kuanzisha viwanda vyta kusindika samaki, kuimarisha sekta nzima ya uvuvi, kuimarisha miundombinu ya kilimo hasa kuchimba visima na kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili tujitosheleze na chakula cha ndani na cha ziada na kuuza nje.

Lakini vile vile kujenga na kuimarisha miundombinu katika Sekta ya *ICT*, kujenga na kuvimarisha vyuo vyta Amali, kuimarisha makaazi ya watoto

yatima na wazee wasiojiweza, kuanzisha Shirika la Ndege na kunua Ndege zake yenye, kuimarisha usafiri wa Baharini, kununua vifaa vya kisasa kwa vikosi vyetu vya SMZ, ili kuimarisha ulizni wetu wa Baharini na nchi kavu pia kuimarisha maeneo huru ya kiuchumi na kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati ili kuongeza ajira kwa vijana wetu pamoja na wanawake, vile vile, kuimarisha sekta ya ujenzi wa makaazi ya wananchi wetu mijini na vijijini pamoja na kuboresha vyuo vyetu na vifaa ili kutoa wataalam wengi wa fani mbali mbali hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama Sera inavyosema kua wananchi wamejenga matarajio makubwa sana kupitia sekta hii jambo ambalo la kuwaomba wananchi wetu ni kuwa wamoja na kuweka pembeni tofauti za kisiasa kwani bila ya utulivu wa kisiasa haya yote yatakua ni ndoto tu, baada ya hayo.

Mhe. Spika, Napenda kuendelea kuwashukuru tena Wajumbe wangu wote wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi kwa kuweza kutusikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliiano na Ujenzi, lakini pia niipongeze hii kamati chini ya Mwenyekiti wake kwa hotuba yao refu, lakini ina mantiki ndani yake kwa maslahi ya Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea muda wetu ni Saa 6.20 na wachangiaji ninao 8 mpaka sasa hivi, lakini naomba niwaambie Waheshimiwa Wajumbe, tutamuita mchangiaji wa kwanza na wa pili ambaye ni Suleiman Sarahan Said na Mhe. Rashid Makame Shamsi, kama muda utaruhusu nitamuita Mheshimiwa wa tatu Simai Mohammed Said wa Jimbo la Tunguu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Suleiman Sarahan, uchangie, lakini pia tuzingatie muda dakika zetu ni kumi na tano, tuanzie hapo twende kwenye mada husika au Mswada husika, tusiwe na maelezo mengi mwisho wake tukapoteza yale malengo ambayo umekusudia kuyachangia katika Mswada huu.

**Mhe. Mohammed Sarahan Said:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama, lakini pia kutuletea jambo jema na kubwa sana katika historia ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo yako lakini na mimi napaswa kupongeza kidogo kwa sababu tumpongeze sana Mwenyekiti wetu wa kamati kwa kazi kubwa alioifanya ambayo ameellezea mbele yenu kamati ilivyofanya kwa

mpango wote, lakini pia pongezi hizi zingeanza mbali sana kwa sababu tumpongeze sana Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein, aliyefanya jitihada kubwa mpaka jambo hili kulitia macho likaweza kuelezeza katika nchi yetu. Jambo hili limeanza tokea enzi za Sultani lakini mpaka leo limefikia tamati ya kuweza kuonekana katika hali hii inayoonekana.

Pia, tumpongeze Makamo wa pili wa Rais kwa ushauri wake na mambo yake, lakini pia tumpongeze Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudhi zake alizochukua kwa kuipatia Zanzibar suala hili ambalo liko mbele yetu, na pia tumpongeze Rais wetu John Pombe Joseph Magufuli ambae pia anatuunga mkono kwa yote, pia tulipongeze Bunge letu la Jamhuri ya Muungano kwa kutuunga mkono katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa hayo, lakini nataka niseme kitu kimoja, ni kwamba nchi yetu imepata jambo jipya kubwa sana hili, imepata jambo jipya zito sana hili, kwenye Kamati tumeshachangia na umeshasikia maelekezo yote. Lakini ningeomba wananchi kuitia Baraza la Wawakilishi jambo hili tukaweza kulipitisha ambalo ni jambo zito na kubwa ili kuweza kupata ukweli na uhakika wa suala hili katika jambo ambalo linakuwa na utata, linakuwa na ubishi, linakuwa la wanasiasa, linakuwa na fitna, linakuwa na tamaa, linakuwa na ushawishi, linakuwa na rushwa na uwongo.

Sasa Mwenyezi Mungu kwa vile kalijaalia jambo hili kulitia macho au kulielekeza katika mustakabali huu basi ningeomba wenzangu wa Baraza la Wawakilishi tukalipatia ufumbuzi kwa kuisaidia Serikali, ili ikaweza kujipima tumepata nini katika nchi yetu na tumekosa nini, tukajua tunajipanga na nini, sio kila siku mafuta yapo au hapana au gesi ipo au hapana, wanasiasa wanatumia maneno hayo, watu wengine wanatumia maneno hayo.

Lakini pia kuna mpaka makampuni ambayo yanatia ushawishi kwamba mna mafuta hamchimbi, kuna mambo mengi ambayo kwa kweli mpaka wataalam wanakuwa wakija kubabaisha watu wakiwaambia mafuta yapo, mwengine hapana, lakini tukipitisha Mswada huu wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia na Mungu akatujaaliya kwa utaaliam uliopo sasa hivi, tutajua nini kilichopo na kipi hakipo.

Kwa hivyo, ningewaomba wananchi na Baraza lako hili tukufu Baraza la Wawakilishi, tukaitambua kwanza mustakabali mzima wa suala hili la mafuta na gesi asilia, Mheshimiwa, jambo hili tukumbuke lina upeo wa kuchukua muda mrefu mpaka kuyachimba mafuta hayo na kuyapata kwa wataalam wanasema isiyopungua miaka minane, ndio tunaweza tukapata kuchimba

mafuta. Lakini katika utafutaji basi tunaweza kutafuta si chini ya miaka miwili na nusu mpaka miaka mitatu, kwa hivyo, tujipime tukijangalia, tusije tukaona kampuni, meli zimefunga gati kesho tukaanza kutiana vijiti kwamba mafuta yapo yanachukuliwa, pana mambo ambayo yatapita katika daraja fulani fulani, mojawapo ikiwa ni utafutaji, mojawapo baada ya kupata hapo kuna uchunguzi, tuna mafuta ya kiasi gani na ya aina gani na vitu gani tulivyonavyo, tunaweza kutafuta mafuta tukapata gesi, hatuwezi kujua kuna kitu gani mpaka wataalam watakapotufafanulia mambo haya ambapo hapa panachukua zaidi ya miaka mitano mpaka kupata uhakika kilichopo.

Baada ya hapo, tuna zaidi ya miaka miwili au mitatu kuunda miundombinu na ya kuyachimba mafuta, kwa hivyo, tunatakiwa ustahamilivu na upeo mkubwa wa kuweza kuyaelezea haya, kwa hivyo, wananchi wetu wayaelewe kwanzia sio kwamba kesho asubuhi tukiona tayari watu wameza maelekezo ya mafuta tukafuta mafuta yanachimbwa kesho. Tunaweza sisi tuliokuwemo humu tukawa hatutoyafaidi mafuta hayo na wakafaidi wenzetu, lakini ilimradi tumewawekea misingi mizuri basi watafaidika hao na sisi ndio itakuwa tumefaidika kwa sababu hata kama ukifanya jambo zuri litakukuta akhera, kwa hivyo, hili liwe jambo la msingi sana kuliangalia kwa upeo.

Lakini mimi nataka niendeleze kusema kwamba elimu inahitajika vya kutosha tena ya taaluma za wananchi kwa upeo mkubwa sana kipindi hichi ambacho tumo katika michakato yetu, basi Serikali pamoja na watu chungunzima pamoja na wanasiasa tukawapelekee ukweli wananchi wetu kuwaelezea masuala haya kwa kuijenga mustakabali wa kuijenga nchi yetu na wamanchi wetu, ambayo tusiwe katika kuingiza nchi yetu katika janga. Jambo hili ni jambo jema, Mwenyezi Mungu akilijaalia litakuwa jambo jema, lakini lisije likawa ndio hasara kwetu, kuna mifano ya nchi za wenzetu ambazo ni nyingi lakini hawakufaidika na matunda haya.

Ningewaomba sana wanasiasa na watu wengine tukaacha masihhara, tukaacha utani, tukaacha mambo yote, tukatizama mustakaboli wa nchi, asije mtu akatumia upeo wake kwa kujifaharisha yeche, chama chake na mambo mengine kwa kutumia Mswada huu akaiweka nchi katika pahali pabaya. Ningewaomba Serikali jambo hili lisiwe la masihhara, mtu yeoyote atakayekuwa kuchenza na masihhara haya, basi Serikali imuandame haraka iwezekanavyo, masuala haya ni masuala mazito ni masuala yanayotaka utaalam na wengi hatunao, kwa hivyo, tunaambiwa ni watu kwamba kuna hichi na hichi.

Lakini Serikali ndio itatoa tamko rasmi kupitia kwa wakandarasi wake tumepata nini, tumepata kitu gani na tutafaidika nini, Mhe. Mwenyekiti, nataka

nikwambie kwamba suala la mafuta ni suala ambalo sio kwamba kisima kama hata ukipata lita mbili unaweza ukasema unachota maji, kwa kiwango cha kimataifa mafuta haya yana viwango vyake vya kuweza kuchimba na kuweza kuuza ukaruhusiwa kimataifa. Ikiwa yapo tu yale yale ya juu tunaweza tusiruhusiwe yakawa kama ni mbolea kwetu sisi, kwa hivyo, ni vitu vizuri vya kuangalia na ni suala linalotakiwa ustahamilivu vya kutosha kuiweka nchi yetu katika masuala kama haya ili na sisi iwe mfano, tukipata mafuta Mungu akitujaalia yaje yatunufaishe sisi na vizazi vyetu.

Kwa hivyo, sio masihhara wanasiasa na wataalam waliokuwa hawajiamini na mambo mengine kutumia mwanya wa kuweza kuwatia pampu wananchi wetu ili kukosana na wananchi wetu kwa Serikali, lakini pia nataka niendeleze Mheshimiwa, Serikali imejitayarisha na imeshatayarisha sheria yake kwa ukweli nataka kuisifu na wananchi wote wameisikia ni kwamba inalinda maslahi ya nchi yetu na maslahi ya wananchi wetu. Mimi nataka nithibitishe Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna kifungu cha 99 cha Sheria hii kinasema;

"Endapo katika shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia, kampuni na mkandarasi wataingilia haki za mkaazi halali wa ardhi yoyote au watasababisha hasara kwa mazao miti, majengo, ghalaa, au kazi zinazofanywa na kulingana na shughuli zinazofanyika, Kampuni na Mkandarasi watamlipa mkaazi halali fidia inayofaa kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa ardhi."

Mhe. Mwenyekiti, hapa Serikali imetoea mwanya ili wananchi wake wasiweze kudhalilika au wakaharibiwa mali zao na wakakaa kimya, kuna kifungu cha 99 cha kwanza na cha pili ambacho kinamlinda Mheshimiwa, mtu atakayeharibiwa mali zake mpaka kwenda Mahakamani kudai haki, kwa hivyo, hii kwanza naipongeza Serikali kwa kifungu hichi cha kuweka bayana kwamba kila mtu atahakikisha anapata haki yake, na aliyejewa haki yake kidogo imeharibiwa basi anaweza akaipata Mahakamani au kwengineko.

Kwa hivyo, hili nilikua nataka niliseme wazi, wananchi watulie wafanye kazi zao na waweze kutulia kama tulivyo sasa hivi, Serikali na wao wanaona tutakopofikia pahala faida itakapopatikana, uwezo utakapopatikana kila mmoja atafaidika na suala hili. Lakini ningependelea sana tusiache kazi zetu, tusiwe na furaha kubwa sana tukaacha mambo yetu halafu tukaja tukawa jambo hili halikutuletea manufaa na baadae ikawa ni vita kwetu. Kwa hivyo, ningeshauri sana Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wakalielewa sana.

Lakini pia nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wazalendo ambao naweza kusema kwamba ndio watakaokuwa katika mambo ya watendaji na mambo mengine hasa haya mambo ya mafuta na gesi, masuala haya mengine ambayo tunayatumia Serikali kwenye hizi Idara za utumishi zikaangalia sana viwango nya kuwalipa hawa vijana ambao wanaingia katika fitna za gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta na wachimbaji wake na watu wake ni watu pesa, ukija ukimuingiza mtaalam katika masuala ya utumishi wa umma ikawa anaingia kwenye Serikali ya utumishi wa umma basi kuna hatari kubwa sana ya kuweza kupatikana fitna na rushwa katika vijana wetu ambao hawakutegemea wanajitolea wazalendo. Lakini tuwahakikishie maslahi yao yanakaa vizuri katika sekta hii.

Kwa hivyo, ningeomba sana vijana wetu hawa kwanza wakasomeshwa ili zile pesa ambazo tunaweza tukasema zinakuja za wataalam tunamlipa mabilioni ya pesa anayachukua anakwenda nayo kwao, bora kumtengeneza mtaalam wetu akaweza kufanya kazi hapa na akaweza kuwa-*train* na wengine na pia na ile pesa ikabakia katika nchi yetu. Hilo nimeliona mfano juzi nilipokwenda Songo Songo katika masuala ya gesi. Mheshimiwa, mle ndani katika kile kiwanda cha gesi kina wafanyakazi wasiopungua 17 wote ni vijana wa Kitanzania walio na elimu ya *engineer* na wapo katika hali nzuri sana mle ndani kiwanda kile wanakiongoza wao, hawana mtaalam hata mmoja, isipokuwa kuna Mchina mmoja aliyebakisha kwa kumaliza kazi ambazo za kiwanda, sio uendeshaji, wanaendesha Watanzania wenyewe, tulifurahi sana Mheshimiwa, wataalam wote wanatoka Tanzania na wanajisifia kufanya kazi ile na vijana tunao wanahitaji kuendelezwa na kuwekwa sawa Mheshimiwa.

Kwa hivyo, Mheshimiwa, ningependelea sana suala hili likatizamwa kwa upeo, lakini vile vile nataka kusema kwamba kwa hali inavyokwenda na mtazamo unavyojionyesha ni maelekezo mengi yanayohitajia mazingira, mazingira katika nchi yetu yanahitaji kuangaliwa kwa upeo, tumejasma sheria nyingi zimo humu lakini ningehitaji tuzifuate nya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, sisi katika bahati yetu tuna samaki wa jodari, nduwaro na wana maeneo yao na matumba na kila kitu, tumejaribu kuwafafanua humu kwamba sekta ambazo bado ni rasilimali hatutozichezea wala kuwapa nafasi wachimbaji mafuta wakaziharibu, kwa sababu mafuta yenyewe hatujajua kupatikana na kutokupatikana, naomba sheria hizi zifatwe ili tusije tukaharibu rasilimali halafu tukaja tukaa hatuna la kukamata. Tuchimbe pale ambapo tuna uhakika kuwa hatutoharibu miundombinu,

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wananchi wetu wanahitaji kufanya kazi zao hizi za kawaida mpaka pale watakapohakikisha kwamba mafuta yanakwendaje na aliyekuwa kapitishiwa bomba au kitu gani katika maeneo yake atalipwa. Kwa hivyo, ingekuwa ni vitu vizuri tukaviangalia kwa kina, tusije tukaanza kuharibu kabla hatujatengenea kuangalia maslahi yoyote.

Pia, nataka niseme kwamba kwa utaalamu nilioupata kwa masuala ya mafuta, miundombinu na hali ya hewa pamoja na mambo mengine yanagusa kama mambo manne; yanaunganisha Serikali, wananchi wake, Kampuni, pamoja na Kampuni nyengine ambazo zinakuja kutoka nje. Suala hili ni suala ambalo lina uzito mkubwa na kinachounganisha pale ni watu kukosa maslahi yao au kupata matatizo katika zile sehemu ambazo zitaonekana mafuta au kupita miundombinu. Lakini kitu ambacho nimejifunza kuna masuala haya ya jamii, Mheshimiwa, kule Songsongo walikuwa wanawambia kwamba kila panapopita lile bomba basi kila kijiji kinachopita bomba wamekaa kama wale watu wana mashirikiano makubwa na wanawalipa au wanasaidia miundombinu ya pale kama ulinzi kwa lile bomba.

Kwa hivyo, wale wana mtu kitengo ambacho kinatokea ustawi wa jamii, wa kuunganisha watu, wa kuunganisha mambo ilimradi pasitokee machafuko baina ya wananchi pamoja na Serikali au Kampuni ambayo inafanya vitu vile. Atafutwe mtaalam sio ni mtu ambaye anatoka kwenye Kampuni wa kwenda kuzungumza na watu, watafutwe watu ambao wana taaluma ambazo wapi miundombinu yetu itapita iwe kama ni ulinzi kwa vijiji, ambapo wale wanawambia kwamba wanasaidia sekta tofauti zile Kampuni. Sekta za Afya, Sekta za Elimu na watu binafsi ilimradi tu kama ni ulinzi katika bomba lile.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikikwambia kwamba masuala ya kwetu hasa Zanzibar tuna mazoea sana kwa mambo tunayofanya haya ya kuchezea miundombinu yetu ambayo tunaichezea kisiasa siasa na mengine hata sielewi, lakini tusije tukafanya masihhara na gesi, Kisiwa kitaondoka chote, huyo aliyefanya na wale waliomo wataondoka wote. Tuna matatizo ya kukata mikarafuu, lakini si masihhara ya mafuta na gesi. Ningemba sana wananchi wakaelewa vyakutosha na wanasiasa tujiingize wala tusiingize matatizo kwa wananchi wetu kuititia mradi huu.

Kwa hivyo, ningekuomba sana Mheshimiwa, ni suala ambalo linahitaji elimu ya kutosha kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, najua unakama *microphone* yako kwamba muda labda umekaribia kufika, lakini michango nimeshatoa nimeshasema lakini cha ziada nilikuwa naomba tu kwamba wajumbe wenzetu wote wa Baraza la Wawakilishi katika masuala haya ningemba suala la

kwanza ambalo tunalitaka kwa hivi sasa ni utafutaji, tusije tukatia maneno mengi, utafutaji, uchimbaji, uuzaji kitu gani, tunatafuta. Ningombu tuipe ruhusa wizara au Serikali ili itafute itupe uhakika wa suala hili ndio tuweze kuweka maelekezo mengine.

Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti.(*Makofit*)

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wananchi wa Magomeni kwa ridhaa yao ya kunichagua. Awali ya yote na mimi nishukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa pili katika mswada huu muhimu na wenyewe lengo zuri sana kwa taifa letu katika kuwalettea maendeleo wananchi wake. Nizishukuru Serikali zote mbili; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliona hili. Vile vile nichukuwe fursa hii ya kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake katika suala zima la kushughulikia sera na kuandaa mswada huu muhimu, lakini nitoe pongezi kubwa sana kwa Kamati inayohusika na Mawasiliano na Ujenzi kwa ripoti yao nzuri ambayo imesheheni ushauri na mapendeleko mengi sana kwa Serikali yetu. Nimpongeze kwa makusudi Mhe. Hamza, kwa uwasilishaji wake. Vile vile, nimpongeze na nimshukuru sana mjumbe mwenzangu aliyetangulia Mhe. Sarahani, kwa maelezo mazuri katika mchango wake.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee sasa na mimi katika suala zima la kuweza kuchangia mswada huu ambao sina wasi wasi nao kwa sababu umekuja wakati muafaka kwa maendeleo ya Taifa hili. Nianze na suala la elimu.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli ambao hatuwezi kuuficha kwamba elimu kwa watu wetu juu ya masuala haya ya mafuta na gesi bado ni ndogo. Niishukuru sana Wizara inayohusika kwa kuandaa sera na kuweza kuandaa mswada huu, lakini wananchi na hususan wananchi wa kawaida bado hawajapata elimu ya kutosha katika suala zima linalohusiana na mafuta na gesi katika nchi yao. Tukiangalia kwenye sera, sera yenye we tokea iandaliwe iko *version* ya Kiingereza, tunatarajiaje wananchi wa kawaida wanaweza wakapata hasa muelekeo wa Serikali katika suala hili la mafuta na gesi.

Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi karibu asilimia 20 tu labda ambao wana *awareness* ya sera hii ya mafuta na gesi, mpaka hivi sasa sisi Wajumbe hatuna sera hiyo, huwezi ukapitisha sheria pamoja na kwamba huna sera au huielewi sera. Sera ni nzuri ambayo tumeelezwa kwa muda mfupi tu inaonekana ni nzuri lakini *awareness* haipo kwa *society* yetu ya Zanzibar.

Ningependa sana nishauri katika hili kwamba Serikali baada ya kupitisha mswada huu ichukuwe juhudzi za makusudi kwanza kuweza kuitafsiri sera hii kwa lugha ya Kiswahili ambayo Wazanzibari wengi ndio wanayoilewa na iwe katika lugha nyepesi ambayo hata mwananchi wa kawaida aelewe nini mstakbalwa wa Serikali katika suala zima la uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi. Katika hili nimuulize Mhe. Waziri, ambaye nimpongeze kwa kuwasilisha atakapokuja aweze kutujibu, ni wadau wangapi wakiwemo wananchi wa kawaida wameshirikishwa katika kupitisha Sera ya Mafuta na Gesi pamoja na mswada huu tunaoujadili hivi sasa, hayo tunataka majibu atakapokuja Mhe. Waziri, ili tuweze kujiridhisha.

Suala la pili, linalokuja ni wataalam wetu walioandaa sera hii tuwashukuru sana na sheria wamefanya *visit* katika nchi ngapi zenyet mazingira yanayofanana na nchi yetu ambao wamepata maendeleo katika suala zima la kutafuta na kuchimba na mafuta na wale ambao wameambulia migogoro, Mhe. Waziri, atakapokuja aweze kutwambia juu ya wataalam wetu wametembelea nchi ngapi ambazo zinachimba mafuta zenyet mazingira sambamba au yanayofanana na yetu na zile ambazo zimepata maendeleo na zile ambazo zimeambulia migogoro ili kuweza kujiridhisha kwamba sera na mswada wetu huu wa sheria kwamba umezingatia *experience* na *practice* ya nchi mbali mbali.

Suala la tatu, ningependa Mhe. Waziri, atakapokuja atuambie kwamba Serikali yetu hivi sasa inajivunia wataalam wangapi ya fami hii mafuta na gesi na katika kada gani ili kuweza kuona kwamba hivi sasa tunajiridhisha kwamba tunao wataalam wetu ambao tutawatumia na watafaidika katika suala zima la kuendeleza suala hili la mafuta na gesi.

Suala jengine ambalo ningependa Mhe. Waziri, atakapokuja atuambie kwamba kutokana na kutokuwepo kwa mfumo unaoeleweka wa kimipaka, Serikali inatoa kauli gani katika Baraza hili kwa wananchi wetu ili kuepuka migogoro ya baadae tusiyoitarajia. Hayo masuala ningependa Mhe. Waziri, atakapokuja basi aweze kutuweka sawa ili na sisi tujiridhishe katika kupitisha mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika mswada wenywewe. Nije katika Sehemu ya Kwanza. Katika Sehemu ya Kwanza ambayo inahusiana na ufanuzi wa maneno mbali mbali. Kwanza nilivyochunguza hii *version* ya Kiingereza na Kiswahili inaonekana kwamba hakuna uwiano wa idadi ya maneno. Katika *version* ya Kiingereza kuna maneno 65, lakini *version* ya Kiswahili ina maneno 69, ningependa ufanuzi wa kisheria mpaka ikawepo hivyo na sijui ipi ilianza Kiingereza au ya Kiswahili.

Lakini mbili katika hapa ni mpangilio ambao unahisi una matatizo kidogo katika baadhi ya maneno ambayo yametolewa ufanuzi. Kuna neno "gesi" sehemu (g) hili neno "gesi" ambalo limetolewa ufanuzi, hapa lilipo tunahisi kwamba halipo pahala muafaka kutokana na mpangilia wa *alphabetical* ukurasa wa 67. Kwa sababu kumetanguliwa na maneno "gesi husishwa" na kumetanguliwa na "gesi isiyochanganyika", neno "gesi" lilipaswa liwe juu kuliko haya mawili.

Vile vile, kuna neno "kisima". Katika ukurasa wa 68 neno "kisima" limetanguliwa na maneno "kisima cha uendelezaji na kisima cha utafutaji". Nahisi neno "kisima" lilikuwa litangulie mwanzo. Lakini vile vile kuna neno "leseni" katika ukurasa wa 69, limetanguliwa na "leseni ya uendelezaji, leseni ya utafutaji", ninafikiri neno "leseni" lilipaswa likae mwanzo. Lakini vile vile kuna neno "mkandarasi", neno "mkandarasi' katika ukurasa huo wa 69 limetanguliwa na maneno "mkandarasi mdo", wakati ki-*alphabetical* ninafikiri neno "mkandarasi" lilikuwa litangulie mwanzo.

Lakini vile vile kuna neno "vitalu" katika ukurasa wa 72 hili neno "vitalu" hapa imetolewa maana yake ni eneo liliolezwa chini ya kifungu cha 33 cha sheria hii. Neno limesemwa vitalu lakini *statement* imeenda katika hali ya umoja. Kwa hivyo, ningependa likae sawa kama tunaamua ni kitabu au vitalu, lakini *statement* ikae katika uhalisia wake.

Vile vile, nije katika ushauri katika baadhi ya maneno kwa mujibu wa mswada huu kwa maoni yangu nahisi haya maneno yangetolewa ufanuzi. Neno "miundombinu" kwa mukhtadha wafuta na gesi lingetolewa ufanuzi. Neno "utafutaji wa mafuta", neno "ubia" na neno "uchafuzi wa mazingira".

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika mswada huu nikiacha katika ufanuzi nije sasa katika suala zima ukurasa wa 73 katika kifungu cha 6 kama sikosei, kinahusu kazi na wajibu wa Waziri. Wenzetu wa Kamati wamependekeza hicho kitu, lakini pamoja na mapendekezo yake na mimi nilikuwa na pendekoz jengine ambalo nahisi lingekaa vizuri zaidi kuliko mapendekezo ya Kamati linasema hivi;

"Waziri atatekeleza kazi na wajibu ufuatao:-

- a) Baada ya kushauriwa na mamlaka atatoa..."

Lakini kifungu hiki baada ya kushauriwa na mamlaka hapa kinachukua nafasi ya kifungu (a) tu, vifungu vinavyofuata haviwezi kubebwa na *stream* hiyo, sasa hiyo *stream* ingeweza kukaa wapi, ingeweza kukaa hapo kwamba, "Waziri baada ya kushauriwa na mamlaka atatekeleza kazi na wajibu ufuatao", halafu

vifungu vyote hiyo vinakubali katika *stream* hiyo. Ningependa ushauri wangu huo uchukuliwe na nipingane na ushauri wa kamati inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niekee katika ukurasa wa 74. Katika ukurasa huu kuna *printing mistake* katika kifungu cha 7(2) kwenye neno la mwisho linasomeka "hapo litaweza". Inavyotakiwa lionekane "itaweza" kwa sababu huku kilichotajwa imesema kwamba "mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, endelevu na chenye muhuri wake na kwa jina lake li", naona imekaa sivyo iwe "itaweza".

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nikija katika ukurasa wa 81 kifungu cha 33. Katika ufanuzi wa maneno, tuliona kule kuna neno "sehemu za graticular", hili neno limetolewa ufanuzi kule lakini unapotaka kutoa ufanuzi maana lile neno liwe limejitokeza humo ndani. Hilo neno halijajitokeza na kama kujitokeza lilikuwa lijitokeze katika kifungu hiki cha 33, halafu na kule ndio tutolewe ufanuzi wa neno sehemu za *graticular*.

Mhe. Mwenyekiti, ninaheshimu sana muda wako, nije sasa katika ukurasa wa 87, kifungu cha 57 mstari wa pili, kuongezwa kwa muda, ilikuwa iwe ni "muda wa ziada" na "sio muda za ziada". Nikija katika ukurasa wa 104 kwenye wajibu wa usambazaji kifungu cha 89, Mkandarasi na Kampuni, hapa imesema "itakuwa na wajibu", hivi ni vyombo viwili tofauti baina ya Mkandarasi na Kampuni, kwa hivyo, ningependekeza kwamba "isiwe itakuwa na wajibu" lakini iwe "watakuwa na wajibu" kwa ni vyombo viwili tofauti na sio chombo kimoja.

Nikija katika ukurasa wa 106 hapa ningependa kujua tofauti katika kifungu cha 94, tofauti kati ya kuziba kisima na kufunga kisima katika mukhtadha wa kitaalam wa suala zima la uchimbaji wa mafuta, neno "kuziba" ni nini na neno "kufunga" ni nini. Lakini nikija ukurasa wa 107, kuna vifungu ambavyo vimo katika kifungu cha 96(3)(b) na (c) haya maneno yaani hisa za mtaji na hisa za upendeleo, vipengele hivi hapa vimetolewa ufanuzi. Nilikuwa nashauri tu kama inawezekana vipengele hivi vipelekwe katika Sehemu ya Kwanza ya ufanuzi kuliko kubaki katika eneo hili kama ni ufanuzi.

Nikija katika ukurasa wa 109 katika kifungu cha 99(1) na (2), ningependa sana hapa hili neno "mkaazi" na "mkaazi halali", neno "mkaazi halali", ni neno ambalo limezungumziwa sana ningependa litolewe ufanuzi kwa sababu linaweza likaja likaleta utata huko mbele juu ya mkaazi halali kwa mujibu wa mswada huu. Lakini je, katika sehemu ya mwisho hapa inasema, "Sheria ya Usimamizi ya Ardhi" katika kifungu hicho cha kwanza, hii sheria ni namba

ngapi na ya mwaka gani, hivi vitu lazima vikae sawa kwa sababu sheria zinabadilika. Kuna sheria mwaka fulani na sheria mwaka fulani hatuwezi tu kuiacha hii ikawa iko *open* kama inavyoonekana.

Lakini katika kifungu cha pili hapa inaposema mstari wa mwisho hapo Mahkama ya Ardhi, Mahkama ya Ardhi ya wapi wakati hakuna ufanuzi, iseme kwamba Mahkama ya Ardhi ya Zanzibar au ya Tanzania, iweze kuweka ufanuzi huo ili kuweza na sisi kukaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee katika ukurasa wa 110, kifungu cha 102(a), iwe "kodi ya" na isiwe "kodi la" Mheshimiwa, naheshimi sana muda wako.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo ambao ninafikiri utasaidia Serikali ningiomba sana Serikali katika suala hili kuepuka suala la shindikizo la kisiasa, kuepuka *corruption*, lakini vile vile kuepuka ajenda za siri na maslahi binafsi tunapoingiana mikataba katika leseni na mambo mengine yanayohusiana na hayo kwa sababu nchi za kiafrika zinapoteza karibu dola bilionti hamsini kila mwaka zinazohamishwa kutoka Afrika kwenda nchi za ng'ambo na haya yanatokana na mikataba mibovu.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana.(*Makofî*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsanteni Waheshimiwa kwa michango yenu lakini niwashukuru kwa utulivu wenu katika kuongoza hili Baraza. Lakini chengine nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, Wajumbe wote tunatakiwa kwenye Kikao chetu cha *caucus* cha Kamati ya Chama cha Baraza la Wawakilishi, baada ya kuahirisha kikao hiki tunatakiwa tuwepo katika ule ukumbi wa juu kupata maelekezo ya huko.

(*Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilitrudia*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

*Mhe. Shehe Hamad Mattar (Mwenyekiti ) alikalia kitî*

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kunipa nafasi hii, lakini pia nichukue nafasi yangu kwa kuwapa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla pamoja na Rais wetu wa Zanzibar kwa kupotezewa na Rais wetu mstaifu Mhe. Alhaj Aboud

Jumbe Mwinyi, *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu amrehemu ailaze roho yake mahali pema peponi, *amin*.

Pia, nichukue fursa hii kuwapa pole Watanzania wenzangu kwa yale maafa ya Kagera juu ya tetemeko na nimshukuru Mhe. Spika, kutuwakilisha sisi sote kuungana na Watanzania wenzetu.

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu walionileta hapa kwa kura zao ili niweze kutoa mawazo yao na ushiriki wao na kuwa sauti yao.

Pia, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa maelezo mazuri aliyyoatoa mapema leo asubuhi. Vile vile, nimshukuru Mkurugenzi mstaafu bwana Yona Killagane kwa kuja kuungana na sisi kutoa mawazo yake na kutusaidia katika mambo yote kwa jumla ili kuitisha mswada wetu huu wa Sheria ya mafuta na gesi.

Mhe. Mwenyekiti, leo ni katika siku moja muhimu sana kwetu katika historia yetu ya Zanzibar, nasema hivyo kwa sababu mnamo mwaka 2009 kama ndugu zangu wajumbe mtakumbuka waziri mwenye dhamana, mwenye wizara hii hii alitamka katika chombo hiki, naomba ninukuu yale maneno yake.

“Ni hulka ya mwanadamu anapokosa hoja usishangae kwani atatukana na anaweza kutupa mawe sasa na ndio hao wabunge wamekosa hoja anapojuu amewatendea wenzake dhambi na wizi wa mchana,” alisisitiza huyo waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nimeipata hii kwenye mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa kuna maneno mengi sana juu ya masuala ya mafuta na gesi, serikali zote mbili zimefanya mazungumzo zimekuwa zinajadiliana katika mambo tofauti. Lakini leo tunashuhudia hapa katika chombo hiki cha wananchi, waziri mwenye dhamana wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mama yetu, rafiki yangu, dada yangu Mhe. Salama Aboud Talib, leo anaweza historia na kufuta kauli chafu ya potofu, ya matusi na kuweka historia mpya kwa kuleta mswada huu wa Sheria ya mafuta na gesi, kuomba ridhaa kwa wawakilishi ambao sisi hapa tupo ili serikali yetu iweze kuendelea na hatua za kisheria kwa kuchimba mafuta na gesi.

Kwa hiyo, niseme kwamba kwa hili nampongeza sana Rais Mstaafu Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyezi Mungu amjaalie apumzike vizuri akiwa yuko shambani, akiwa anapata muda wa kusafiri basi aendelee na shughuli

zake tumuhakikishie sisi kama wawakilishi na Wazanzibari wote tunamthamini, tunampenda na tutaendelea kumkumbuka.

Lakini pia nimpongeze Rais Mhe. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja hapa na akatamka pale kwenye viwanja vyta demokrasia Kibanda Maiti, akasema kwamba anataka mafuta yachimbwe wakati wowote. Kwa hiyo, nasema hivi, kwa nini? Wale wote wanaotia chokochoko, wanaotumia neno la "mafuta na gesi" kujaribu kutugawa, kubeza Muungano wetu, kutuletea maneno ambayo yaliyokuwa sio sahihi kabisa, basi hao leo hawana nafasi ndani ya Jamhuri, wende zao tena hao tunaweza tukawaita watu ambao waliokuwa hawana akili timamu. Huu Muungano wetu ni Muungano wa kihistoria Joseph aliyekuwepo kwa Tanzania Bara kama Kagera, Misenyi kama yupo huko Simiyu, yupo Dar-es-Salam Manzese na Mzanzibari aliyekuwa Machomane au aliyekuwa Paje, Chwaka au jimboni kwangu Tunguu wote sisi ni wa moja ni Watanzania na kamwe mafuta na gesi hayawezi kutugawa sisi, tutabakia kama Tanzania na tutaendelea kupendana.

Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii kuwashakikishia Watanzania na Wazanzibari wote kwamba sisi wawakilishi na serikali yetu ipo, tutaendelea kuwashawishi na kuwashauri ili kazi hii ya uchimbaji wa mafuta na gesi iendelee vizuri na Mhe. Waziri, uzipokee na hizi salamu pamoja na Makamu wa Pili sisi kama Baraza la Wawakilishi tuko nyuma yenu kuwasaidia. Pale ambapo patatokea mapungufu yoyote msione tabu kurudi na sheria yenu mkaja hapa tukaipiga msasa na kuirekebisha ili mkaendelea kuchapa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kuchangia mswada wetu huu ulioletwa hapa ambao umetokana pia na sheria mbali mbali. Niseme kwanza tunaishukuru Jamhuri kwa kuitishsha sheria ya 2015 ambao ni *Petroleum Act, 2015*. Sheria hii ya mafuta ya 2015 kwenye kifungu cha 2(2), kinaitambua kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendesha shughuli zake za utafutaji na uzalisha wa mafuta na gesi kwa kutumia rasilimali yake wenywewe, na hii ndio tuko hapa kwa pamoja. Nataka nisema katika suala zima la mafuta na gesi kuna misingi ambayo itahitajika tuiweke vizuri katika kuwavutia wawekezaji. Uhuru wa kuuza, kutokubadilika kwa sheria za kodi na mikataba, nguvu ya utekelezaji wa mikataba, ushindani uliopo na wenyewe haki na sawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, ukiangalia kwa upande wa wenzetu wa Jamhuri wana sheria kwao ambayo pia inasema ile ya *Transparency and Accountability Act, 2005* mwezi wa 6. Hii itaifanya makampuni kutoa taarifa ya malipo na serikali bila ya kutoa taarifa ya walichopokea. Uainishaji huu umefanyika na

*independent party.* Mimi naamini Mhe. Waziri, hili ni katika jambo muhimu utapoliweka kisheria. Lakini katika suala zima la mapato, haya mapato ya mafuta na gesi hubadilika sana na hutegemea hali ya kisiasa na uchumi duniani. Nchi yetu nashauri isitegemee mapato ya rasilimali kwenye mipango yake ya matumizi ya kawaida, twende nacho. Wananchi wetu huko wanawaza wao kwamba tutapoanza kuchimba mafuta na gesi sheria ikipita, basi kesho mafuta na gesi yatatoka. Kuna umuhimu wa kuelimisha kwamba haya yote yatachukua muda ni hatua baada ya hatua, lakini mambo yote haya yende yakae kwa uwazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ambayo nimeangalia yanataka kuangaliwa zaidi kisheria nitakwenda kwa haraka na nitashauri Mhe. Waziri, aangalie kwenye *Hansard* kutokana na muda. Kwenye ukurasa wa 12(d), Jukumu la Waziri wa Fedha, ukurasa wa 13 na 14, *Cost ya oil na gas and upon laws*, jukumu la kampuni na *contractor* isiwe kampuni pekee. Ukurasa wa 22 *departmental health* wawajibike kwa Mkurugenzi Mtendaji na sio bodi. Kwenye *paragraph* ya 29(1), *In accordance with accepted accounting principles*, hapo naona ingesoma *in accordance to the laws of Revolutionary Government of Zanzibar*. Kwenye *paragraph* 29(3), nashauri ingesoma kwamba; *the statement of accounts shall include those stipulated by the laws of Revolutionary Government of Zanzibar*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo ambalo nimeliona ni taarifa ya bodi ya kila mwaka, kwenye *paragraph* 30(2), nataka hesabu ziwasilishwe kwa CAG miezi mitatu baada ya mwaka kwisha. *Paragraph* ya 31(1), inaitaka Bodi ya Wakurugenzi kuwasilisha taarifa ya mwaka *annual report* katika kipindi cha miezi minne baada ya mwaka kwisha. Ina maana kuwa CAG ana muda chini ya mwezi mmoja kukamilisha ukaguzi na hili halitowezekana, kwa kawaida CAG huhitajika kutoa taarifa yake ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea hizo hesabu. Muda muafaka wa bodi kupeleka taarifa yao inatakiwa kuwa miezi saba baada ya mwaka kwisha.

Mhe. Mwenyekiti, pia, ukiangalia katika eneo la kuonesha utafiti wa mafuta kwenye *paragraph* 34, Jukumu la kubaini maeneo haya mapya yakufanya utafiti iwe mamlaka baada ya kibali cha Waziri wa Mafuta na utaratibu uwe shirikishi kwa ngazi za mamlaka na waziri wakati wa kutoa kibali ahusishe mawaziri wenzake. Waziri akihusika kubuni uteuzi wa maeneo ya utafiti anaweza kudumaza kasi ya utafiti nchini kwa pamoja. Kwenye *paragraph* 9, yafuatayo yaongezwe mwishoni "*upon recommendation of the authority*".

Kwenye ushirika wa kampuni ukurasa wa 30, kwenye *paragraph* 45(5), aya inayosomeka kuwa ushirika wa kampuni usizidi asilimia 25, naona hapa pana kosa ilikusudiwa 25 kwenye ya Kiingereza ni 45. Rasilimali hii ya wananchi, hivyo, wao ndio watakoakuwa wananaufaika, kampuni ni mali ya serikali, hivyo, wakishiriki kwa sehemu kubwa maana yake rasilimali itabakia nchini kwa manufaa ya wananchi wote. Mhe. Mwenyekiti, ushiriki wa kampuni usipungue kwa idadi ambayo itakayopangwa.

Sasa nataka nichangie kwenye suala hili ambalo la ZPDC. Kwenye *paragraph* 45(4), 46 na 47 ni muhimu kila ombi la kushirikiana na kampuni lihusishe angalau kampuni mbili au tatu au zaidi. Hawa ndio watakuwa wakandarasi na watamteua mmoja kuwa mtendaji wao ambaye atakuwa kama ni *operator* kwenye mfumo wa namna hii udanganyifu mwangi utapungua, na hili linaangalia zaidi kwenye masuala ya *consortium*. Ukipishiriki kwa upande wa *consortium* pia unakuwa na mafanikio na mazuri kwa kushirikiana kitaaluma, kifedha na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika masuala ya uwezo wa mamlaka ya waziri pamoa na mamlaka ya kutaka kupata taarifa kwenye *paragraph* 32, baada ya zabuni sheria hajatoa uwezo kwa waziri au mamlaka kuomba taarifa zaidi ya waombaji vitalu kama zinahitajika kwenye uamuvi wa zabuni au kufanya uchunguzi wa kina. Taarifa hizi nashauri ni muhimu kampuni zinazoomba vitalu ni muhimu vifanyiwe upukuzi wa kutosha kuhusu uwezo wao na sio kutegemea taarifa zinazowasilishwa kwenye zabuni pekee. Aya hii ipo katika Sheria ya petroli ya SMT kifungu 49.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ukubwa wa vitalu, sheria lazima ioneshe nashauri ukubwa wa vitalu ambazo ni *blocks*. Vitalu visiwe vikubwa na hasa ambavyo kama sasa hivi wastani wa mita za mraba 10,000, nafikiria tayari kwenye marekebisho yameoneshwaa kwenye sheria kwa kamati, lakini wastani inatakiwa isizidi mita za mrahaba 3000, najua Kenya na Uganda wamefanya hii, kampuni nyangi zinakuja kufanya utafiti na hivyo, kuongeza upatikanaji wa rasilimali. Umbo la vitalu ni muhimu kwa waendeshaji na utafutaji wa siku za usoni.

Mhe. Mwenyekiti, gharama katika eneo lilorudishwa. Kwenye *paragraph* 58(3), sehemu hiyo inasema kuwa serikali haitahusika na gharama zilizoingiwa kwa sehemu ambayo imerudishwa, kwa tafsiri hii ni sahihi na ndio nia ya kifungu hicho, adhma hii itawakatisha tamaa wawekezaji. Aidha, itakuwa pia vigumu kujua gharama zilizotumika kwenye sehemu ambayo pekee ndio inayorudishwa serikalini. Nia ya kurudisha eneo ni kuhakikisha kuwa

mwekezaji analifanya kazi lote na serikali inapata faida ya *data* zilizokusanywa kwa tafiti kwa ajili ya baadae.

Lakini pia uongezaji wa muda wa leseni za utafutaji. Kwenye *paragraph* 59, kampuni yoyote itayogundua rasilimali katika kipindi cha tatu au cha miaka miwili ya mwisho itamlazimu ifanye utafiti ili ilete maombi yake ya kupatiwa leseni za uendelezaji. Kufuatana na kifungu 63(1), kampuni imepewa miaka miwili au mitatu kufanya utafiti huo. Muda huu wa ziada unaweza ukaanguka nje ya leseni ya utafutaji na hivyo, mwekezaji kutokuwa na leseni yoyote.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, una dakika mbili.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante naomba nisaidie kidogo. Mwekezaji hatoweza kukubali jambo hilo, sheria lazima iruhusu nyongeza hiyo jambo hili linaweza kutokea pia kwenye kipindi cha kwanza na cha pili cha utafutaji ikihusika eneo la kuachia.

Kwenye *paragraph* 62(1), muda uliotolewa kwenye kifungu hicho kukamilisha uchunguzi ulioanishwa kwenye *section* 62(2) ni mfupi kutokana sehemu gani ya ugunduzi utafanyika. Muda umebainishwa kuwa usizidi miaka miwili kwa utafiti wa mafuta na miaka mitatu kwa ajili ya gesi asilia. Kwenye bahari ya kina kirefu muda huo utalazimika kuongezeka, kifungu hakitoi ruhusa hiyo kwa mamlaka kuongeza muda huo kwa kampuni kufanya utafiti huo. Kwenye Sheria ya petroli ya SMT *paragraph* 65(1) na pia kwenye kifungu 66(1) inatoa ruhusa hiyo.

Kwenye uendelezaji eneo lisilokuwa la leseni la utafutaji kwenye kifungu 42 cha leseni ya uendelezaji kwenye maeneo ambayo mkandarasi hufanya utafiti na kubaini kuwa hawesi kuendeleza ugunduzi huo kwa sababu yoyote ile anatakiwa kurudisha eneo hilo serikalini ikitokea mwengine ana leseni ya utafutaji akagundua hatimae kuombewa leseni ya uendelezaji inawezekana kabisa ikawa jambo zuri, uendelezaji ule ufanyike na kwa ugunduzi wa eneo lilokuwa limeachiwa kwa sababu ya kiuchumi na kiufundi na ukiangalia katika Sheria ya SMT kwenye *section* 66(3) hiyo ipo.

Nia ya kumnyima leseni ya uendelezaji. Ukiangalia kwenye *paragraph* 65(2), waziri haruhusiwi kumnyima leseni hadi awe ametoa *notice* kwa muombaji. Hivyo basi, muombaji anatakiwa apewe muda wa kujieleza na kumpa muda wa kurekebisha sababu za kumnyima leseni, akishindwa kujitetea au kurekebisha makosa ndipo leseni isitolewe, bila ya kuwa na haki ya kujitetea na kurekebisha

makosa ikawakatisha tamaa wawekezaji, sheria hii ipo katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano Nam. 69(2)(b), maelekezo ya mamlaka ya jinsi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda wako umemaliza.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Naomba nimalizie dakika mbili...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda umemaliza, usile muda wa mwenzako.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, baada ya nafasi hiyo uliyonipa nakushukuru sana na maeneo yaliyobakia nitampelekea Mhe. Waziri, na nimpongeze sana hoja hii naunga mkono asilimia 98, mitaomba maelezo hayo niliyoyazungumza na mengine ya maandishi kumpelekea waziri ili atapokuja aweze kuniambia, lakini nimefurahi sana naipongeza serikali, naipongeza *cabinet*. Mwenyezi Mungu ajaalie salama aibariki nchi yetu. Ahsante. (*Makofî*)

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata):** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu kuelezea mswada huu wa Sheria ya usimamizi, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hususan tukiangalia katika maisha yake yote anahangaika kutafuta kila mbinu na anajaribu kusimamia vyema pato la nchi yetu kwa kadri muda unavyokwenda. Lakini pili Mheshimiwa, nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake, niseme tu kwamba nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa juhudzi zake ambapo kwa muda mfupi huu tuliokuwa naye tumeona machachari yake pale unapomfikia kumuendea kumueleza jambo lolote, yupo tayari papo kwa papo kutoka kwenda kulifatilia na kulitatu.

Huo ni muono mzuri na ni utendaji ambao tunautaka, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, unapopewa taarifa basi fatilia taarifa, ukisema nitasikiliza basi utaharibikiwa. Kwa hiyo, nampongeza kwa moyo wangu wote Mhe. Waziri, kwa hilo kwa juhudzi yake hiyo na ndio nikasema kwamba ninaamini Mhe. Mwenyekiti, mswada huu Mwenyezi Mungu atatujaalia utapita na ukipita najua Mhe. Waziri, kwa usimamizi wake mzuri na kwa washauri mbali mbali ambao watampa maelekezo mema basi tutafanikiwa tunakokwenda na tutafika. Kwa hivyo, pongezi zangu hizo azichukue na niko sambamba na yeye au tuko

sambamba na ye ye katika kumsaidia kila panapohitajika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, sina pingamizi nao, lakini nitatoa rai na maelekezo ya hapa na pale kwa hatma huko mbele tunakokwenda kwa usalama wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kitu kibaya katika dunia hii tuliyokuwa nayo ni kipato, ukiwa na kipato wewe utakuwa na maadui wengi katika upande wako, na ukiwa huna kipato hata mtu hakuulizi. Kwa hivyo, suala la mafuta ni pato la nchi yetu. Mwenyezi Mungu akitujaalia ni nchi ambayo itatizamwa kwa hali mbaya na maadui zetu, lakini kubwa ni wanasiasa pamoja na sisi, kwa sababu ni wanasiasa wa pande zote. Mwanasiasa maana yake ni mwanasiasa tu, kubwa atalolitaka ye ye pengine penye mafanikio atataka kuchochea ili mafanikio yale yasipatikane. Mimi ombi langu naiomba sana serikali au wizara hili lizingatiwe kwa usalama wa maeneo yetu katika kuhakikisha kwamba ufanisi na usalama unapatikana juu ya hatma ya neema hii Mwenyezi Mungu aliyotujaalia kwa manufaa ya nchi yetu na watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kulisema ni vyema wananchi wetu wakapewa taaluma kubwa sana, jambo hili ni kubwa sana na tunashuhudia katika nchi za wenzetu kama walivyosema baadhi ya wenzangu, mafuta na gesi ni rasilimali kubwa sana katika maisha ya nchi au kwa maendeleo ya nchi. Lakini kama hakuna maelezo ya watu wetu kuwaelimisha basi itakuwa ni hatari tunakokwenda. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri, awe na kitengo maalum cha kusimamia usalama na kuwaelimisha wananchi wetu siku hadi siku kadri ya mwanzo utakavyoanza na huko mbele tutakofikia, adhma yetu moja, mbili, tatu kwa faida ya nchi yetu. Elimu ni jambo zuri na wananchi wakielewa kinachofanyika watajielewa kwa faida ya nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili tumelishuhudia kwa wenzetu Tanzania Bara kwenye mradi mkubwa wa gesi asilia. Wenzetu wamepiga hatua kubwa, lakini naamini walianza mapema kwa sababu walikuwa wameshajitayarisha. Nije kwenye ajira, hili suala lina ajira katika sehemu mbali mbali, namuomba sana Mhe. Waziri, kupitia Baraza hili vijana wetu wengi wako mitaani na vijana wetu wana uwezo wa kuajiriwa na kujajiri katika sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba suala hili aliangalie kwa upeo wa mbali vijana wetu inapotokea neema wafaidike wao mwanzo kuliko wengine.

Pamoja na kupata ajira kwa vijana wetu hao uzalendo tuuveke mbele, tusikubali hata siku moja kuchezea rasilimali hii na tukafanya masihara yeoyote

apewe tu. Mtu achunguzwe, aangaliwe uwezo wake na vitendo vyake kujua kwamba je, hapa anapowekwa anastahiki kuwepo kwa manufaa ya nchi yetu? Namuomba Mhe. Waziri, upembuzi yakinifu lazima uwepo kwa walengwa ambao watateuliwa katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili linakuwa na migogoro sana, Mwenyeyezi Mungu atuondolee yasitokee katika maeneo yetu, lakini jambo hilo mara nyingi huwa haliepukiki. Kwa hivyo, kitengo cha kutatua migogoro kiwepo kizuri, wawepo watu mashuhuri wazuri wanaoweza kupatanisha mawili, matatu ili kuweka mwelekeo mzuri katika kuondoa matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Migogoro inatokana na biashara na wafanyabiashara wengi ndio wanaosababisha migogoro, inaweza kuja kampuni fulani mimi nasema nitafanya hivi, akatokea mwengine kupitia mbinu yake anayojua ye ye akageuza hivi kutaka kuleta ufitina ili jambo hilo lisifanikiwe. Nimuombe Mhe. Waziri, makampuni yatakayokuja hapa kwetu tunayahitaji, lakini tuyasome, tuyajue au tujue wanakotokea, walipo na wanakokwenda, kwa sababu wengine hawana mwelekeo mwema wamo katika mahitaji yao kwa kupata faida wao kuliko serikali. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, hili aliangalie na litupe faida katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, uchumi ni siasa na pato lolote la taifa ni siasa. Kwa hivyo, narudia tena ni lazima tukae tutafakari siasa, lazima iwemo katika kuelekeza, kwa sababu bila ya kuelekezwa jambo hilo hatwendi. Nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba, atumie wakala na wabunifu ambao wana uzoefu katika mambo haya ili kusaidia katika kukuza hili suala letu liende vizuri huko mbele tunakokwenda. Sisemi siasa ya vyama hapa, nasema utaratibu katika jambo hili lazima uwepo mzuri na utaratibu ukipangwa vizuri tutafanikiwa mara moja tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hii ni nyota ya jaha, tuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wetu wa Awamu ya Nne Mhe. Jakara Mrisho Kikwete kwa kulia linalofanya kwa maslahi ya Wazanzibari. Lakini pia Mhe. John Joseph Pombe Magufu, alipokuja kwenye kampeni yake na akarudi tena kauli yake mbiu ni ile ile kwamba atasaida Zanzibar kwa uwezo wake wote kwa kila linalostahiki katika maisha yake. Kwa hivyo, niseme kuwa hili ni suala zuri na litatufaa katika maisha yetu.

Jengine ninalotaka kulisema ni kwamba, muda huu tuharakishe sana na muda huu sio wa kungojea kwa sababu wakati haumngojei mtu ni vyema tukaharakisha suala hili likapita haraka na naamini kwa uwezo wake aliopewa

Mhe. Rais, tukimaliza vyema sisi na ye ye yuko njiani atatungojea. Hivyo, tuombane Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuchangie, tuelekezane, lakini neema kubwa hii tunapata Wazanzibari wote na hakuna hata mmoja atayeikosa kwa njia moja au nyengine.

Kwa sababu likipatikana pato tutajenga barabara Jimbo la Kijitoupele, tutapeleka umeme, tutapeleka michirizi ya maji niliyomwambia Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maaum za SMZ. Nataka kutengeneza michirizi yangu ya Daraja la Kwa Shunda, Meli Nne na Daraja la Meli Nne, Uzi, pesa zitatoka hapa. Kwa hivyo, huu ni wakati wa kuharakisha kwamba tukae na kusimamia ili litekelezeke haraka faida hiyo tuipate.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kuwa nimetanguliza kauli yangu ya mwanzo, lakini natamka la mwisho kwamba, mimi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele wanayoitakia maendeleo nchi hii tunaunga mkono mswada huu kwa asilmia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofî*)

**Mhe. Ussi Yahya Haji:** Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, awali ya yote ni wajibu wangu kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa uamuza wao wa kulipwekesha suala la mafuta likawa liko Zanzibar. Leo hii katika Mkutano wetu huu wa Tatu, Kikao cha Nne cha tarehe 26/9/2016 tunazungumzia suala la mafuta, uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu naomba kufanya marekebisho madogo katika kurasa zifuatazo:

Kwanza katika ukurasa wa 66, katika sheria hii wanasema kwamba, Sheria inayohusiana na uchimbaji, utafutaji na gesi na mafuta. Mswada huu kisheria ungeliitwa hivi: "Mswada wa Sheria ya Utafutaji, Uchimbaji Mafuta na Gesi", hii 'na' moja hapa itabidi itoke.

Ukurasa wa 67 *paragraph* ya 9, kuna maelezo hapa ningeliomba Mhe. Waziri, atakapokuja kuzungumza anihakikishie tu, kuna maneno yanazungumza kwamba: "kutokana na msukumo wa hewa na kiwango cha nyazi joto 60 (*Fahrenheit*). Je, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ya dunia kiwango hiki ambacho kinatarajiwu kuwepo leo kitaendelea kuwa hiki hiki au kutatokea mabadiliko? Mabadiliko ya hewa yako juu ya ardhi. Je, chini ya ardhi mabadiliko haya ya hewa hayatobadilika? Hilo lilikuwa la kwanza.

La pili, ukurasa wa 78/79 kuna maneno hapa katika kifungu cha 23(b). Michango, ruzuku, wasia au mikopo iliyopatikana..." Huu wasia hapa unakujaje na maana yake nini wasia huu.

Halafu katika kifungu cha 25(b), kifungu hiki kinasema: "Kwa niaba ya mamlaka fedha hizo zinahifadhiwa benki".

Ningeliomba ikaingizwa Benki ya Watu wa Zanzibar lisiachwe neno 'benki' tu. Katika ukurasa wa 91, 92, kifungu cha 63(1), *paragraph* (i)(ii) kinasema; "kima cha maji kama kipo", hakuna kima cha maji, kuna 'kina cha maji kama kipo'.

Ukurasa wa 131, kuna taarifa kifungu cha 11(1)(b) kwamba: "Iwapo bila sababu ya msingi ameshindwa kuhudhuria vikao hivyo mfululizo...", mfululizo iongezwe bila ya taarifa, asije akaadhibiwa kwamba hakuhudhuria lakini kuna taarifa.

Mwisho katika kusawazisha haya katika mirahaba. Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa mirahaba katika kifungu cha 2, jadweli la II, kuna eneo la nchi kavu na eneo la baharini. Je, viwango hivi vyta mirahaba vilivyoainishwa hapa vimekisiwa vipi? Kitaifa, kimataifa au kimekisiwa kwa misingi gani hata ikapatikana mirahaba hii asilimia hizi zilizowekwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nichangie machache sana. Suala la gesi na mafuta katika nchi yetu ni historia na historia hii kwa bahati nzuri serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imeleta Mswada huu ambao ukipitishwa na nina hakika utapitishwa, una faida kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba. Sasa basi, kuna haja moja kubwa sana, kwanza wizara kuhakikisha inatoa taaluma ya kutosha kabisa kwa wananchi wa Unguja na Pemba ili kulielewa hili suala. Kwa sababu wasije wakafikiria kwamba, ukishapita tu mswada huu mafuta yatachimbwa kesho au keshokutwa, kwa hivyo, lazima tutoe taaluma itakayotosheleza kabisa. Hilo la kwanza.

La pili, bila shaka mswada huu tutahitaji wafanyakazi watakaofanya kazi katika mamlaka na watakaofanya kazi katika kampuni, lakini mimi nazungumzia zaidi katika mamlaka na kampuni yenye. Ni lazima serikali sasa hivi isimame kidete ielimishe wananchi wa Zanzibar wawe na taaluma ili kuelpuka kuja kukodi watu au kupata watu ambao hawana uzalendo na nchi hii. Tukipata watu ambao hawana uzalendo ni hatari kubwa sana kwa taasisi hii. Kwa hivyo basi, kuna haja Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya wizara hii ikaangalia vizuri sana nani na nani wanapewa taaluma kwa kuja kufanya kazi

hii, isijekuwa tutasomesha vijana wetu wakapata taaluma na dunia hii kuna utandawazi wanaweza wakapata taaluma halafu wakaja wakaibiwa njoo huku, njoo huku, kuna marupurupu haya. Kwa hivyo, wale ambao watakuwa wanafanya kazi hii mikataba ambayo watakaotiliana na serikali mikataba hiyo ije ilinde maslahi ya serikali na ilinde maslahi yao. Hilo ni jambo la msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunazo taarifa kwamba kuna vijana wetu wameshapelekwa nchi za nje kusomea mambo ya mafuta, nafurahi sana kuwa suala hilo lipo. Lakini je, tumeambiwa hapa katika sehemu mbali mbali kuna vijana wamekwenda kusomea mafuta, lakini kuna wengine wamekwenda kwa fedha zao, wengine wamepata wafadhili na wengine wamepelekwa na serikali. Sina mashaka na waliopelekwa na serikali kama wamepelekwa nina hakika ni wazalendo wa nchi hii. Lakini kuna wale ambao ni Wazanzibari wenzetu ambao wana haki kabisa ya kufanya kazi hii tunayoizungumzia hapa. Je, serikali wamewafanya *vetting* na ni wazalendo?

Kwa sababu dunia ya leo ina matatizo, inawezekana mimi nikenda kusoma nchi za nje nikasomesha na taasisi yangu nikafanyiwa na kila kitu, lakini narudi kuja kufanya kazi hapa ikawa nafanya kazi nikiwa na lengo la *double standard*, nitakuwa nafanya kazi katika Zanzibar lakini pia nawafanya kazi watu wengine. Kwa hivyo, wale ambao wataajiriwa katika taasisi hii ya mafuta ni watu ambao serikali iwachunguze na iwjue, wawe wazalendo. Hatuna ubaguzi ikiwa atakuwa Mswahili, Mwarabu, Muhindi, madhali Mzanzibari ana haki ya kufanya kazi, lakini huyo ye yeyote atakayefanya kazi katika taasisi hii ni lazima achujwe na ajulikane ana uchungu wa nchi hii, kama uchungu waliokuwanao Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuipitisha sheria hii, sio tuje tupate makapi.

Mhe. Mwenyekiti, mfano huu umetokea hapa Zanzibar mwaka 1965 ilikusudiwa kufunguliwa Benki ya Watu wa Zanzibar, walifutwa vijana maalum na naomba kama hao waliopelekwa hawatoshi kuanzia sasa serikali itafute vijana maalum wenye taaluma wanaoweza kwenda kusoma masuala ya mafuta na gesi, ili hapo mbele baadae tupate vijana wetu wataalamu.

Mwaka 1965 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipotaka kufungua Benki ya Watu wa Zanzibar ilipeleka vijana wake maalum Ujeruman, wakapelekwa Pakistani na China, waliporudi wakafungua benki na ilivyokuwa wamepelekwa wale walichujwa na wanajulikana wazalendo na wanaumwa na nchi yao, mpaka leo benki ile inaendelea na ipo na ni moja katika taasisi za serikali zilizopata faida kubwa na inayoendelea mpaka sasa hivi. Kwa hivyo, na vijana

hao watakaopelekwa na serikali lazima wajulikane nani na nani, sio mtu ana pesa zake anasoma tu huko nikafanye kazi ya mafuta Zanzibar, kama hamumjui badala ya hisani, itakuja kuwa lukusani.

Jengine kuhusu taaluma, Taasisi hii tutahitaji tuwe na waandishi wa bahari wa taasisi wanahusika na mafuta tu. Naishauri serikali kuanzia sasa ifundishe wananchi wa Zanzibar taaluma ya habari inayohusiana na habari ili wapate taalamu wawe waandishi wa habari wa Mafuta na Gesi tu, ili wabobee katika taaluma hiyo.

Jengine la mwisho, naiomba serikali mswada huu ukishapita ijaribu kuulinda mswada huu, kuukubali mswada huu na sisi hapa tutaupitisha mswada huu lakini ulindwe kwa ulinzi na usalama wa taifa kwa mswada ni jambo muhimu sana. Wale wote ambao watafanyakazi katika taasisi hii serikali iwatambue na iwafanyie *vetting*.

Mwisho, sina zaidi ya hayo isipokuwa naunga mkono mia kwa mia suala hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kuwa pamoja hapa katika Baraza lako tukufu.

Lakini pia nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizi kwa jitihada yake kubwa kwa kuleta Mswada huu wa sheria yaa uchimbaji wa mafuta.

Nimpongeze sana Mhe. Waziri, dada yangu Salama Aboud Talib kwa juhud zake kubwa na kwa bahati yake nzuri kwa kuingia katika Baraza hili tukufu na sera imekuja ya mafuta ikapata neema kubwa kwa siku nyingi tulikuwa tunaisubiri.

Mhe. Katibu Mkuu wa Wizara hii Mhe. Ali Khalil Mirza nimpongeze sana kwa kweli juhud zake kubwa tangu miaka ya nyuma, nakumbuka Baraza lililopita alikuwa anajitahidi sana na ana nia njema na nchi hii kuhakikisha mafuta haya yanachimbwa na tunafaidika sote.

Pia, niipongeze wizara na watendani wao wote kwa juhud zao kubwa. Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa juhud zake kubwa sana na kwa ripoti ya kamati nzuri imeleeza mambo mengi sana mazuri kwa uwazi kabisa. Pia,

niwapongeze wajumbe wote wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kazi yao nzuri walioifanya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niingie kidogo kwenye mswada huu wa uchimbani wa Mafuta na Gesi. Lakini mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, mswada huu mimi sina mashaka nao kwa asilimia mia kwa mia, mswada mzuri umetuelekeza mambo mengi sana mazuri na sheria ambazo nimeziangalia ndani ya mswada huu hauna tatizo kabisa na naamini tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Lakini pia nilipongeze sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa marekebisho ya Katiba kuliondoa suala la Mafuta na Gesi katika Katiba inayopendekezwa. Kazi kubwa na Mhe. Mwenyekiti, kama unakumbuka mimi nilikuwa ni Mjumbe wa Bunge Maalum la Katiba lilofanya kipindi cha mwaka 2013/14. Ilikuwa kazi kubwa sana suala hili la Mafuta na Gesi kuiweka tafauti katika Tanzania Bara na Zanzibar. Lakini kazi ilikuwa sio ndogo, ni kazi kubwa sana, lakini wenzetu kwa nia njema wakaona hili suala tulitoe tuliweke tafauti ili waweze Wanzanzibari kufaidika na mafuta yao haya. Kwa hiyo, mimi nalishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Bunge la Katiba kufanikisha suala hili.

Pia, niwapongeze sana ndugu zetu hawa wa *TRA* kutoka Tanzania Bara na sisi, tuwapongeze sana. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wananchi wengi wanapotoshana hapa wanasema *TRA* kodi ikukusanya hapa inachukuwa Tanzania Bara, ni kitu cha uongo nimefanya utafiti mkubwa, nimeangalia kodi yote ya *TRA* inayokusanya hapa Zanzibar inabaki kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatusaidia sisi wananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo, mimi niwapongeze sana ndugu zetu juu ya changamoto nydingi, lakini pesa zinazokusanya hapa zinaendelea kubaki hapa, ukiangalia katika mswada huu katika kifungu 6(2)(d), kinaleaza wazi kuhusu waziri atasimamia kodi hii. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana wenzetu wa *TRA* kwa kuiona hilo na kuweka tafauti juu ya mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niipongeze sana juhudhi pia za wizara kuona umuhimu wa kuwasomesha wataalamu wetu juu wa Mafuta na Gesi. Hii kazi imefanyika siku nydingi na bado inaendelea tangu hapo nyuma wameshaanza kusomeshwa vijana wetu ili kuwa wataalamu wa mafuta kwa ajili ya kuweza kuitambua mambao tafauti. Kwa hivyo, wizara inafanya juhudhi hii na nampongeza Katibu Mkuu wa wizara yake kwa kazi kubwa walijokuwa wanaifanya tangu hapo awali kwa shughuli hii ya uchimbaji wa mafuta.

Lakini nianze kuhusu wataalamu, Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu sehemu ya mswada huu kifungu 25 kuanzia kifungu cha 7 - 32 vinaeleza muundo mbali mbali kuhusu majukumu ya kampuni watakayopewa kuhusu kushughulikia masuala ya mafuta. Jukumu moja walilopewa makampuni na mswada huu au wizara yetu iliyoweka mswada huu au wizara yetu moja kwa moja kuwasomesha wataalamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza sana wizara kwa kuwasomesha wataalamu hawa ni fedha nyangi sana inatakiwa. Lakini watalamu hawa kwa nia njema na kwa nia njema wizara yetu hii ya ardhi imewe ka wataalamu kuwasomesha hawa ndugu zetu wa Kizanzibari waweze kuwa na utaalamu juu ya Mafuta na Gesi. Kwa hiyo, mimi napongeza sana suala hili na wengine ukitizama waliosoma wamesoma kwa mifuko yao, yaani fedha zao za ndani kabisa wamejitätahidi, lakini bado wataalamu tunao kidogo. Lakini kama wizara wataalamu imekubali wawekezaji kuwasomesha jambo jema na jambo zuri kabisa. Kwa hiyo, mimi nalipongeza sana suala hili na nampongeza waziri kwa kifungu hichi kuanzia kifungu namba 7 - 32 cha mswada huu kimeeleza wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme suala moja kidogo,, wenzetu Tanzania Bara tayari wanachimba Gesi na mimi mmoja nimewahi kufika Mtwara Songsongo nimewahi kufika, nimeona mafanikio makubwa wenzetu wanapata kwa ajili ya Gesi na ukitizama pale wataalamu karibu 17 wote Watanzania Bara wanafanyakazi pale, kwani hawataki wataalamu kutoka nje wapo Wachina baadhi tu wanawasaidia, lakini mambo yote wamekamata wenye wale Watanzania Bara kwa uzalendo waliokuwa nao na kazi wanaifanya kwa bidii kubwa na mkujitolea kwa ajili ya ule utaalamu huu wa Gesi kuchimba na ukitizama ni maisha yao ni hatari, kwa sababu kuna mitambo pale ukija kurupuka wale hawana maisha tena.

Lakini wanafanyakazi kwa juhudu kubwa, wanajitätahidi sana Gesi inapochimbwa inapohifadhiwa mpaka inakuwa Gesi salama kufika sehemu husika. Kwa hiyo, kazi wanaifanya mimi nawapongeza sana wataalamu hawa. Lakini na sisi tuwe na wataalamu wetu kutoka hapa hapa Zanzibar kama wizara ilivyokuwa imekubaliana na makampuni haya kuwasomesha ndugu zetu hawa. Lakini mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, mafanikio makubwa yatapatikana sana kwa mswada huu, ndio maana nikasema kwamba mswada huu mimi sina mashaka nao na naomba Wajumbe wote muupitishe kwa nia njema hauna mashaka yoyote wala kushindana. Kwa sababu mswada mzuri na una mafanikio kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mafuta haya na sheri hii ikishakupita itatoa fursa nydingi kwa ajira vijana wetu, vijana wetu sasa hivi hawana ajira, wengi wanazurura mitaani tu na wanaweza kufanya kazi hii ya Mafuta na Gesi katika sekta tafauti, kuna mambo mengi yatakuja kwa ajili ya ajira kwa ndugu zetu, karibu ajira ya watu elfu ishirini wataajiriwa kwenye sekta hii ya Mafuta na Gesi. Kwa hiyo, mimi naomba sana ipite haraka iwezekanavyo na serikali yetu ya hapa Zanzibar ifanye haraka kufanikisha suala hili.

Lakini mimi naomba sana wizara ijitahidi sana kutoa taaluma hasa kwenye *TV*, siaona hivi vipindi vyta Mafuta na Gesi ili kuwaelimisha wananchi wetu, bado wananchi wetu hawafahamu suala hili la Mafuta na Gesi kabisa, hawajui umuhimu, faida na uchumi wake, hawajui kitu bado.

Naomba sana wizara iwafahamishe taalamu wananchi wetu ili tuweze kushirikiana pamoja nao kuanzia serikali, Wawakilishi, Wabunge, hawa wafanyabiashara wakubwa wakubwa, wadau mbali mbali na hawa viongozi wa vyama vyta kisiasa pia washiriki suala hili, hili suala sio la mtu mmoja, hili suala la taifa zima. Leo mambo haya wakifanikiwa, tutafanikiwa sote, sifanikiwi mimi peke yangu ila tutafanikiwa sote. Kwa hiyo, mimi naomba tushirikiane sote kutoa taaluma kwa wananchi wetu, faida hii ikipatikana itapatikana kwa faida ya kizazi chetu cha leo na cha kesho pia.

Kwa hivyo, mimi naomba tushirikiane sote, kila mtu mwenye sehemu basi aweze kuwafahamisha wenzetu. Kwa sababu kama tunavyojuu Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi wamezungumza hapa hili suala lina fitina kubwa na kama tukifanya mchezo tutaanza kupigana wenye kwa wenye sasa kwa ajili ya Mafuta na Gesi. Mwenyezi Mungu keshatupa neema kama hii tuisiifanyie mchezo, kwenye pahala pazuri tuseme hapa pazuri na pabaya tuseme hapa pabaya, lakini tusianze kufitinisha haya mafuta yasichimbwe Mhe. Mwenyekiti, mimi huko siko nina nia njema kabisa na nchi hii, nataka wananchi wangu wafaidike ili tuweze kufika mbele kama nchi zilizoendelea. Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee na mswada huu, kifungu cha 6,(2)(9), kinasema;

"Waziri atahakikisha mafuta kupatikana ndani na usafirishaji mafuta nje ya nchi kuona wananchi wanafaidika na rasilimali hii".

Mimi nimesema Mhe. Mwenyekiti, kuwa mswada huu ni mzuri na waziri kakiri mwenye kwenye atahakikisha hapa mafuta yatapatikana ndani na nje ya kusafirisha ili kuuza. Lakini mimi niseme kuna changamoto nydingi, faida hii ikipatikana wenzetu wana changamoto nydingi hasa wananchi wetu masikini, wana mambo mengi ya kufanya. Lakini mambo hayaendi kutokana na fedha

zinakuwa tabu, rasilimali hii ikipatikana kwanza tutatizama afya, afya yetu sisi bado iko nyuma sana, shida nyingi, ukitizama skuli zetu bado shida, walimu bado hatuna wa kutosha, ukiangalia ajira bado, barabara zetu sio nzuri, ukitizama Bandari zetu bado zinataka kujengwa, maji safi na salama bado tatizo. Lakini niwapongeze sana Mhe. Mwenyekiti, hawa wawekezaji wa Raslhema wameonesha nia njema mwanzo kabla hawajaanza kuchimba mafuta haya na Mwenyezi Mungu awazidishie, awape imani hiyo ya kutusaidia, wameanza kutuchimbia visima 50 na matenki 50 wamejitolea kwa ajili ya Pemba na Unguja kuona shinda ya maji ipo kubwa, hawajaanza kuchimba mafuta wameanza kutusaidia.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ya Mafuta na Gesi ina fedha nyingi, hawa wawekezaji wa kuja kuchimba watusaidie kwanza kama wanavyoonesha Raslhema mfano wao wametusaidia mambo mengi. Sasa na hawa kampuni ya *Shells* kama watapewa kuchimba na wao basi watusaidie na wao barabara, hospitali, maskulim wanafunzi wetu wanatapa tabu juu ya usafiri kwenda huku na huku. Ukiangalia Pemba Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wanatembea karibu kilomita 5 au 6 kwa miguu kwenda skuli na kurudi kitu ambacho kinaumiza sana.

Mimi naomba sana hawa wawekezaji basi wasaidie na ukitizama, jambo jengine la msingi namuomba Waziri aangalie hawa wawekezaji wanataka kuekeza katika mafuta, lakini tuangalie Bandari mfano ya Pemba mambo mengi hamna. Kwa hiyo, hawa wawekezaji waambiwe kabla ya kuchimbwa haya mafuta basi kwanza wajenge Bandari ile ya Pemba kwa sababu wataweka vifaa vingi wataleta kama makontena mengi wataleta kwa ajili ya uchimbaji wa mafuta yale.

Kwa hivyo, waanze kuekeza kwenye Bandari waweze kutusaidia Bandari yetu kama ya Pemba iweze kuwa na vifaa na meli kubwa kubwa ziweze kufunga Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie mwisho hapa kwenye ripoti yetu ya Kamati nimemsikia Mwenyekiti anasema baadhi ya vitalu vya Zanzibar vinaendelea kulipwa kodi ya *TPDC* Bara wanalipa kodi kule. Lakini hizo ni changamoto za Muungano zipo, lakini kwa nia njema serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. sheria hii ikishapita kodi hii italipwa kwa Serikali ya Zanzibar SMZ, hata ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika kifungu cha 133 na 134 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuwepo kwa *account* ya pamoja. Lakini hii bado ni changamoto, lakini kwa nia njema hili suala lifanikishwe.

Lakini nasema hapa hii sio changamoto ya ugomvi baina ya Tanzania Bara na sisi visiwani. Mimi nitoe mfano mmoja Mhe. Mwenyekiti, hapa sisi katika kipindi cha nyuma tulikuwa na deni karibu bilioni sabini tunadaiwa, yaani *ZECO* wanadaiwa na *TANESCO* bilioni sabini. Lakini kama sisi ni Wajumbe wa kamati, mimi nilikuwa ni Mjumbe wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi niliwhali kufika mpaka Tanzania Bara *TANESCO* Mkurugenzi akasema tunadai *ZECO* bilioni sabini kesho tunaweza kukata umeme kutoka Bara kwenda Zanzibar umeme utakatwa mpaka mlipe dini, lakini kwa nia njema wenzetu wao wameshaanza kuchimba Gesi tangu miaka mitatu sasa hivi kuchimbwa Gesi na Gesi ile inatumiwa kwenye umeme sasa hivi pale Ubungo ukitizama mitambo iliyowekwa wanatumia Gesi hii. Lakini wenzetu neema hii yameshaipata lakini bado wanatusaidia kwenye umeme na ukiangalia mpaka leo *ZECO* ina deni kule *TANESCO* lakini hawatukatii na tunashirikiana.

Kwa hiyo, mimi naomba sana tushirikiane kwa pamoja, hii neema imekuja upande wetu, tukae pamoja tushirikiane sio suala la kugombana kwenye suala la Gesi na Mafuta kwa sababu ni neema Mwenyezi Mungu katupa na sote ni ndugu tukae pamoja ili tutoe changamoto hizi tuweze kuchimba mafuta yetu kwa salama na amani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi pamoja na Jimbo langu la Mtoni naunga mkono asilimia mia kwa mia kwenye mswada huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Abdalla Maulid Diwani:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi leo nikawa katika wachangiaji wa mswada huu wa utafutaji wa Mafuta na Gesi Zanzibar.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu hili kupata nguvu kuchangia haya nitakayochangia muda mfupi ujao.

Vile vile, napenda kutoa shukurani zangu za dhati ya moyo wangu kabisa, mimi pamoja na wananchi wa jimbo langu la Jangombe kuwa leo kuwa siku adhimu sana katika historia ya Zanzibar na Baraza hili la Tisa nikiwa Mjumbe wa mmoja Mhe. Abdalla Maulid Diwani tunapitisha au tunataka kupitisha Sheria ya Uchimbaji na Utafutaji wa Gesi na Mafuta Zanzibar.

Yapo mengi yalizungumzwa katika nchi hii kwamba, hayachimbwi, hayapo, hakuna, nini. Lakini leo hii hatiame Mhe. Waziri, kaja kasimama kifua mbele kututangazia sasa rasmi anasoma mswada huu na kwa niaba ya yangu na

wananchi wa Jang'ombe nazungumza kwamba mswada huu tunaupitisha kwa asilimia mia moja bila hata ya kimeme na kuweza kuiletea Zanzibar neema hiyo ambayo inazungumzwa kuibalisha ikawa kama mfano wa nchi nyengine hizo ambazo wanzungumza wenzetu.

Naomba niende moja kwa moja kwenye hoja zangu, mimi katika kuchangia mswada huu nitakwenda katika kifungu cha 15 ambacho kinasema:

"Sifa ya wenyeviti wa Bodi"

Mimi nitakwenda katika Wajumbe wengineo. Kiwango cha elimu. Hapa kwa kweli imeandikwa tu; "Wajumbe wawe na elimu" Elimu gani basi hiyo. Kutona na unyeji wa kazi hii *at least* kuweke vile viwango vya elimu angalau tuwajuwe wale watu ambao wanachanguliwa katika nafasi ya Ujumbe wana viwango vya aina gani ya elimu. Ukisema kuwa na elimu ya kujua kusoma na kuandika, kwa hivyo, watakuwa hawatupeleki kule ambako tunakuhitaji. Kwa hivyo, naomba kwanza Mhe. Waziri, hapo upaangalie ili mswada wetu uwe mzuri zaidi.

Vile vile, nitakwenda katika kifungu cha 21 katika mswada huu pale palizungumzwa kwamba:

"Kinga dhidi ya Wajumbe wa Bodi na Maafisa wa Mamlaka".

Mimi ningependekeza kwa muona wangu hichi kifungu kiondoshwe kwa sababu hichi kinaweza kutoa njia moja ya ufisadi. Naomba nikinukuu:

"Mjumbe wa Bodi au Afisa wa Mamlaka au mtu atafanya kwa maelekezo ya Bodi au Afisa wa Mamlaka kutohusika ye ye binafsi kwa kufanya au kuwacha kufanya kwa nia njema katika utekelezaji wa kazi chini ya sheria hii".

Sasa hii "kutohusika kufanya au kutokufanya", hii inawezekana kwamba itatumika vibaya, leo *Alhamudulilah*, tunazungumza kwamba Waziri anaeshughulika na masuala ya Mafuta na Gesi, Mwenyezi Mungu akijaali atakuwa Bi Salama wetu, tunamuweza na tumemzoea, baadae mbele Mungu bariki mambo yanabadilika tunampata mtu dhalimu hapa katika taasisi kama hiyo au jitu jambazi, ina maana tayari unamuwekea kinga za kufanya maamuzi ambayo yatakuwa hayana kheri kwa taifa hili baada ya kuijangalia ye ye mwenyewe.

Vile vile, naendelea mbele katika kifungu cha 33,(3) katika mswada huu uliopendekezwa wa uchimbaji wa Mafuta na Gesi ambazo zimesema ramani

iliyotayarishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo, tumepiga kelele sana tunataka kujua ramani zetu hizi ya vitalu vyetu viko wapi tujuishwe kabisa, tujue Zanzibar tuneshaambiwa kuwa kuna Vitalu 12, angalau tujue basi Kaskazini, Kusini na Mashariki katika visiwa vyetu vya Unguja, yaani kitalu chetu kinatoka wapi mpaka wapi ili visijekuwa na matatizo hapo baadae kwamba tuneshapistisha sheria hii, lakini ile ramani ya Vitalu vyetu tukawa hatuvijui. Sasa kama Wajumbe tunataka tupitishe kitu ambacho chenye kukielewa, kwa hiyo, tujuishwe.

Vile vile, nitakwenda mbele katika kifungu 45(5), juu ya utoaji wa leseni. Imezungumzwa hapa kwamba leseni itatolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), itataka kampuni kuwa na hisa isiyozidi asilimia 25. Hapa kidogo munatuumiza padogo. Tuandike hapa neno "isiyopungua", kwa sababu isiyosidi asilimia 25, anaweza kusema mtu awe asilimia 10, asilimia 5 ni ndogo sana katika shughuli nyeti kama hii. Angalau isiyopungua asilimia 25, angalau tumemfunga hapa *twenty five percent*, lakini ukisema isiyozidi, atakwambia mimi ninaingia mkataba katika asilimia 5 au 10, itakuwa kwa kweli siyo vizuri.

Kwa hivyo, nikiendelea mbele vile vile nakuja kwenye Kinga ya Waziri. Waziri kapewa mamlaka makubwa sana katika hili. Mimi ningeomba tu apunguziwe kidogo ili iwe *cabinet* au Baraza la Mapinduzi au pengine Bodi na Mamlaka husika ndizo zinawenza kumshauri Waziri moja kwa moja, hata katika maamuzi magumu kwenye hili, basi BLM au *cabinet* itoe maamuzi katika suala zima juu ya kadhia hii ya Gesi na Mafuta.

Vile vile, nikiendelea mbele kuwepo kwa wataalamu wa kutosha. Ni kweli wenzetu wanasema kwenye Mswada huu, ninafikiri bado hatujakuwa na wataalamu wa kutosha kama wenzetu wamesema wamekwenda kutembea Songosongo wakabahatika kuona wafanyakazi wa pale karibu kumi na tano, *ma-experts* wa pale wote ni Watanzania. Kwa hivyo, na sisi tutaji-*proud* tutakapopata wataalamu halisi kutoka Zanzibar wanasmamia shughuli ile na itakuwa ni sifa nzuri na itaondokana na ule usaliti wetu wa kuwapa kazi hizi watu wa nje wakati watu wa ndani wenye zile sifa watanyimwa.

Kwa hivyo, tujitahidi sana kusomesha watu na sasa hivi bado muda tunao kidogo ili wazalendo wa kweli waje kusimamia katika raslimali hii baada ya kuwa faraja kwetu hii, isije kuwa adhabu. Mwenyezi Mungu atuepushie mbali.

Vile vile, nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, juu ya suala zima la utafutaji wa kampuni. Sasa hivi watu wanazungumza baada ya kuletwa Mswada tu,

washaanza kuzungumza kuna *Ras Gas*. Mimi niseme kwamba kuna watu wanaanza kuposa mimba. Hatujajua kinachokuja kuzaliwa lakini tayari watu wanaanza kukiposa. Kwa hivyo, tuangalie na hata hawa watu wenye we wapo viyi na wana sifa ya aina gani, na wameshafanya kazi wapi. Kwa sababu utakapompa huyu, ukatafuta mtu mwengine itakuwa biashara juu ya biashara. Yeye kafanya biashara na sisi, na ye ye kenda kampa mtu mwengine kufanya biashara. Kwa hivyo, hatutoendelea sana. Hivyo, tupate watu ambao *exactly* wenye uwezo na wenye sifa na ujuzi wa kutosha juu ya suala zima la tafiti mpaka kufika kutupatia gesi yetu hiyo au mafuta.

Pamoja na tafiti zote za uchimbaji, vile vile, kuna tatizo tumeruhusiwa tuchimbe mafuta, lakini ninapata wasi wasi kwamba hizo pesa zote za mauzo ya mafuta haya, pesa zake ziingie kwenye Mfuko wa Maendeleo wa Mafuta. Sasa hapa kidogo panatupa wasi wasi. Lakini ninajua sisi sote ni ndugu, hatuwezi kugombana kwa hayo, tutafika pahala tutaambizana na tutafikia muafaka tutakubaliana. Unajua siku zote ndugu hawagombani, wanaelekezana tu. Pale ambapo wameona tumekosea basi tunakaa na wenzetu tuwaambie bwana wee! munatwambie kwamba hizo pesa zote ziingie katika Mfuko wa *TPDC*, aah! sasa hivi kuna *ZPDC*. Kwa hivyo, ninafikiri itafika wakati tutakubaliana mpaka kufikia shughuli nzima hiyo ya mafanikio katika nchi yetu.

Vile vile, limezungumzwa suala zima la mazingira. Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwenye rasimu hii kuwa mazingira yapewe kipaumbele. Kwa sababu tukumbuke katika maeneo yetu kuna shughuli mbali mbali zinafanyika; shughuli za kilimo, uvuvi kwa hizo sehemu ambazo zitakazochimbwa gesi. Hivyo, lazima na hawa watu tujitahidi sana katika kuwaangalia mazingira kwanza. Kama tutakuwa na mazingira mabovu ninafikiria hata hicho ambacho tunachokitafuta leo hii, itakuja kuwa adhabu kwetu sisi.

Kwa hivyo, ninaiomba sana Serikali, ninajua imeshafanya tafiti zote na mpaka imeleta huu Mswada, haya mambo yote ninajua wameshayapitia. Ni Serikali sikivu na inafahamu kila kitu, lakini kwa sababu hili suala la unyeti wake kwa mara ya kwanza leo Zanzibar linazungumzwa suala zima la gesi na mafuta. *Of course*, tusiogope changamoto zake. Changamoto ndogo ndogo tutakaa pamoja, ikiwa kwamba kule kwenye Serikali ishakuwa kubwa basi tuletewe katika Baraza la Wawakilishi ili kuweza kuangalia na kuweza kusaidia kuhakikisha kwamba tunazitatu hizi changamoto na kuendelea mbele na shughuli nzima ya uchimbaji.

Baada ya hayo machache mimi niseme kwa sababu umenishitukiza kidogo, nitaendelea kusikiliza zaidi na ninaunga mkono huu Mswada wa gesi na mafuta kwa asilimia mia moja kabisa. Na ninawashauri Wajumbe wenzangu pamoja na kuichangia kwetu vizuri lakini tuiunge mkono bila ya kumpa matatizo Mhe. Waziri, ili akajipange vizuri kwa shughuli nzima ya utafutaji mafuta Zanzibar. (*Makofî*)

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofî*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Sasa anayefuata Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Omar Seif Abeif, ajitayariske.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataalla* kwa kutujaalia jioni ya leo nikapata fursa hii na mimi kuendelea kuchangia mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Micheweni. (*Makofî*)

Baada ya hapo, naomba Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja mimi niende katika kuanza kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kuangalia na unyeti wa jambo hili ambalo kama wenzangu ambavyo wametangulia kusema, limeshazungumzwa sana na limeshapigwa kelele sana, lakini leo tunalo mezani tunaendelea na mchakato katika kuona kwamba tunapitisha hili na hatimaye tuweze kupata mafanikio kwa lengo la kupata maendeleo zaidi katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba nianze kwa kuanza na ushauri, lakini kabla ya ushauri mimi niseme kuwa Kamati leo imefanya kazi kubwa sana, kwa kuwasilisha ripoti yake na jinsi ambavyo imeshauri na mapendekezo ambayo wameyatoa. Ni kwamba wamefanya kazi kubwa ambayo Kamati hii nichukue fursa hii kuwapongeza sana kwa kazi kubwa na ngumu ambayo wameifanya hatimaye leo wakaweza kutushauri. Sasa sisi fursa nyengine ambayo tunayo sasa hivi ni kwamba tunapitapita tu lakini kazi imeshafanywa tena ni kazi nzuri na ya kupigiwa mfano sana. (*Makofî*)

Naomba sasa moja kwa moja niende na uzoefu na ushauri. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli uzoefu katika miradi mbali mbali inayoasisiwa hapa nchini imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto kubwa ipo katika *level* ya wananchi huko vijijini. Kwa sasa ni kwamba tuna maeneo ambayo tayari yameshatambuliwa kuwa yameshafanyiwa utafiti kuonekana kazi hii ya

uchimbaji wa mafuta inatarajiwa ifanyike katika maeneo yale. Lakini kama nilivyosema uzoefu ni kwamba tumeshuhudia migongano, vikwazo mbali mbali vinavyojitokeza ndani ya jamii, ama kwa kusikiliza watu au kwa kutokuelewa wenyewe ni mambo ambayo kwa kweli yanatokea sana.

Sasa kwa kupitia fursa hii naomba nishauri kwamba ni vyema kabisa katika kuliangalia suala hili kabla shughuli nyengine kubwa hazijaendelea kuhakikisha kuwa Wizara inayohusika kuweza kuangalia kukaa katika yale maeneo ili kuyadhibiti mapema na kuanza *process* ya kuondoa vile vikwazo vidogo vidogo kwenye *level* ya wananchi, ili pale shughuli itakapokuja kuanza kusije kuwa na migongano mikubwa ambayo itakuja kufanya au ya kuja kutoa mianya ya kuweza kusitisha zoezi kwa hatua ambayo labda inatarajiwa ifikiwe. Hili naomba sana lifanyike kwa sababu tumeshaona na kushuhudia mambo mbali mbali.

Kwa mfano, katika jimbo langu kuna miradi mingi ambayo ilianzishwa na mengine inataka kuanzishwa. Lakini kwa uelewa mdogo wa jamii basi kulitokea vikwazo mbali mbali na badala yake watu wakawenza kuiona kama Serikali, kwamba labda ina nia mbaya na wananchi kwenye maeneo husika. Sasa ili kuepuka hili ningeomba sana kwamba Mhe. Waziri pamoja na watendaji na ninaamini wewe mwenyewe upo makini ninadhani hili tulifanyie kazi mapema kabla halijaleta usumbufuli katika wakati ambao tunatarajia hiyo kazi kuanza rasmi.

Baada ya hapo naomba tu mimi niende katika Sehemu ya Pili kwenye kuangalia haki za mafuta na gesi asilia kusimamiwa na Serikali. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba ufanuzi umeshaanza kutolewa na wakati Mwenyekiti alipokuwa akichangia wa Kamati alitutoa hofu, lakini bado hofu kwa watu wengine tunaweza kusema ni jambo ambalo linaweza likawepo kwa maumbile ya binadamu. Kwa mfano, leo tunataka kuupitisha Mswada huu lakini tukumbuke kwamba Mswada huu tunaoendelea nao, sasa hivi tunatumia Katiba ambayo ipo kwa sasa hivi ambayo katika mambo ya Muungano kama vile ambavyo tuliviyokuwa tumeona ni kuwa bado hili suala lipo mambo ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, Ijapokuwa kwamba tunaambiwa kuna makubaliano, makubaliano siyo jambo bayu na mimi ninaliafiki sana na kama vile vile mfano Mwenyekiti wa Kamati alipotoa ushuhuda kwamba kwa mfano kama TRA, tumekubaliana na sisi tunakusanya na wao wanakusanya hakuna migongano yoyote. Lakini bado jambo hili tuna Katiba ambayo inapendekezwa

tumeshawoneshwa mazingira kwamba inatoa mwanya kuwa Zanzibar kuweza kujitegemea kwenye suala hili kufanya shughuli zake wenyewe.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala langu na hofu yangu ni kwamba tunaingia katika kuja kuipigia kura hiyo Katiba ambayo ni pendekenzwa. Tunatarajia kwamba itapita lakini je, suala kama haijapita itakuwaje. Hiyo ndiyo hofu yangu. Ningombwa sana pamoja na mambo mengine basi ninadhani ni vyema katika kuharakisha kwenye zile hatua mbali mbali tukiwa tukiendelea, lakini na hili pia Serikali ni vyema zaidi kupitia Wizara husika itoe tamko ambalo litakuwa ni vyema zaidi katika kuliangalia kwa upana wake jambo hili.

Kama imepita Katiba ni jambo moja zuri, ninadhani tutakuwa hatuna kikwazo chochote, hatua yetu itakuwa haina tatizo, lakini endapo je, Katiba haikupita iliyopendekenzwa na badala yake ikaja ikatumika hii hii, ninadhani kuwe na jambo jengine la kufanya. Nilitaka nitoe wasi wasi kuhusiana na jambo hili. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee katika ukurasa wa 73 kwenye Kifungu 1(a), kinasema;

"Kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika sekta".

Hapa kwenye kipengele hichi ningetaka kujua tu labda sekta ipi. Kwa sababu sekta hapa ambazo zinaweza kuwepo zinaweza zikawa sekta fulani, sijajua ni sekta ipi. Kwa hivyo, ningependa kujua au tuongeze neno "katika kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika sekta", lazima tuseme tuainishe sekta ipi. Maana sekta yenyewe sijajua au sekta haijajulikana. Hivyo, ningombwa sana Mhe. Waziri, atakapokuja atuweke mazingira mazuri ili kuweza kupata kuelewa zaidi juu ya lile ambalo hapa litakuwa limekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende katika ukurasa wa 85. Katika ukurasa huu kwenye Kifungu cha 49(4), kinasema kwamba;

"Waziri anaweza kupitia Kanuni kueleza namna ya utaratibu wa kusimamia zabuni".

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina wasi wasi na Waziri aliyepo sasa hivi. Ni kwamba ni mtu ambaye ninamuamini sana na kufanya kazi vizuri. Lakini kwa vile Rais ana mamlaka mwenyewe ya kuweza kumteuwa mtu ye yeyote, wasi wasi wangu ni kwamba fursa hii kwa Waziri ambapo pengine wakati anaweza akaja

kuwa si mtu ambaye ni mpenda maendeleo, akaja akaitumia fursa hii kwa *interest* yake. Hivyo, hii mimi ninahisi kwamba hapa panatoa mwanya wa kuweza kumfanya Mhe. Waziri, kulitumia rungu hili kwa maslahi yake au kwa *interest* yake.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo yangu naomba basi hapa tupazingatie kwa kusema labda kwamba; "Waziri anawenza kupitia Kanuni kueleza namna na utaratibu wa kusimamia zabuni", lakini vile vile kuwe na watu wengine au kuwe na chombo chengine ambacho kitatajwa ndani ya Mswada huu ili ijulikane kwamba na isiachwe hivi hivi tukaja tukaambwi pengine kuna na Bodi, sijui kuna nini, lakini tuainishe hapa kimaandishi. Kwa sababu maandishi ndiyo ambayo yanatoa kifungu cha mtu au kuweza kumzuia mtu asiweze kuitumia fursa kwa anavyotaka mwenyewe. Ningeshauri sana Mhe. Mwenyekiti, hili Mhe. Waziri, atakapokuja pia nalo alizingatie.

Lakini niende katika ukurasa wa 86, kwenye kifungu cha 53(2) kinasema;

"Waziri atatoa sababu za kukataa au masharti ya kutoa leseni".

Mimi kwa ushauri wangu hapa naona kidogo tungebadilisha kidogo, tukasema kwamba; "Waziri atatoa masharti kwanza yaanze na badala yake masharti ya leseni au sababu za kukataa", na isisomeke kama ilivyo sasa kwamba; "Waziri atatoa sababu za kukataa au masharti ya kutoa leseni", ninarejea isomeke; "Waziri atatoa masharti ya leseni au sababu za kukataa". Ningombaa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, atakapokuja ninadhani ni vyema hili nalo pia tulizingatie.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende ukurasa wa 117...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda wako unakaribia kumaliza, bado dakika moja.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Ninamalizia Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 117 (3), inasema;

"Kampuni na Mkarandasi watalipa fidia kwa mamlaka kwa athari yoyote na Gesi Asilia na njia mbadala za kulipa fidia zitafuata".

Lakini mimi nilikuwa ninauliza hii mamlaka tayari imeshawekewa uhakika, lakini je, kwa upande wa wananchi inakuwaje. Kwa upande wa wananchi viyi wananchi wao kuhusu hiyo fidia. Kwa sababu itakapokuwa tukifanya usambazaji wa hii gesi, ninadhani kutakuwa na mabomba, wakati mwengine mafuta yanaweza yakavuja au gesi ikavuja na wakati mwengine mafuta yakachafua bahari na viumbe hai. Sasa mimi ninadhani mamlaka imeshaona kwamba imeshakikishiwa hapa, lakini kwa wananchi naomba pia hapo ingeonekana kuwa na wao pia wanaweza kupata fursa hii.

Lakini kwa vile muda umeshakaribia kumaliza naomba niende moja kwa moja kwenye 115. Kuna kipengele katika 115 (c) anasema;

"Kuendeleza, kuwasilisha mpango unaonesha njia ya kujikinga na ushughulikaji na upunguzaji wa virusi vyta Ukimwi na maradhi mengineyo".

Mhe.Mwenyekiti, hapa naona kidogo ningeomba tufanye marekebisho. Marekebisho yangu naomba tusitumie hii kusema "upunguzaji wa virusi vyta Ukimwi" na badala yake tuseme "upunguzaji wa maambukizi ya virusi vyta Ukimwi". Ninadhani kitaalamu kw lugha za kiafya inapendeza zaidi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Muda umemaliza.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe.Mwenyekiti, Ninakubali kama muda wangu umemalizika, naomba tu moja kwa moja kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu naunga mkono asilimia mia moja Mswada huu. (*Makofii*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa ni zamu ya Mhe. Omar Seif Abeid, tafadhali na baadae atafuatia Mhe. Mgeni Hassan Juma.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia. Mimi kwanza kabla ya yote nitaunga mkono mara mbili. Mara ya kwanza kabla ya kutoa mchango wangu ninasema naunga mkono hotuba hii au Mswada huu kwa asilimia mia. Lakini pamoja na kuunga mkono kuna mambo kidogo na mimi naomba niyachangie. (*Makofii*)

Kwamba maneno madogo madogo ambayo ni matatizo ya kibinadamu. Binadamu sisi sote hakuna ukamilifu. Kwa hivyo, pale tunapoyaona ni vizuri tukafanya kwa umoja wetu kuyarekebisha. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nianze moja kwa moja kwenye huu ukurasa wa 66, kuna maneno madogo madogo ambayo kidogo yamekosewa.

Kama kwenye neno "Bodi". Bodi maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka iliyoanzisha. Kwa hivyo, hilo neno "anzisha" lina *error*, kwa hivyo, naomba lirekebishwe. Lakini pia hiyo kuna tafsiri ya ufukwe. Hili neno la 'ufukwe' mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa tunavyofahamu sisi ufukwe ni sehemu ambayo maji ya bahari yanaishia na kutoka, na baadae pakabakia mchanga ndiyo maana ya neno 'ufukwe'. Kwa hivyo, wataalamu au wafasiri wa Kiswahili waliandika hili neno 'ufukwe' walitafsiri vizuri, siyo kwamba kuna maji ya kuingia na kutoka. Hata kwenye miamba huko watu wanakokwenda kuchokoa pweza maji yanaigia na kutoka. Lakini tafsiri ya ufukwe au eneo la ufukwe ni sehemu ya maji yanayoingia na kutoka baadae ukabakia mchanga karibu na ardhi ya nchi kavu. Kwa hivyo, hilo neno mimi napendekeza kwamba hiyo tafsiri ya neno 'ufukwe' iwekwe sawa.

Kuna maneno mengine Mhe. Mwenyekiti, naomba tafsiri, kwa sababu sisi pamoja na kusema kwamba Kiswahili hakijitoshelezi, lakini Kiswahili kinajitosheleza. Kwa hivyo, mimi napendekeza maneno yasijirudie, kwa sababu maneno yakijirudia unakosa ile tafsiri halisi, ingawa watu wa sheria watakuambia ni maneno ya kisheria, lakini na sisi ni Waswahili kwa sababu tunakijua Kiswahili, maneno sio vizuri kuyafanya yakajirudia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano utaona neno kama 'kibali', wameandika neno 'kibali' wanasema maana yake ni kibali. Ina maana limeshindikana neno la kutumia likawa ni maana ya neno 'kibali'. Kwa hivyo, mimi napendekeza hayo maneno Mhe. Mwenyekiti, yasipende kujirudia rudia, kwa sababu pamoja na mambo mengine ni vizuri haya maneno pamoja na kuwa ni ya kisheria, kwamba wananchi wayaelewe kwa sababu watataka kuelewa baadhi ya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, niende tena kwenye maeneo katika ukurasa huo huo wa 68. Kuna maeneo haya yalijotajwa ya meli 200. Narudia tena kuomba, kwamba hizi meli 200 ziainishwe, kwa sababu sisi tunapozungumza meli 200. Kwa mfano, sisi Pemba tumepakana na nchi jirani ya Kenya, tukizungumza meli 200 pale sisi tuko ndani ya Mombasa na tuna bahari pale, wanaita *Pemba Channel*, wenzetu wa Mombasa ndio wanaitumia kama yao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka waziri atakapokuja hapa aniambie, ni lini atasimamia mipaka hasa ile ya Pemba, kuweza kujua sisi maeneo yetu halisi ya Pemba kati ya Kisiwa chetu cha Pemba na Mombasa, kwa sababu kule tuna imani kwamba hilo *Block No. 12* liko huko, na wenzetu wa Kenya hivi sasa mchezo wao wote hawachezi mbali, wanachezea pale pale, boti zao za uvuvi ziko pale na vitu vyao viko pale kwenye hiyo *Pemba Channel*.

Kwa hivyo, naomba haya maeneo yaainishwe na tukirudi kwenye bahari kuu, pia inasemekana kwamba, hatuna uhakika wataalamu watakuja kutuambia kwamba maeneo yanayotajwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kupata mafuta haya kwa wingi, ni eneo liliopo Kaskazini Mashariki kati ya Kisiwa cha Unguja na Kisiwa cha Pemba, ambapo huko inasemekana kwamba ndipo waliko hao Tuna, eneo la Tuna linalotajwa ndio eneo lililokuwa lina mafuta.

Mimi ninapendekeza kwamba waziri atakapokuja, tumeshapitisha mswada huu, lakini shauri la mipaka ni jambo muhimu. Wenzangu wamelisema sana na mimi nalirudia, kwa sababu tumezikuta nchi nydingi zikiingia kwenye mizozo baada ya kupatikana kitu, siku zote pakiwa hapana kitu huwa hapana maneno, lakini pakitokeza kitu basi maneno yanaanza.Utakuja kusikia Wamarekani wamesema kwamba hizi meli 200, pia na wengine wenye uwezo wao na ubavu wao wanaweza kuja wakasema aah! eneo hili ni la kimataifa, kwa hivyo, sisi tunaweka *base* yetu tunachimba.

Kwa hivyo, pamoja na mambo mengine, lakini meli 200 mimi napendekeza zitajwe kwenye eneo la Kaskazini Mashariki ya Kisiwa cha Unguja na Pemba zote. Suala hili namuomba Mhe. Waziri, akija kwanza suala la mipaka ndio kilio chetu, wawakilishi kila anayesimama hapa anazungumzia suala la mipaka. Mimi nafikiria Mhe. Mwenyekiti, sisi hakuna mjambe anayeupinga huu mswada, imani yangu ni hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwenye ukurasa 72, kuna neno 'vifaa' vile vile nilipendekeza litafutwe neno jengine, kwa nini iwe vifaa, vifaa na vifaa ni zana. Au ukiisoma hii kwenye ukurasa wa 72 utakuta neno 'vifaa' anasema maana yake ni kiwanda, jengo au vifaa vinavyopataikana. Sasa mimi nauliza hiki kiwanda nacho ni kifaa. Kifaa mimi najua ni zana inayotumika kwenye kile kitu, sio jengo, jengo ni jengo na kifaa ni kifaa na zana ni zana. Kwa hivyo, hili neno mimi naomba lirekebishwe Mhe. Mwenyekiti.

Pia, kuna jambo moja nimeliona ambalo mimi napenda kutoa ushauri lifanyiwe marekebisho, katika kifungu cha 5 kinasema; "Serikali kupitia kampuni inaweza kuingia makubaliano na mkandarasi au mtu ye yeyote". Mimi napendekeza kwa uzito wa hili jambo, waziri anayehusika na hii wizara akishirikiana na hiyo kampuni, lakini ye ye waziri ndiye awe *mas-ul* wa kusaini mikataba ya mambo haya ya mafuta na gesi, asiachiwe mtu mengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 75, mstari wa pili, neno 'wanaopiza' kuna mapungufu kidogo, lisomeke 'wanaopuuza', kuna neno linaitwa 'wanaopiza', sijui kama kuna Kiswahili kinachokubaliana na hili neno 'wanaopiza'.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwenye ukurasa wa 76 (1), kwamba; "kampuni au mkandarasi anaweza kupewa adhabu". Lakini kwenye kifungu 5 cha ukurasa wa 72, kampuni ndio imepewa uwezo. Sasa tujitizame huku kampuni inashtakiwa, na kadhalika, lakini huku kampuni ndio imepewa kwa niaba ya serikali iweke saini, itafute kampuni isimamie kila kitu. Mimi naona mamlaka ya hizi kampuni pamoja na kuwa ni ya serikali, lakini sio vizuri kila kitu kuiachia kampuni. Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria serikali kuu iwajibike iwe ndio *mas-ul* wa mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 88, kifungu kidogo cha (2) kwenye mstari wa pili ule, kuna neno 'utafutaja', naomba lirekebishwe ni 'utafutaji' badala ya utafutaja. Kifungu cha 34(3)(vi) kuna neno limeandikwa 'hathari' liandikwe 'athari' lirekebishwe. Ukurasa wa 84, kifungu cha 45(3) imeandikwa 'haiaulishwa', lisomeke 'haitahaulishwa'.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 84, kifungu cha 45(7), kinasomeka kwamba; "Kwa madhumuni ya sheria hii kampuni itaiomba kampuni..." Sasa tuijulize ni kampuni gani itakayoiomba kampuni.

Mimi napendekeza irekebishwe na itamkwe hasa, "kampuni tanzu itaitaka kampuni kuomba leseni...", lakini hapa kampuni itaiomba kampuni. Sasa kampuni gani itaiomba kampuni. Kwa hivyo, ni vyema ikaainishwa kwamba ni kampuni ipi ina uwezo wa kuitaka kampuni nyengine. Kwa hivyo, hapa isomeke "kampuni tanzu itaitaka kampuni kuomba leseni...", mpaka mwisho wa sentensi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama wenzangu walivyotoa tahadhari juu ya mambo haya, kwamba suala hili la mafuta na gesi ni kilio chetu cha muda mrefu. Tumeanza kukisikia kilimo hiki kikipigwa mbiu ya mgambo siku nyingi, tukaambiwa watoto nyoka yuwapi na aje, nyoka yuko, mpaka sasa nyoka amefikia alipokuwa anatakiwa afike, kwa hivyo, nyoka amefika. Kwa hivyo, mimi ni imani yangu kabisa kwamba suala hili limekuja wakati mzuri, na ni jambo la kufurahisha, kwa ajili ni jambo lenye muelekeo wa kuleta maslahi ya nchi yetu. Lakini kila penye uzuri hapakosi kasoro. Tujitahidini kwa sababu sisi ni binadamu kasoro hazikosekani. Pale panapotokezea kasoro basi tuwe wepesi wa kukubali, kwamba kasoro imetokea, watu waitane na wakae pamoja watengeneze kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki kumaliza muda wangu, kwa sababu ya jambo hili, narudia tena kusema kwamba naunga mkono mswada huu kwa

asilimia mia, na ni imani yangu kwamba wawakilishi wote tutaukubali. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono. (*Makofî*)

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii adhimu kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia, katika mswada unaohusiana na Sheria ya usimamizi wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, pia kwa kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, ambaye katujaalia kuwepo hapa tukiwa wazima wa afya kabisa na kuweza kuendelea na shughuli zetu.

Pia, nichukuwe fursa hii adhimu Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutuletea mswada huu ambaao ni mswada uliokuwa muhimu sana. Katika kipindi kirefu sana mswada huu tulikuwa tuna usubiri kwa hamu uletwe tuweze kuupitisha, ili sasa na sisi Zanzibar tuwe na uwezo kamili wa kutafuta na kuchimba mafuta pamoja na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote katika wizara, wakiwemo wana sheria pamoja na wataalamu mbali mbali, ambaao wameweza kuukalia mswada huu na kuufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe pongezi sana kwa Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia masuala ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na kamati ambayo inahusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, niseme kwamba nilibahatika kuwa katika kamati hii, sio kwa sababu ni mjambe wa kamati, lakini nilipewa mualiko kwa sababu mimi nilikuwa ni mmoja wa wadau ambaao walialikwa kuweza kutoa michango ndani ya kamati hii. Kwa kuwa sisi wanawake wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi ni wadau wakubwa sana wa suala zima la utafutaji wa mafuta na gesi asilia, kwa hivyo, tulipewa nafasi hii kushiriki kikamilifu ndani ya kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeanza kwa kuipongeza serikali, kwa sababu ya mambo mawili, mbali ya kuuleta mswada huu, lakini Sera ya uchimbaji wa gesi na mafuta Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sera hiyo imewekwa vizuri sana. Ni sera ambayo imemitzama kila mtu ndani ya jamii tukiwemo sisi wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwapongeze sana wizara, kwa sababu sera hii ndio ambayo imeweza kuleta sheria ambayo itaweza kutekelezeka vizuri. Lakini jengine sera hii imeweka msingi mzuri sana madhubuti, ambao unaifanya sheria hii iweze kutengenezewa mpango mkakati ambao utaweza kutumika kwa kipindi kirefu kwa ajili ya kutafuta na kuchimba mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapo awali ulipokuwa unaletwa mswada huu na wakati nauangalia nilianza kutaharuki, hasa kwa kuwa nilisoma tafiti mbali mbali za nchi mbali mbali na kutizama namna gani mwanamke, aidha, alivyo faidika au alivyo athirika na uchimbaji wa gesi na mafuta. Kwa bahati mbaya sana katika nchi mbali mbali ambazo akina mama wengi walikuwa wanajishughulisha na harakati za kiuchumi wakitumia ardhi, lakini walikuwa wajasiriamali wanaofanya shughuli mbali mbali, kwa bahati mbaya sana wameathirika vibaya sana katika nchi zao, hasa kwa sababu ya sekta hii ya gesi na mafuta. Lakini tatizo kubwa lilikuwa ni kushindwa kuwajumuisha wanawake, pamoja na makundi mbali mbali katika sera zao.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, sera yetu imetuonesha dhahiri kwamba shughuli hii itakayofanywa, basi itamjumuisha kila mwanamke ambaye alikuwemo ndani ya ardhi hii ya Zanzibar.

Jengine ambalo mimi nimeliona kuwa ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti. Wakati tukiwa katika kamati nililiona suala la uteuzi wa bodi ambapo mamlaka amepewa waziri. Kulikuwa kuna uteuzi wa wajumbe kadhaa, lakini ikajitokeza kasoro na tukatahadharisha kwamba kasoro ile inayojitokeza basi inaweza kusababisha wanawake kusahauliwa kuwemo ndani ya bodi hii. Mhe. Mwenyekiti, hili sio geni linatokea sana na kwa bahati mbaya sio kwa makusudi, kwa sababu sheria zetu hazimbani yule anayeteua, hukumbuka jinsia nyengine. Nasema nikikusudia mwanamke, humkumbuka kwamba na ye ye ni sehemu ya maendeleo ya nchi hii, matokeo yake kuna bodi nyengine hazitambui ule ulazima au ule umuhimu wa kumuweka mwanamke ndani ya bodi zile.

Kwa kweli tulishauriana sana na wataalamu, lakini nashukuru sana kifungu kile cha 12 kilifanyiwa marekebisho na suala zima la kuzingatia jinsi limo, nashukuru sana na ninawashukuru sana wanasheria kukubali suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo nawaomba sana akina mama wenzangu wote waliomo ndani ya Baraza hili, waikubali sheria hii kwa asilimia mia moja. Hilo Mhe. Mwenyekiti, nafikiria halitokuwa gumu kwetu sisi akina mama kwa sababu mimi nafahamu wawakilishi wanawake waliomo humu ndani ya Baraza

ni madhubuti, lakini ni waelewa wazuri sana na wamekuja hapa kuwawakilisha wanawake wengine ambao wamewachagua. Kwa hivyo, mimi naamini kabisa kwamba kwa upande wetu sisi wanawake, na nadhani ni Baraza zima, siwezi kusema tu wanawake, lakini na wengine wote wajumbe wataiunga mkono sheria hii ili sasa iweze kutumika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba sana na katika utafiti wangu, kwenye mambo ambayo nimeyagundua, vile vile, nimeona kwamba nchi nyingi wakati zimeanza suala la kuchimba mafuta, kuna suala ambalo walikuwa wanalisahau sana ni suala la jamii kuwa na mahusiano mazurina suala zima la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, lakini mimi nishukuru kwamba pamoja na yote sera hii imehakikisha inaleta ukaribu wa kiuchumi, lakini vile vile wa kimazingira na kijamii kwa jumla.

Lakini ningeomba sana katika utayarishaji wa mipango au tunaweza kusemea *frame work* ambayo itatayarishwa kwa ajili ya utekelezaji kuhakikisha kwamba wataalam katika sekta zote hizi wawemo ndani ya matayarisho haya.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, wakati tunazungumza suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi asilia, tujue kwamba sekta nyengine zitakuwa zinakuwa vile vile, kwa hivyo, hapa tunapozungumzia suala la kutayarisha wataalam tujue tutahitaji wataalam wengine zaidi katika sekta ya afya, sekta ya miundombinu na sekta ya elimu. Kwa hivyo, kwa ufupi katika sekta zote lazima tuhakikishe kwamba tunakwenda sambamba na uchimbaji au utafutaji wa mafuta. Kwa hivyo, ningeomba sana hilo tulitilie maanani sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la tuone namna gani mitaala yetu ya elimu itakavyoweza kuitisha na suala zima la utafutaji na uchimbaji mafuta na hilo lianzé katika shule za msingi, najua mipango hiyo ipo, lakini ningeomba sana katika kipindi hiki hiki shughuli hiyo ianze ili sasa tuanze kutayarisha vijana kwa ajili ya shughuli hizi za utafutaji na uchimbaji wa mafuta, tunajua athari yake ipo wapi, inaweza kufika wakati. Mimi nashukuru wakati tumo ndani ya kamati Mhe. Waziri, alituhakikishia ana wataalam wa kutosha kwa sasa hivi kwa masuala mbali mbali na wengine wamekwenda kwa ajili ya mafunzo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokifahamu mimi katika sekta hii hawatakiwi tu wataalam wanaoshughulikia kwa ngazi ya *Degree* au *Diploma* au Elimu ya Juu zaidi, kunatakiwa wataalam wengine ambao watakuwa zaidi wanatumika katika nguvu kazi na wataalam hawa kwa bahati nzuri sana tuna *vocational training* hapa *centres*, mimi ningeomba sana hizi *vocational training centres*

zetu sasa zianze kutayarishwa, ili kuhakikisha tunapata wataalam katika masuala hayo. Tuna mambo mengi sana ambayo wanaweza kuyafanya ambayo yanahuasiana na uchimbaji wa mafuta, sio lazima tupate watu wenye *Degree*, lakini hata yule ambae atapewa mafunzo ya kutengeneza na kuunganisha vyuma na kufanya mambo mengine, basi anaweza kushiriki kikamilifu katika suala zima la uchimbaji na utafutaji wa gesi asilia na mafuta.

Kwa hivyo, ningeomba sana wakati huu tulionao mimi ukinambia kutafuta mafuta na gesi, tumeambiwa kwamba kwa kipindi cha miaka mitano baadae ndio yanaweza kugundulikana, lakini hichi kipindi cha miaka mitano Mhe. Mwenyekiti, mimi nakiona kidogo sana matayarisho yanatakiwa kuwa makubwa sana, makubwa sana. Sasa najua kwamba uwezo huo tunao, lakini hawa ambao wanakuja kuchimba mafuta au hawa wanaokuja kuanza kutafuta tuhakikishe *to the maximum* wanatoa misaada hususan kwenye suala la elimu la kutayarisha nguvu kazi, katika kuhakikisha watakaoweza kufanya shughuli hizi za kiuchumi basi wawe ni wazawa wa hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana hili ningeomba Wizara kushughulikia suala la elimu.

Mhe. Mwenyekiti, elimu kwa jamii, suala la elimu kwa jamii ni muhimu sana na sote tunafahamu sisi wanasiasa kila mtu huko nje anasema lake, na jamii yetu kwa bahati mbaya sana mara nydingi sana inakosa elimu na taarifa za kutosha na matokeo yake wanaamini vile ambavyo vilivyokuwa sio kweli. Sasa ningeomba sana kwa Wizara ni wakati wa kutoka nje wa kutumia media zetu Redio. Televisheni, lakini tuna mitandao mbali mbali kuanza kuelimisha wananchi kuhusu elimu hii ya mafuta. Wananchi wasije wakabweteka wakasema sasa tunaanza kuchimba mafuta tayari tumeshakuwa matajiri na wakaacha kufanya shughuli zao za kiuchumi ambazo wanafanya kila siku. Hilo limetokea katika mataifa mengine.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri, wewe ndiye uliyepewa dhamana na mimi nakuamini sana, una uwezo mkubwa wa kusimamia hili, Mhe. Waziri, tunakuomba hili ulisimamie uhakikishe jamii nzima inafahamu maudhui yote kwa nini tunachimba mafuta na lini mafuta hayo yataweza kutusaidia, na fedha zake zitakwenda wapi na zitamfikia nani na nani katika jamii.

Vile vile, tujaribu kuhakikisha kwamba kile ambacho kinapatikana kinasaidia wajasiria mali wetu, yale ambayo tunaona kwamba yanaweza kufanya wa Zanzibar katika nchi kwa mfano nchi ya Nigeria, wakati wanachimba mafuta watu walikaa wakafikiria kwamba utajiri unakuja, wale wajasiria mali wadogo wadogo wakaanza kujipweteka, matokeo yake bidhaa ambazo zilikuwa zinakuja nchini ni bidhaa za nchi za nje. Zile ambazo zinazalishwa pale bidhaa

zile zikawa hazipo, matokeo yake wale wajasiriamali wengi wao wakawa hawana shughuli za kufanya Mungu atunusuru kufika huko ambako wao walifika. Lakini ni tahadhari kwa sababu tumejifunza kutoka kwa wenzetu lazima tuhakikishe kwamba tunatoa elimu ya kutosha ili wananchi waweze kutumia vizuri fursa hii ambayo tumeipata.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda umemaliza.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, muda umemaliza?

**Mhe. Mwenyekiti:** Ndio umemaliza.

**Mhe.Mgeni Hassan Juma:** Mheshimiwa, naomba nimalizie jengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda wako wewe umemaliza.

**Mhe.Mgeni Hassan Juma:** Mheshimiwa, naomba unipe muda kidogo nimalizie.(*Makofit*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakugaia dakika mbili.

**Mhe.Mgeni Hassan Juma:** Nataka nimalizie kwa sababu lina umuhimu wake, kwa hivyo, naomba sana nimalizie dakika mbili. Ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sana wananchi wa Zanzibar walikuwa wakililia Benki ya Wanawake, najua hii ni ndoto lakini katika kila ndoto lazima uwote ili ulipate lile jambo bila ya kuota mafanikio yanakuwa madogo sana. Naiomba sana Serikali yetu ianze kujipanga. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema hivi kwamba kuna sheria ambayo naamini kwamba itaileta hapa Barazani ambayo inashughulikia suala zima la ukusanyaji wa mapato ya uchimbaji wa gesi asilia pamoja na mafuta.

Sasa ningeomba sana katika sheria ile tuwekewe akina mama kwa ajili ya benki yetu asilimia fulani ya mapato yale ili yaweze kusaidia wajasiriamali wanawake, Mheshimiwa, katika suala la umasikini wanawake linawagusa sana, wanawake wengi ndio wanaoathirika katika suala zima la umasikini na kama tunafahamu kwa maumbile yetu sio wanawake wengi watakaoweza kushiriki katika suala zima la uchimbaji wa mafuta. Kwa hivyo, ili wanawake waweze kushiriki katika mambo mengine ambayo watakuwa na uwezo nayo, naiomba sana Serikali wakati ambapo tutakuwa tayari tunaanza makusanyo iweke

asilimia fulani ili tuweze kufaidika katika suala zima la uchimbaji na utafutaji wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, nasema tena naiunga mkono sheria kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu Wajumbe wa Baraza hili waiunge mkono sheria hii, Ahsante sana. (*Makofī*)

**Mhe. Hassan Khamis Khafidh:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii jioni hii ya leo na mimi kuchangia Mswada mahususi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, itumie spika hiyo iwe karibu na wewe.

**Mhe. Hassan Khamis Khafidh:** Kuchangia Mswada mahususi Mswada wa Mafuta na Gesi kwa maendeleo ya Wazanzibari. Kwanza nchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kadhalika kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla wake kwa kuwasilisha mswada huu muhimu.

Pili, namshukuru sana Waziri anayeshughulikia mambo haya kwa kuwasilisha Mswada mzuri uliopangika, tatu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua kwa kura nydingi kuwa Mwakilishi wao, wakulima na wakwezi kuja kuwatetea katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia ningependa kuwakumbusha msemo wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza wa kwanza mwanamke mama Margaret Thatcher alisema nanukuu; "*Oil and gas has done more waste and good to the developing countries*" Ugunduaji wa mafuta kwa nchi zinazoendelea yamefanyika mabaya mengi kuliko waliyoyatarajia yalikuwa yawe mema, lakini imeleta athari nydingi kwa nchi zinazoendelea, Na sisi Zanzibar leo tarehe 26 tumeanza kuchangia mswada wa kuwa na Sheria ya uchimbaji wa mafuta yetu kwa malengo yale yale ya Mapinduzi ya kuwalettea wananchi maendeleo yanayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya siri nchi yetu ni nchi ya kimapinduzi, lengo la Mapinduzi ni kuwalettea maendeleo wakulima na wakwezi, lakini bado ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wamo wengine ni wapinga Mapinduzi. Lakini bado ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamo watu wapinga maendeleo, ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado wamo wengine ni wezi, na leo hii tunapitisha mswada mgumu ambao utaleta rasilimali kubwa kwa maendeleo ya wakulima na wakwezi wa nchi hii. Lakini tusipoangalia na tusipokuwa makini, lazima tuache kumuonea haya mtu na kumuogopa mtu zidi

ya rasilimali hii ya wakulima na wakwezi, ni rasilimali muhimu na tukiichunga naamini umasikini Zanzibar utakuwa basi.

Kama alivyosema Mandela "*poverty is man mode*" Mhe. Mwenyekiti, tuna jukumu la kuhakikisha umasikini huu kwa rasilimali yetu hii ya mafuta umasikini Zanzibar unakuwa historia. Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, Mswada una vifungu 100 mpaka 151, lakini kifungu cha 12 cha Mswada ina bodi ya Wakurugenzi, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa, bodi ya Wakurugenzi ni kitu muhimu sana kilikuwa kitajwe na sifa za wale watu watakaoteuliwa kuwa Wajumbe wa bodi za Wakurugenzi, mswada huu haujataja sifa. Nitatoa tanbihi, aliyekuwa Gavana wa Mkoa mmoja Nigeria ambao ulikuwa una mafuta asubuhi alipoamka aliwasilisha kwa uongozi wa Nigeria wa eneo lile alimpa yule mtangazaji akatangaze huyu ndiye ninayemtaka awe Mkurugenzi wa bodi ya Mafuta ya Mamlaka hii. Akasema mbona Mheshimiwa, hujapitia utaratibu akasema "*aaa! Why you are ask me that, I say, I give the name, take the name and go name him*", akaambiwa Mheshimiwa kuna utaratibu akamuuliza "*Do you know where I got this name? I got this name from my wife,eee! Don't you know my wife is my boss, go name him*".

Mhe. Mwenyekiti, itatusaidia katika kupunguza kuwapata watu wasio na sifa naomba sheria itaje sifa za watu wa kuteuliwa katika bodi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 31, inasema; "Ndani ya miezi mitatu atawasilisha taarifa ndani ya Baraza la Wawakilishi" kifungu cha 31 ndani ya miezi mitatu Waziri atawasilisha, Mhe. Mwenyekiti, sio kuwasilisha tu, awasilishe na tuijadili, lazima iongezwe neno 'kujadili', tuijadili taarifa tuliyoipata kifungu cha 31 haina neno 'kipengele kujadili' tayari Mheshimiwa, nimetayarisha *Charge Laws of Amendment* ya kwamba, lazima iwasilishwe na tuijadili hiyo katika kifungu cha 31.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 32 cha Mswada, kuhusu kuanzishwa kwa kampuni *ZPBC*, hii ni kampuni muhimu sana kwa sababu ndio kampuni itakayotizama mali yetu Wazanzibari, itakayotizama mali ya wakulima na wakwezi, hii ni kampuni muhimu ndio itakayoingia ubia na kampuni ya kigeni ikiwa Rasil-hema, ikiwa *BP*, ikiwa nani, hii ndio yenye dhamana ya kuingia ubiya. Sasa lakini cha kusikitisha inasema pia wale watu wake hawajatajwa sifa Mhe. Mwenyekiti, zitajwe sifa zao, wawe na sifa fulani iwemo ndani ya sheria sifa zao ambao watakaosimamia kampuni itajwe ndani ya Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika ningeomba kampuni hii pia itiwe ndani ya Katiba isijekuwa kama *PBZ* kuna siku watu wakasema inataka kuuzwa, hii kampuni isije ikafika pahali ikauzwa ili wakanunua *Share* hasa ukizingatia 99% ya *Share* zote zitakuwa za Serikali, iwemo ndani ya Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, Vifungu vya 48, 51 na 59, vinamzungumzia Waziri, Mhe. Mwenyekiti, nimesema nchi hii bado mna wezi mna watu wengine si waaminifu, ni wezi, nchi hii bado kuna watu wengine wapinga maendeleo, nchi hii bado kuna watu wapinga Mapinduzi matukufu ya Januari 1964. Vifungu vya 48, 51 na 59, vinampa mamlaka Waziri makubwa sana, Mhe. Mwenyekiti, ningependekeza na hii pia imo katika *Schedule of Amendment* kwamba, Waziri asitoe leseni wala kibali chochote, baada ya kushauriwa na kampuni lazima aipeleke katika Baraza la Mapinduzi. Katika Baraza la Mapinduzi Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wengi kule, 'kauli ya wengi ni risasi'. Lakini tukimpa mamlaka peke yake Waziri, hatujui Waziri wa leo *alhamdullillahi*, dada yetu Salama Aboud keshaahidi hataki cha mtu. (*Makofit*)

Mhe. Mwenyekiti, je, Waziri ajae! Tumeona hapa Mawaziri kila kitu chake, tumeona watu walivyokuwa wezi hapa na hii tukizembeya tutazalisha wezi, leo tunashukuru Mhe. Salama Aboud, amehiji, yeye hataki cha mtu tunamshukuru sana, lakini hatujui Mawaziri wajao Mhe. Mwenyekiti, tukitoa fursa hii bila ya kupeleka Baraza la Mapinduzi, watahongwa watapitisha miswada hii, watapitisha leseni hizi kwa sababu ya kuhongwa bila ya kuzingatia kwamba hizi pesa na hii mali ni ya wakwezi na wakulima wa nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, asiamue yeye aipeleke Baraza la Mapinduzi ndio likaamue.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 61 cha mswada, kama mafuta yatagundulika na Mkandarasi, Kampuni itapewa taarifa naomba tufahamiane, ile Kampuni ya Zanzibar itataarifiwa na Kampuni ya Mkandarasi kwamba Kampuni ya ndugu yangu Abdalla Diwani tumegundua mafuta. Kampuni ya Zanzibar ndio itakayomwambia Waziri kwamba tumegundua mafuta, halafu Waziri yeye ndio atatoa taarifa kwa vyombo husika. Mhe. Mwenyekiti, hapa ni *wrong*, unajifunza nini, unachojifunza kumbe hii Kampuni haishirikiani na Kampuni ya Mkandarasi, Kampuni ya Kigeni. Kampuni ya Kigeni unachojifunza inafanya kazi peke yake, ndio maana itapata *room* ya kumuhadithia tu kwamba mafuta tayari tushayagundua.

Kwa hivyo, ninachokiomba Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya Mkandarasi ya Kigeni ifanye kazi bega kwa bega na Kampuni ya Zanzibar. Kwa sababu Kampuni ya Zanzibar ndio yenyenye jukumu la kutulindia mali yetu. Lakini inapongojewa kupewa taarifa kwa maneno ya kileo itapigwa bao, hao

Makandarasi wengine si waaminifu ni wezi, lakini ndio hatuna budi lazima tuwe nao kwa sababu ya uwezo aliotujaalia Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hiyo naomba Kampuni ya Zanzibar ifanye kazi bega kwa bega, sheria ilazimishe Kampuni ya Zanzibar kufanya kazi na Kampuni ya Kigeni kwa sababu ndio yenye jukumu la kutulindia mali yetu, wasingoje kupewa taarifa, wakifanya kazi kwa pamoja kinachogundulikana na wao watajua, kimegundulikana vipi na kila kitu. Lakini kwa kupewa taarifa Mhe. Mwenyezekiti, hapo maneno ya leo tutapigwa bao.

Mhe. Mwenyezekiti, kifungu cha 91. Katika kipengele muhimu cha mswada huu wenye 1 mpaka 151 ni 91 kwa sababu kinazungumzia wananchi, mwananchi yejote ambaye ataondolewa maisha yake ya kawaida kama alikuwa analima, anavua na anafanya nini katika eneo lililogunduliwa mafuta atalipwa fidia.

Mhe. Mwenyezekiti, nilikuwa nasema asilipwe *one go* fidia, alipwe *sustainable* fidia, yaani fidia endelevu kwa maisha yake, maadam Kampuni ile inaendelea kupata na mwananchi aendelee kupata au ukoo ule uendelee kupata. Tumeona hapa Chwaka, Uroa, Marumbi walivyouza maeneo ya bahari na leo hii wazungu wananeemeka, lakini sisi ndugu na jamaa zangu kule Chwaka na Uroa wao bado maskini kwa sababu waliuza minazi yao tu kwa kukosa ubia, lakini wangeingia ubia kama Mauritius na nchi nyengine, leo jamaa zangu Chwaka, Uroa na Marumbi bado wangeendelea kupata kila faida inapoingia kwa mzungu aliyewekeza katika hoteli. Mhe. Mwenyezekiti, napendekeza sana katika kifungu cha 91, asilipwe fidia aondoke, alipwe fidia *sustainable* neno la Kiingereza ni 'endelevu'.

Mhe. Mwenyezekiti, Kampuni yoyote ile inayokuja kutafuta mafuta hapa Zanzibar lazima ioneshe historia, sheria ioneshe historia imefanya wapi, imefanikiwa vipi, lazima ioneshe *track record* yake, isije tu Kampuni ikasema mimi nataka mafuta kwa maneno tu, lazima ioneshe rikodi na Kampuni inayotaka kuja Zanzibar ifatilie ione rikodi zake ni sahihi. Kama si hivyo Mheshimiwa, tutapata kampuni hewa tele hapa. Nasikia Wizara ya Fedha tumempata fundi mabomba kenda kujenga nyumba huko Pemba na jumba limeanguka leo. Hayo yote lazima tuyaone leo kabla ya kesho.

Mhe. Mwenyezekiti, chengine muhimu hakuna kitu kibaya ambacho Waafrika tunaingia mkenge kama katika kusaini mikataba, hii inatokana na nini, inatokana na uelewa mdogo wa mikataba. Mhe. Mwenyezekiti, naomba sana mikataba tutakayotaka kuingia ni lazima tutafute wataalam, bora tukakodi kwa pesa zozote zile lakini wawe wataalam kuja kutusaidia katika kuingia mikataba, ili mikataba

ile tunayoingia kwa niaba ya wananchi wakulima na wakwezi iwe tunapata, isiwe tunaingia mikataba badala yake tunakuja kuliwa sisi.

Mhe. Mwenyekiti, mikataba ni kitu muhimu tumeshuhudia nchi za wenzetu nyangi zimeingia mikataba, mikataba ile kumbe haineemeshi nchi hasa ukizingatia kuna wachache wengine huingia mikataba kwa niaba ya Serikali, lakini kumbe kwa sababu wameshapewa 10% wanaingia mikataba ile kwa kuitosa Serikali. Tumeshuhudia mikataba mingi Tanzania na nchi nyengine, sasa mikataba Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tujifundishe mikataba, tuisome na bora tukakodi Kampuni zije kushirikiana na sisi katika *ku-sign* mikataba, kwa kunusuru Mhe. Mwenyekiti, mali ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniambia lakini muda wangu bado dakika nne, tano ninaziona, watu walisema mengi kwamba mafuta hayachimwi, itakuwa hivi, hakuna, lakini Mhe. Mwenyekiti mafuta kumbe tunayo *Shell, BP, Ras al-Khaimah* na wengine wasingehangai kila uchao kujifanya kusaidia, kujifanya wanatoa, yote wanayavizia mafuta aliyyojaalia Mwenyezi Mungu mwaka huu wakwezi na wakulima na wao wapate kufaidika na neema hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri, sisi Wajumbe wa Baraza la Tisa la Wawakilishi tunayoyasema yote kwa lengo moja tu, kwa lengo la kuiletea maendeleo Serikali yetu kwa niaba ya maendeleo na lengo la Mapinduzi mahususi la kuwaletea maendeleo wakulima na wakwezi.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Welezo ninaunga mkono mia juu ya mia mswada huu wa Sheria ya Mafuta na Gesi uliowasilishwa katika Baraza la Mapinduzi tunaujadili leo tarehe 26/09/2016.

Mhe. Mwenyekiti, leo ni siku ya historia kwa Zanzibar tunapitisha na kujadili mswada wa mafuta, raslimali ya Wazanzibari itakayotuletea maendeleo. Nawaomba na wenzangu kuipitisha sheria hii, halafu tumuone huyo mtu aje aseme sasa, kisima changu hivi, nchi yetu sisi bwana hatukuipata kwa bendera shusha, bendera pachika, aa, sisi tumeipata kwa Mapinduzi. Sasa atakaesema pake au hapa pangu tutakuwa tuna uwemo kabisa wa kumfata kupambana nae popote pale alipo, mafuta ni yetu tutumie kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo naunga mkono mia juu ya mia katika kutumia raslimali yetu hii aliyojualia Mwenyezi Mungu. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu. (*Makofii/Kicheko*)

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliényiwezesha kusimama hapa na nisipoteze muda ukaja ukamaliza haraka. Kwanza niipongoze Serikali kwa nia njema na nia nzuri, lakini vile vile Serikali naweza kusema hapa imefanya haraka na mswada huu wakati muda tunao tukakaa tukaujadili, tusiwe na haraka muda tunao wa kutosha. Vyengine vyote, tuangalie na athari zake huko mbele zikoje, lazima Mhe. Mwenyekiti, hapa tuwe wakweli na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, naomba unisikilize kwa makini na wewe ndie utayesaidia.

Waheshimiwa Wajumbe, nilipokuwa nikisoma mimi skuli nitoe historia yangu ndogo tu, nilipewa *home-work* nikawa sijaifanya, siku ya pili mwalimu anakagua mabuku nikachukua *cover* ya Mhe. Raza, nikabadilisha tu, buku lile katika *cover* yangu. Akanambia mwalimu mbona leo una hati nzuri, mtihani mkubwa huu, buku langu ni hili hapa lakini naogopa bakora asubuhi mapema sijafanya *home-work*, nikachukua buku la Mhe. Raza, nikabadilisha *cover* tu nikaandika Jaku Hashim, anakagua mwalimu ananambia mbona Jaku leo una hati nzuri kama hizi, kumbe hati za Mhe. Raza, ulikuwa mtihani, mwalimu alipofungua *cover* anakuta jina la Mhe. Raza, nilichezea mikwaju mikubwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu, nisikilize kwa makini kama upo, tunaanza na huu ukurasa wetu, unajua haya mambo ya ku-*copy* yana hasara zake na faida zake. Waheshimiwa Wajumbe, hebu tuukamate huu mswaada tuuangularie mwanzo kabisa, Zanzibar 16 Mei, 2014 kosa kubwa sana hili, la ajabu Serikali ilikuwepo wapi, haya mambo ya ku-*copy* yana hasara zake na haraka, ndio hii hasara, uangalieni mswada jamani 16 Mei, 2014, mswada mwanzo una haraka na makosa hayo hapo. Kwa hivyo, ninachokijadili hii haraka haraka, ndio yale niliosema siku moja naandika nachukua buku nakuja ku-*copy* baadae nikapigwa mikwaju, ni hatari hii.

Lakini jengine mswada kama huu wenye vifungu mpaka 150, hata Kanuni zinatueleza yaliyomo, utakitafuta kitu hapa siku mbili hujakiona, haya mambo ya ku-*copy* yana hasara zake. Nia ya Serikali narudia tena ni nzuri, yaliyomo humu hamna, hata hizi kanuni zetu za Baraza, hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano utaangalia ukurasa wa ngapi utapata kitu, ada ya vikao vya Bunge ni ukurasa wa 94, Kamati za Bunge ni ukurasa wa 96, sasa utatafuta kitu kwa misingi gani. Serikali imefanya haraka kuleta Msaada huu, nia narudia tena ya Serikali ni nzuri, lakini unakuja kutwambia 16 Mei, 2014 hapa mapema, Mwanasheria Mkuu, unaishauri vipi Serikali hapa sijui kama yupo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, zungumza na kiti.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini yaliyomo yako wapi mswada kama huu utatafuta kitu kiko wapi. Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu vitatu, Serikali, Bunge na Mahkama ni mihimili mitatu ya Serikali. Baraza wajibu wetu kuisimamia Serikali na kuihoji kwa nia njema tu kabisa, huu ni wajibu wetu. Serikali kazi yake kushughulikia ma-cabinets, civil services, Polisi na wengineo na Mahkama tunachokipitisha hapa tukaunda Serikali, Serikali inapeleka Mahkamani. *Separation of power* inayosema humu, tunafukuzia mambo, lakini kuna hasara mbele yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niliuliza swali Bungeni na jawabu nilizozipata hazijawahi kutokea, unauliza swali unanyang'anywa unapewa jawabu nyengine, unaambiwa Serikali imekosea. Hii hapa na wabunge walioko kule watasikia. Naomba ninukuu;

"Atamuuliza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Makamu wa Rais Muungano, kwa mujibu wa taarifa rasmi ya Serikali ya Mapinduzi SMZ iliyotolewa mwaka 2014 Kisiwa cha Latham Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar tangu kilipotangazwa rasmi mwaka 1898. Hata hivyo zipo taarifa zilizothibitishwa na Serikali ya Muungano kwa Ofisi ya Waziri Mkuu iliandikia SMZ kuwataarifu kwamba Kisiwa hicho ni cha Tanzania Bara. Je, Serikali haioni kuwa mgogoro huu au umiliki wa kisiwa hicho ni aibu kutokea kwa nchi moja na kuonesha kwamba kero za muungano hazijatatuliwa na ufumbuzi. *That is (a).*

(b) Kisiwa cha Latham kimepeleka vitalu namba 7 na 8 ambavyo tayari *TPDC* imeshavigawa bila ya ridhaa ya SMZ. Je, Serikali haioni mgogoro huo sio wa mipaka bali wa mafuta na gesi.

(c) Serikali inachukua hatua gani kumaliza mgogoro huo".

Nilipewa jawabu mbili hizi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mipaka ni muhimu, nataka kujenga nyumba yangu, kiwanja changu hiki nataka vyumba 60 kitatoka kweli kiwanja hiki vyumba 60. Narudia tena tunajadili mswada suala la mipaka ni muhimu, nina jawabu mbili hapa ukizitaka nitakuletea. Shamba lako unalo la mikarafuu utahitaji mipaka yake ili ujue tija yake nini? Lakini Mheshimiwa, suala la mipaka kwa Serikali limekuwa gumu, mimi nia yangu sio mbaya, ataekwenda kunihukumu hiari yake, wala sio langu hili. Mipaka kama huna huwezi kuja kufanya hata hilo shamba lako, hata nyumba kama unataka kuchora nyumba yako na kiwanja chako kidogo unataka kujenga vyumba 30, 50, mipaka utaipata wapi? Itakuwa vichekesho kwa hapa Serikali itueleze suala la mipaka. Mhe. Raza, amepiga kelele sana kuhusu

Kisiwa hiki kuna *Block No. 7* na *8* sio kisiwa na asili ya Fungu Mbaraka tuelezwé ni mali ya Zanzibar, lakini wenzetu sijui wamebakia nini.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna Kamati imeundwa na wataalam waliobobeza wakiongozwa na sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kutatua suala la mafuta na gesi ikiwemo Fungu Mbaraka, ile ripoti kwa nini hatukuletewa? Ripoti imekwenda wapi? Kwa hivyo, tunapofanya suala la mipaka kama hatukuliangalia bado. Tuangalie wenzetu hawa wa Songosongo wamegundua mafuta na gesi 1974, *Professor Muhongo* alizungumza Uingereza 2013 yamechimbwa lini, ni mwaka 2000, 2004 ndio yakaanza kupatikana. Sasa tusijaribu kurukia tu, ukirukia mwendo katika gari usioijua mwendo wake lazima ikutowe meno.

Mhe. Mwenyekiti, Tuangalie *Mnazi bay*, 1982 wamegundua, uchimbaji na process umeanza lini mwaka 2002, *Mnazi bay* Tanganyika huko lakini tukafukuzia hatuwezekani, lakini cha kichekesho Mheshimiwa, tunakwenda kwa hoja ya kikatiba, je, sheria iliyotungwa na Baraza ni kinyume na Katiba ya 1964 tuangalie inasema nini. Kwa hii hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu, angetusaidia, hii ni sawa sawa na Halmashauri ya Mhe. Haji Omar Kheri tu waziri, Manispaa inapitisha kanuni 64(3), naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

“Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inayohusu jambo lolote katika Tanzania Bara ambalo liko chini ya Mamlaka ya Bunge, sheria hiyo itakuwa batili, itaanguka na pia endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inayohusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, sheria hiyo itakuwa batili, itaanguka”.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hii, kwa hii tunayoipitisha bado, hatujawa tayari sisi. Mimi ninashangaa wizara ina wanasheria chungu nzima, kwa hivyo, sisi tukipitisha hapa ni sawa sawa na kupiga mziki tu, hii hapa na bado suala la mafuta na gesi ni mali ya Tanzania. Kwa hivyo, tunavyokwenda hivi tuliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nije mpaka wa *Exclusive Economic Zone (EEZ)* imesema nini; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, imejifunga, zikubaliane itumie kwa pamoja, lakini Mhe. Mwenyekiti, cha kushangaza tena kifungu cha 2 cha Sheria ya Tanzania Bara kinachohusu matumizi hakijaeleza suala la mipaka ya Serikali mbili katika suala la mafuta, ugawaji wa vitalu ni muhimu Mheshimiwa, suala la mipaka lina umuhimu wake kama hatukuzingatia hii itatufikisha pahali pabaya. Narudia tena mara ya tatu, nia

ya Seriakali ni nzuri, lakini mswada wakati wake bado lazima tukajipange, kuna suala la *TRA* hapa hayo yote tukayapitisha, kuna kodi *TRA* tukishakupitisha, *TRA* ni chombo cha Muungano, tutayapanga yote haya, ni sawa sawa na kupika pilau nzuri ikaja ikadondokea mafuta ya taa tu tena toje moja tu. Bado suala tunatengeneza njia lakini matokeo yake *TRA* suala la Muungano, na humu yamo mambo ya *TRA* katika mpango huu kuwa bado sheria tunayoipitisha suala ni zito, hatuwezi kufika nayo huko.

Mhe. Mwenyekiti, Tuangalie fidia kwa jamii vile vile. Kifungu cha 99, *community* itaathirika vipi, hapa haikueleza usumbufu wananchi wataoupata, kama mfano wananchi pale Tundauwa watakenda kuchimba mafuta, wananchi wale shughuli zao zitapotea watafidiwa vipi wananchi wa Tundauwa. Haya mambo tuyafanye tuyaa ngalie msije mkafika mkatuuhukumu na mkatua hivi, lakini nia ya Serikali narudia tena na tena ni nzuri, lakini mswada tumefanya haraka, muda tunao tuombe uhai tu. *Mnazi bay* nimewataja, Songsongo nimewataja miaka mingapi imechukua kwa uchimbaji wa mafuta. Lakini Katiba hii, sasa tunapitisha kanuni tu, kwa yote tunayopitisha hapa tutagongwa na Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano ndio itayotugonga, tuwe tunapiga kelele tunaambiya Fungu Mbaraka mali yetu, mali yetu, huku inatolewa bila kushirikishwa. Kwa hivyo, tunapokwenda tujuwe tunachokitenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningefurahi hasa Mwanasheria Mkuu mwenyewe alikuwa awepo, lakini bahati mbaya hayupo. Mimi si mtaalamu wa sheria, lakini tunapitisha Kanuni, Katiba tunayoizungumza hii hapa inatusokota wenyewe ya 1964, kwa hivyo, tunachopitisha hapa ni Kanuni, sawa sawa na Halmashauri tumekaa tu hapa, tutafanya nini. Masikitiko makubwa Mhe. Mwenyekiti, tunafanya kitu kwa nia safi, lakini tunapokwenda suala la *TRA* la Muungano humu zimo, kwa hivyo, tukisha kupanga haya mambo kuna kodi huko *TRA* watakuja kutupangia vizingiti vyengine, hatujui tunachokifanya. Bado suala la mafuta halijaondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano mpaka Katiba tuipitishe Mungu akitujaalia panapo uhai. Mimi ninashangaa tunafukuzia mwendo hatuujui.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie hapo wala nisipoteze muda na majawabu mawili haya niliojibowi Bungeni, nauliza swali naambiwa Serikali imekosea napewa jengine hii hapa karatasi na kama utaniruhusu kusoma ninazo nilizopeleka Bungeni, maana yake haijawahi kutokea msiba mkubwa unauliza unaambiwa Serikali imekosea kweli hatujui tunakoelekeea, tunafanya nini, ikaja neema haichagui aliyekuwemo na asiyekuwemo atapata, ikaja dharuba ya Mwenyezi Mungu inafyagia tu. Tunazungumza kwa nia njema kabisa, ndio nimesema tuna mihimili mitatu; Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama,

kuwa tupo hapa kuihoji na kuisimamia serikali kwa nia njema, sio ikafika pahali Waswahili wanasese; "hoi hoi nacho kilindo". Mhe. Mwenyekiti, nililia mimi humu katika bajeti ya Wizara ya Afya nikaonekana kama anafanya uchepe au muongo...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda wako umebakia dakika moja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Rais, juzi ametoa 1.6 bilioni tumshukuru kuisaidia sekta ya afya kwenye madawa, kama hatukupiga kelele sisi wawakilishi, tungefika wapi. Mimi nimtakie afya njema Dkt. Ali Mohammed Shein, umri mrefu na tuweze kuendelea. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

## UTARATIBU

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Mwenyekiti, asubuhi na mapema nililetile barua yangu na Mwenyekiti alipomaliza muda wake akasema ana wachangiaji wanane, anamaliza asubuhi wachangiaji wanane nikiwemo na mimi na tokea asubuhi sijatoka, niko hapa mpaka sasa hivi tushakuwa na wachangiaji 16. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba utaratibu na kanuni.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sijakupata neno lako la mwisho.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Mwenyekiti, Nataka muongozo wako wa kiti, kwa sababu Mwenyekiti, alipotoka kasema kuna wawakilishi wanane na mimi sikutoka toka asubuhi mpaka sasa hivi wameshafika kumi na sita. Sasa nataka ukweli wako wewe Mwenyekiti, muongozo na utaratibu, kila imoja ana demokrasia ya kuzungumza, sio kila anayepepesuka mlevi. Kwa hiyo, tuelezane huyu wa kumi na sita na wengine nimeona kwa macho yangu wanaandika wanakupelekeea na unawaita, kwa macho nimeona wameandika sasa hivi umewaita. Ahsante sana Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa, nimekuelewa na nimekusikia muda bado upo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mswada huu wenye anuani ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, na kuanzisha mamlaka yanayohusiana na jambo hilo. Nimesimama hapa kwa niaba ya

wananchi wangu wa Jimbo la Mkoani, Pemba kwa ajili ya kutoa maoni juu ya mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mswada huu una sehemu nyingi, mimi nimeusoma, pia nimeusoma pamoja na sera yake kwa kweli mswada huu umeonesha ubora na unaweza kukidha matakwa na mahitaji ya jamii yetu. Lakini wakati tunauptisha mswada huu tuelewe kwamba wananchi wetu wanatafsiri nyingi juu ya zoezi hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Kuna tafsiri zilizo sahihi, kuna tafsiri zisizo sahihi, ni wajibu wetu sisi sote kubuni njia ya kuwaelimisha wananchi wetu tokea awali.

Wenzangu wengine walisema ni kutoa taaluma, lakini mimi nasema ni kutoa elimu, kwa maana ya kwamba kupata maarifa ya jumla jumla juu ya suala hili la mafuta na gesi hasa katika kipengele kinachohusiana na jamii, utamaduni na uchumi unaohusishwa na suala la mafuta na gesi. Wananchi wetu wengi wao hawana haja ya kujua *chemistry* ya mafuta, mafuta yanatokana na *hydrocarbon*, lakini tunapaswa kuwaelimisha kuna faida gani ya kijamii itapatikana katika zoezi hili, pia kuna faida gani ya kiutamaduni itapatikana, lakini pia kuna faida gani ya kiuchumi itapatikana na kinyume chake, lazima tuwaelimishe tokea mwanzo faida na hasara ambazo zitatokana na zoezi zima hili. Kuna wenzetu wamejenga matumaini makubwa na bila shaka ni sawa, lakini matarajio hayo yanapaswa kudhibitiwa.

Pia, kuna wenzetu wengine wamekata tamaa sana juu ya suala hili nao pia wanapaswa kudhibitiwa kwa kutoa elimu. Lakini suala la kutoa elimu limekuwa tukilitaja jumla jumla tu, tuijilize je, hizi njia ambazo tunazitumia sasa katika kupashana taarifa zinfaaa kwa ajili ya zoezi hili la kutoa elimu la mafuta na gesi. Tumekuwa tukitaja vyombo vya habari, wengine wamependekeza kuundwa pengine kitengo maalum cha kutoa taarifa hizi, na wengine wamekuwa wakitoa maelezo mbali mbali ya kuanzisha mitaala katika skuli, je, zinfaaa, hilo ni muhimu sana.

Kwa hivyo, ni busara kuanza kujadiliana na mapema ni mkakati gani bora tena wa kudumu ambaa utasaidia kutoa elimu kwa wananchi wetu kwa madhumuni ya leo elimu juu ya mafuta na gesi asilia, lakini kwa kweli ni elimu juu ya masuala yote yanayohusu jamii.

Kwa hivyo, ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, kuweka mikakati sahihi juu ya utoaji elimu, wenzetu wengi ambaa walioingia katika uchimbaji na utafutaji mafuta katika mataifa mengine walishindwa katika kipengele hiki cha utoaji wa taarifa. Taarifa hizi lazima zimfikie kila mwanajamii ili apate uhakika wa

jambo lilivyo, kama hatukuwa imara baadhi ya wakala wanaotoa taarifa katika jamii zetu wanaweza wakashinda na kuweza kuidhoofisha taarifa sahihi za serikali. Kwa hivyo, hili ningeliomba tupate muda tulijadili hasa kwa kina nadhani ni *best strategy* ni ipi ya kutoa taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la kuwataarisha wananchi wetu kuwa tayari katika zoezi hili la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia mapema, tuwafanye wawe tayari. Hii ni nyongeza tu kwamba utayari wa wananchi utapatikana pale ambapo patakuwa wana taarifa sahihi, kama hawakupata taarifa sahihi utayari wao unaweza ukawa wa chini na tukaanza kupingana mapema kabisa, hili ni suala muhimu. Ni vyema wakaelewa kwamba zoezi hili linawezekana likawa la muda mrefu, linaweza likawa na muda mfupi, sasa hivi watu wengi wanadhani pengine tukipitisha sheria kesho na kesho kutwa tayari mafuta yanapatikana, kumbe tuko katika zoezi zima la utafutaji kwanza mpaka tutapoyagundua wa kima na wingi unaotakiwa wa kibashara ili tuweze kufanyakazi. Kwa hivyo, tuwaelimisha wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika kuelimisha wananchi wetu tuwaeleze suala la muda kwamba zoezi lenyewe linaweza likawa la muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi tuwaeleze ili wajue. Tuwaeleze masuala ya faida, je, zoezi hili litaweza kuleta faida gani kwa jamii, faida gani kwa mtu binafsi na faida gani kwa taifa. Hili ni muhimu sana kuelimishana mapema.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia jambo jengine muhimu sana ni suala la taarifa juu ya kazi, tutoe elimu juu ya kazi, wananchi wetu karibu wote wanadhani kwamba mafuta yatakayopatikana wote wataweza kupata ajira za moja kwa moja juu ya suala la mafuta. Kwa hiyo, tuwaweke sawa kwa kutoa taarifa sahihi, bila shaka ziko tafasi za kitaalamu wenye utsalamu huo bila shaka wanaweza kupata, lakini pia kuna nafasi nyengine za nguvu wanaweza kupata lakini sio wote, kwa hivyo, lazima tuwaelimisha mapema kabisa ili huko baadae tusijeingia kwenye migogoro na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, tuwaeleze katika kuwaelimisha ugumu wa kazi hii, kuna wengine wanadhani labda uchimbaji na utafutaji mafuta ni kazi nyepesi. Ni kazi ngumu sana na tuwaelimishe ugumu wenye na wajue. Pia, kuna sehemu nyengine ni za rahisi sana tuwaelimishe pia nao wazijue, lakini kubwa zaidi tuwaelimishe penye hatari ya kazi zinazohusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kwamba tuanze kuwaelimisha wananchi wetu juu ya kujenga uchumi unaotegemea mafuta, lakini wakati huo huo tuisahau kuendeleza shughuli nyengine za uchumi katika taifa. Tukikosea hapa mnaweza kushtukia pengine watu wote wameacha shughuli nyengine na tumejiingiza katika suala ambalo pengine hatimae linaweza likaathiri mwelekeo wa uchumi wetu. Kwa hivyo, lazima tuweke *balance* katika kutoa elimu juu ya mafuta na gesi asilia, lakini pia tuisahau kutoa elimu juu ya kazi nyengine za kiuchumi ambazo wanafanya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nimeisoma kwa makini sheria yetu, nimesoma kwa makini sera zetu, haya ni mambo muhimu sana katika suala la uwekezaji na tuelewe kwamba hata sisi wenyewe wawakilishi, tuelewe kwamba suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta ni suala la uwekezaji kwa kweli. Sasa uwekezaji mara zote wanajaribu kuangalia ubora wa sheria zetu, ubora wa sera zetu katika tasnia hii ya uchimbaji na utafutaji wa mafuta. Kwa hivyo, mimi sina mashaka na sheria zetu na sera yetu, lakini hivi peke yake bado havijatoa ushawishi wa kutosha kwa wawekezaji. Kuna jambo jengine muhimu lazima tulitilie mkazo nalo ni suala la kuendeleza utulivu katika nchi yetu.

Hili ni suala muhimu sana ili wawekezaji wapate moyo wa kuekeza fedha nyingi hasa kwa kuelewa kwamba mitaji hii inahusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta ni mitaji ambayo inachukua fedha nyingi, kwa hivyo, tunahitaji utulivu. Lakini kubwa zaidi tunahitaji viongozi wetu, wananchi wetu tuwe na kauli njema juu ya uwekezaji, hili nalisisitiza tuwe na kauli njema, ikiwa tuna kauli zenyenye kubadilika hizi pia zinakatisha tamaa wawekezaji. Kwa mfano, leo tumeshasema hivi, kesho pengine mtu aseme hatutaki, kesho kutwa tunataka, kesho tufanye hivi, kauli hizi zinaathiri uwekezaji. Kwa hivyo, mara tutapoupitisha huu sote tuwe na kauli moja kwamba yakuhimiza uwekezaji katika tasnia hii ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, pia, tunahitaji kuwa na sheria nyengine zisizohusiana na mafuta na gesi lakini nazo pia zinahitaji kuwa nazo ziwe rafiki kwa wawekezaji. Kwa mfano, sheria zinazosimamia kodi na sheria nyengine ambazo zinasimamia uchumi kwa jumla nazo pia inabidi tuzitizame upya kama hazikidhi basi tuzifanyie marekebisho na kama zinakidhi basi tuendeleze kuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji pia wanahitaji na wanachunguza taasisi zetu uwezo wake na hapa wanaangalia zaidi suala la taasisi zenyenye kuwajibika, ufanisi na zenyenye kufanya kazi kwa wakati. Najua sheria imeelekeza kuundwa kwa mamlaka, kwa hivyo, mamlaka hiyo inatarajiwa kwa kweli ifanye kazi

kwa ufanisi mkubwa sana, na hili lazima tulisimamie kwa karibu sana, ufanisi na uwajibikaji unapokosekana kwa kweli tutawa-*frustrate* wawekezaji katika tasnia hii na kwa hiyo, tutaathiri kabisa sekta nzima hii ya uchimbaji wa mafuta. Kwa hivyo, niseme kwamba tunahitaji kufanya kazi kama anavyosema Mhe. Rais, tusifanye kazi kwa mazoea, tubadilike, lazima tuwe wabunifu na ndio maana sekta hii ya uchimbaji na utafutaji wa mafuta tutaifanya haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nimalizie katika suala la kuwapongeza viongozi hawa wa wizara hii ambao tokea awali walifanya kazi ya kitaalamu, walifanya kazi ya kisiasa ambayo kwa kweli matunda yake tunayo leo hii hapa. Mimi binafsi sina wasi wasi na waziri tuliyenae, ni mtu salama na nina hakika atasimamia tasnia hii kwa salama.

Mwisho kabisa nirejee tena kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu. Ahsante sana. (*Makofit*)

**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi (Makoti):** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji waliokwisha kuchangia mada hii nzuri kabisa ya gesi asilia ambayo tunategemea kuwa nayo nchini kwetu hapa. Ni mawazo yaliyotawala dunia sasa hivi kwamba mafuta na gesi ni chanzo kikuu cha uchumi, wenzangu wengi hapa wamechangia, wengine wamejaribu kutahadharisha kwamba tusije tukaingia kwenye mafuta na tukasahau mengine. Sasa nawaunga mkono sana, nafikiri nchi ya Nigeria lilitokea tatizo hilo kwamba wao walithamini sana mafuta wakasahau kilimo, wakasahau na mambo mengine, matokeo yake walitetereka kwa kiasi fulani. Kwa hiyo, nawaunga mkono wale waliosema kwamba mafuta tusije tukategemea hayo tu na nyenzo nyengine za uchumi tuziendeleze kama kawaida.

Sasa baada ya kusema hayo, nadhani nianze kwenye hii shughuli yenye we ya mafuta, na nizungumze kwa jamii yale ambayo kwa kweli yanahitaji kuzingatiwa ili jamii iende sambamba na uchimbaji huu wa mafuta. Kwanza thamani ya shughuli au kuthaminika kwa kushughuli yenye we kwa wananchi. Shughuli hii itathaminika sana kama wananchi watahasi kuwa mafuta haya yanawahusu, wenzangu walisema waelimishwe nakubali. Pia, wataithamini sana hii kama mafuta haya yanayozalishwa yatazalishwa ya kutosha kwa faida ya wananchi na nchi kwa jumla.

Pia, watathamini sana kama uchimbaji huu utakuja kuendelea kuchangia maendeleo ya nchi. Vile vile, utathaminika sana kama uchimbaji utakwenda vizuri na utakuwa wa kiushindani, nayo itakubali hivyo kama itakwenda

sambamba na mahitaji ya jamii. Pia, kama utaendeshwa bila ya upendeleo kwa umahiri na kwa umakini sana. Vile vile, utathaminika kama utaendeshwa kwa heshima inayostahiki.

Sasa lazima kuwe na mwelekeo wa haki na wajibu kwa shughuli nzima ya uchimbaji wa mafuta na lazima iende sambamba na mahitaji ya wananchi. Hii ni kwa sababu wapo watu wasiopendelea maendeleo ambao wanaweza wakafanya mambo ambayo yatakuwa ni kichume na uchimbaji wa mafuta wakawavunja moyo watu, wakawashawishi hata wawekezaji ikawa vurugu tupu na mafuta hayachimbiki.

Halafu na nguvu za kisiasa tuzitumie kwa sababu sera zetu za CCM zinasema kwamba tuondoe umasikini kwa wananchi, sasa nguvu hizi pia zilenge kwenye kuimarisha mawazo ya kimaendeleo ya wananchi kwenye masuala ya mafuta. Ziimarishe uwajibikaji kwa wananchi wote na kuwawezesha kuleta maisha bora. Sasa baada ya kuzungumza mwelekeo huo naomba sasa niende kwenye mambo ambayo nayahisi yamekosekana kwenye hii *document* yenye. Ni *document* nzuri sana na naiunga mkono asilimia mia juu ya mia, lakini nahisi kwamba madamu tunazungumzia mambo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta kuna jambo la *refining*, yaani kuya-*refine* haya mafuta halikutajwa kwenye hii shughuli ya Sheria za uchimbaji wa mafuta.

Nadhani itakuwa ni jambo la busara kuweza kuingiza na *refining*, hata kama mafuta yenye tunatafuta maana yake sasa hivi tunatafuta na tunaeleza juu ya utafutaji huo na uchimbaji. Sasa tutakopochimba basi bila shaka kutakuwa na *refining* au kama hakuna *refining* basi pia ileezwe hapa hatutafanya *refining* na tutauza mafuta haya kama *crude oil* na tutakapoeleza kwamba yatafanyiwa *refining* basi waeleze yatakayopatikana bila shaka kutapatikana *diesel*, kutapatikana girisi, kutapatikana lami, kutapatikana hiyo *petrol*, *kerosene* na mengi mengine yangeingizwa hapa kwenye hii sheria yetu ili nayo yawe yamefafanuliwa vile ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kwa kweli shughuli hii ya uchimbaji wa mafuta inastahiki iwepo na sote wawakilishi sote kama tulivyokwisha kuambizana wale waliochangia tunapaswa kuiunga mkono mia kwa mia kwani itapunguza kwa kiasi kikubwa umasikini ambao kwa baadhi ya watu umekithiri sana. Kwani matatizo ya kiumasikini tunajua kwamba umasikini unatokana na matatizo ya kiuchumi, matatizo ya kijamii, matatizo ya kisiasa, matatizo ya hisia za watu tu, matatizo ya kisera, matatizo ya nyenzo, matatizo ya maarifa hayo, maarifa mafupi na ukosefu wa nafasi ya kuwasaidia

kupata njia za kujiedeleza na tukipata mafuta haya, matatizo haya yote yataweza kutatuka.

Kwa hiyo, nasema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtopepo kwa sababu najua na kule matatizo ya maji, matatizo ya barabara, matatizo mengi sana yataweza kutatuka, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Narejea kusema kwamba nawoomba wawakilishi wenzangu tuunge mkono kwa maana jambo lolote litakalosaidia kuimarisha uchumi inafaa tulunge mkono kwa pamoja na kwa nguvu zote. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii na naiombea kheri wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, iendelee na kuimarisha shughuli hii ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta ili tuweze kufaidika haraka iwezekanavyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yenu na utulivu wenu mliokuwa nao kwa muda wote huo katika kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu. Naomba niwatangazie kwamba katika orodha yangu ni wajumbe 7 ambaao hawajachangia kwa vile kila ambaye anajua amejiweka katika orodha hii wakiwemo mawaziri hawa watamalizia kesho tukijaaliwa. Baada ya maelezo hayo naomba nilahirishe Baraza hadi kesho mnamo saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza lilahirishwa hadi  
tarehe 27/09/2016 saa 3:00 asubuhi)*